



كنز العرفان في ترجمة القرآن

Tafsiri rahisi ya Quran

سُورَةُ الْبَقْرَةِ

Ng'ombe

(Swahili)

مع حاشية افهاماً القرآن

Pamoja na Ufanuzi juu ya ufahamu wa Qur'an

Mufti Muhammad Qasim Qadiri Attari

*Imetafsiriwa na
Idara ya Tafsiri (Dawat-e-Islami)*

1. Sura
Al-Fatiha
Ufunguzi 5

(Sura hii ni Makkiyah,
yenye sehemu 1 na aya 7)

اٰسُورَةُ الْفَاتِحَةِ مَكِّيَّةٌ ۝
أَيَّاتُهَا: ۱ رکوعها:

Kwa jina la Mwenyezi Mungu, Mwingi wa Rehema, Mwenye kuhurumia.

بِسْمِ اللَّهِ الرَّحْمَنِ الرَّحِيمِ

الْحَمْدُ لِلَّهِ رَبِّ الْعَالَمِينَ ﴿١﴾

الْمَنْزِلُ الْأَوَّلُ ۚ ۱

1:1 **Sifa** njema zote ni za Mwenyezi Mungu,
Mola Mlezi wa walimwengu wote.

رَحْمَنِ الرَّحِيمِ ﴿٢﴾

1:2 Mwingi wa Rehema, Mwenye kuhurumia.

مُلِكٌ يَوْمَ الدِّينِ ﴿٣﴾

1:3 Bwana wa Siku ya Malipo.

إِيَّاكَ نَعْبُدُ وَإِيَّاكَ نَسْتَعِينُ ﴿٤﴾

1:4 **Wewe tu** tunakuabudu na Wewe tu tunakuomba msaada.^①

إِهْدِنَا الصِّرَاطَ الْمُسْتَقِيمَ ﴿٥﴾

1:6-7 **Njia** ya wale uliowaneemesha, sio ya wale waliokasirikiwa, wala ya wale waliopotea.^③

صِرَاطُ الَّذِينَ أَنْعَمْتَ عَلَيْهِمْ لَا غَيْرُ الْمَغْضُوبِ عَلَيْهِمْ وَلَا الضَّالِّينَ ﴿٦-٧﴾

يَعِ

Mada

- Sifa na pongezi ni za Mwenyezi Mungu Mtukufu.
- Kumuabudu Mwenyezi Mungu peke yake na kutafuta msaada kutoka Kwake.
- Dua ya kutembea kwenye Njia Iliyo Nyooka.
- Njia Iliyo Nyooka ni njia ya watu wema.

Maoni

^① Kimsingi, Mwenyezi Mungu Mtukufu ndiye Msaidizi wa asili, kwa vile Yeye ndiye mwenye uwezo wa asili, umiliki wote ni Wake, hamtegemei wala hamhitaji yeyote. Watu wateule wa Mwenyezi Mungu Mtukufu husaidia tu kwa kupewa uwezo kutoka kwake. (*Angalia ufafanuzi wa aya hii katika Tafsīr Sirāt al-Jinān kwa maelezo zaidi.*)

^② Hii inarejelea “njia iliyonyooka ya itikadi” iliofuatwa na Mitume au “Njia iliyonyooka ya Uislamu” iliofuatwa na Maswhahaba na watangulizi wema.

^③ Wale waliopata "ghadhabu" ya Mwenyezi Mungu Mtukufu ni Mayahudi na waliopotea ni Wakristo au watu wenye imani potofu.

2. Sura
Al-Baqarah | (Sura hii ni Madaniyah,
yenye sehemu 40 na aya 286)
Ng'ombe 87

٢ سُورَةُ الْبَقَرَةِ مَدَنِيَّةٌ ٨٧ | أَيَّاتُهَا: ٢٨٦ - ٣٠ | رُكُوعُهَا: ٣٠ | الْجَزْءُ : ١

Kwa jina la Mwenyezi Mungu, Mwingi wa Rehema, Mwenye kuhurumia.

بِسْمِ اللَّهِ الرَّحْمَنِ الرَّحِيمِ

2:1 Alif. Lām. Mīm.^①

الْمَ

2:2 **Kitabu** hicho kilichotukuka hakina shaka ndani yake; uwongofu kwa wamchao Mwenyezi Mungu.

ذَلِكَ الْكِتَبُ لِرَبِّيْبٍ فِيهِ هُدًى لِلْمُتَّقِيْنَ ۝

2:3 **Ambao** wanayaamini ya ghaibu, na wanasmamisha Sala, na wanatoa (katika njia yetu) katika riziki tulizo waruzuku.^②

الَّذِينَ يُؤْمِنُونَ بِالْعَيْبِ وَيُقْيِمُونَ الصَّلَاةَ وَمَنْ

سَرَّأْتُهُمْ يُنْفِقُونَ ۝

2:4 Na wanayaamini yaliyo teremshwa kwako na yaliyo teremshwa kabla yako,^③ na wana yakini na Akhera.

وَالَّذِينَ يُؤْمِنُونَ بِهَا أُنْزِلَ إِلَيْكَ وَمَا أُنْزِلَ مِنْ

قَبْلِكَ وَبِإِلَّا خَرَقُوهُمْ يُؤْفِقُونَ ۝

2:5 **Watu** hawa wamo juu ya uwongofu utokao kwa Mola wao Mlezi, na watu hawa ndio wenye kufaulu.

أُولَئِكَ عَلَى هُدًى مِّنْ رَّبِّهِمْ وَأُولَئِكَ هُمُ الْمُفْلِحُونَ ۝

Mada

- Quran ni kitabu cha mwongozo ambacho hakina mashaka ndani yake.
- Sifa za wachamungu.
- Malipo ya wachamungu, uongofu duniani na kufaulu Akhera.

Maoni

^① Herufi hizi ni siri za Mwenyezi Mungu Mtukufu na zinatokana na Aya za mutashābihāt (ambazo maelezo yake hayajulikani kwa uhakika); Mwenyezi Mungu Mtukufu na Mtume wake ﷺ wanajua tafsiri yake, na sisi tunaziamini kuwa ndio ukweli.

^② Inatakiwa mtu asitumie katika njia ya Mwenyezi Mungu Mtukufu mali nyingi kiasi kwamba inampeleka kwenye majuto, na pia ajiepushe na ubakhili. Njia bora zaidi ni ya kati.

^③ (Tazama maelezo ya aya hii katika Tafsīr Shirāt al-Jinān kwa maelezo zaidi.)

2:6 Hakika wale ambao wameandikiwa kukufuru, ni sawa kwao ukiwaonya au usiwaonye; hawataamini.

إِنَّ الَّذِينَ كَفَرُوا سَوْاءٌ عَلَيْهِمْ أَنَّذَنَا تَهْمُمُ أُمُّ لَمْ يُنَزِّلْ رَهْمًا لَأُنْيُ مُنْوَنَ ﴿٧﴾

2:7 Mwenyezi Mungu amepiga muhuri juu ya nyoyo zao na masikio yao, na juu ya macho yao pana pazia,^① na watapata adhabu kali.

خَتَمَ اللَّهُ عَلَىٰ قُلُوبِهِمْ وَعَلَىٰ سَعْيِهِمْ وَعَلَىٰ أَبْصَارِهِمْ غَشَاؤَةٌ وَلَهُمْ عَذَابٌ عَظِيمٌ ﴿٨﴾

2:8 Mionganoni mwa watu wapo wanaosema: "Tumemuamini Mwenyezi Mungu na Siku ya Kiyama," na hali wao si wenye kuamini.

وَمِنَ النَّاسِ مَنْ يَقُولُ أَمَنَّا بِاللَّهِ وَبِالْيَوْمِ الْآخِرِ وَمَا هُمْ بِمُؤْمِنِينَ ﴿٩﴾

2:9 Watu hawa wanataka kumdanganya Mwenyezi Mungu na Waumini,^② ingawa wana-jidanganya wenyewe tu. Na wao hawatambui.

يُخْرُجُونَ اللَّهَ وَالَّذِينَ آمَنُوا حَمَّا يَخْدُعُونَ إِلَّا أَنْفُسُهُمْ وَمَا يَشْعُرُونَ ﴿١٠﴾

2:10 Kuna ugonjwa ndani ya miyo yao,^③ Basi Mwenyezi Mungu akawazidishia maradhi, na watapata adhabu chungu kwasababu ya kusema kwao uwongo.

فِي قُلُوبِهِمْ مَرَضٌ فَرَأَهُمُ اللَّهُ مَرَضًا وَلَهُمْ عَذَابٌ أَلِيمٌ بِمَا كَانُوا يَكْنِيُونَ ﴿١١﴾

2:11 Na wanapo ambiwa: "Msifanye uharibifu katika ardhi" husema: "Sisi ni watengenezaji tu."

وَإِذَا قِيلَ لَهُمْ لَا تُفْسِدُوا فِي الْأَرْضِ قَالُوا إِنَّا نَحْنُ مُصْلِحُونَ ﴿١٢﴾

Mada

- Hali ya makafiri maalum na matokeo yao.
- Hali ya wanafiki katika suala la kukumbatia imani na matokeo yao.
- Uharibifu wa wanafiki kwa jina la utengenezaji.

Maoni

^① Hali hii ya makafiri ilitokana na ukafiri wao, uadui, na chuki yao kwa Mtume Vinginevyo, njia za uwongofu hazikufungwa kamwe.

^② Mwenyezi Mungu hawezi kudanganyika. Kwa hiyo kinachomaanishwa na hili ni kujitahidi kwao kumdanganya Mtume wake Kipenzi . صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ

^③ Ugonjwa wa kiroho yaani unafiki wa wanafiki na chuki yao kwa Mtume . صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ Imani potofu huharibu hali ya kiroho, na mtu anayekereka na utukufu wa Mtume ana ugonjwa wa moyo.

2:12 Zingatia! Hakika, wao ndio wenye kueneza uharibifu,^① lakini hawautambui (ukweli huu).

2:13 Na wanapoambiwa: Aminini kama walivy-oamini watu,^② wanasema: Je, tuamini kama walivyoamini wapumbavu? Zingatia! Hakika wao ndio wapumbavu,^③ hata hivyo hawajui.

2:14 Na wanapokutana na walio amini husema: Tumesilimu, na wanapokuwa peke yao na mashetani wao husema: "Sisi tuko pamoja nanyi, tulikuwa tukiwakejeli tu.

2:15 Mwenyezi Mungu atawalipa malipo ya dhihaka zao,^④ lakini (kwa sasa) anawapa muhula ili wabaki wakitangatanga katika upotovu wao.

أَلَا إِنَّهُمْ هُمُ الْمُفْسِدُونَ وَلَكِنْ لَا يَشْعُرُونَ ⑩

وَإِذَا قِيلَ لَهُمْ أَمْنُوا كَمَا آمَنَ النَّاسُ قَالُوا أَنُؤْمِنُ
كَمَا آمَنَ السَّفَهَاءُ ۚ أَلَا إِنَّهُمْ هُمُ السَّفَهَاءُ وَلَكِنْ
لَا يَعْلَمُونَ ⑪

وَإِذَا لَقُوا الَّذِينَ آمَنُوا قَالُوا أَمَّا ۖ وَإِذَا أَخْلَوُا إِلَى
شَيْطَانٍ فَقَالُوا إِنَّا مَعَكُمْ لَا إِنَّمَا حُنُّ مُسْتَهْزِئُونَ ⑫

أَللّٰهُ يَسْتَهْزِئُ بِهِمْ وَيَبْدُّلُهُمْ فِي طُعْيَانِهِمْ يَعْمَلُونَ ⑬

Mada

- Kukanusha lawama dhidi ya Maswahaba.
- Udanganyifu wa wanaafiki na kuwakejeli kwao Waumini.
- Adhabu ya wanafiki.

Maoni

^① Tabia ya wanafiki inaangazia jinsi wale wanaoeneza ujisadi kwa jina la "marekebisho" (wema) walivyo wabaya zaidi kuliko wafisadi wa kawaida. Katika jamii yetu inaonekana hawakosekani watu wa aina hiyo wanaoeneza ujisadi kwa jina la uboreshaji na kuita matendo mabaya kwa majina mazuri.

^② Inafahamika kutokana na amri ya kuamini kama walivyoamini watu wema katika aya hii ya kwamba kuwafuata wao kunapelekea kwenye wokovu, na kukengeuka kutoka katika njia yao ni njia ya wanafiki. Pia tunajifunza kwamba watu wanaodhishaki na kuwasema vibaya watu hawa wacha Mungu walikuwepo hata karne nyingi zilizopita.

^③ Tumepata kujua kwamba Maswahaba wa mtume wana cheo kikubwa katika mahakama ya Mwenyezi Mungu Mtukufu kiasi kwamba Yeye Mwenyewe aliwajibu wale waliowadharau.

^④ Mwenyezi Mungu Mtukufu ametakasika na mzaha; kwa Kiarabu, matokeo ya kitendo yanaweza kuelezewa na neno la kitendo chenyewe (kama ilivyo hapa). Kwa hivyo hii ina maana kwamba Mwenyezi Mungu Mtukufu atawalipa malipo ya dhihaka zao (kwa kuwaadhibu) wanafiki.

2:16 Hawa ndio walio nunua upotofu kwa uwongofu; kwa hivyo biashara yao haikuleta faida yoyote — na watu hawa hawakujua hata njia.

أُولَئِكَ الَّذِينَ اشْتَرَوُ الْأَصْلَالَةَ بِأَهْدَىٰ فَمَا
رَأَبِحْتُ تِجَارَتَهُمْ وَمَا كَانُوا مُهْتَدِينَ ٦٣

2:17 **Mfano** wao ni kama yule aliywasha moto, kisha moto ulipomulika mazingira yake, Mwenyezi Mungu aliiondoa nuru yao na akawaacha gizani, hawaoni kitu.

مَثُلُهُمْ كَيْشَلُ الَّذِينَ اسْتَوْقَدُوا رَأْسًا قَلَّتِ آَضَاءُ ثُمَّ
حَوْلَهُ دَهَبَ اللَّهُ بِنُورِهِمْ وَتَرَكُهُمْ فِي ظُلْمَتِ
لَا يُبَصِّرُونَ ٦٤

2:18 Viziwi, mabubu, vipofu^① kwa hivyo hawatarudi.

صُمَدْ بِكُمْ عَنِ فَهْمِ لَا يَرْجِعُونَ ٦٥

2:19 **Au** (mfano wao ni) kama mvua inayonyeshya kutoka mbinguni ambayo ndani yake mngiza, ngurumo na umeme. Wanaweka vidole vya masikioni mwao kwa ngurumo ya radi, wakiogopa mauti, na Mwenyezi Mungu amewazunguka makafiri.

أَوْ كَصِيبٍ مِّنِ السَّبَابِ فِيهِ ظُلْمٌ وَرَعْدٌ وَبَرْقٌ
يَجْعَلُونَ أَصَابِعَهُمْ فِي أَذَانِهِمْ مِّنَ الصَّوَاعِقِ حَذَرَ
الْهُوتٍ طَ وَاللَّهُ مُحِيطٌ بِالْكُفَّارِينَ ٦٦

2:20 Inaonekana umeme utanyakua macho yao. Kila ulipowatolea mwangaza, walianza kutembea humo, na giza lilipowafunika, walibaki wamesimama. Na lau Mwenyezi Mungu angeli takaa angeyaondoa masikio yao na macho yao. Hakika Mwenyezi Mungu ni Muweza juu ya kila kitu^②.

يَجَادُ الْبَرْقُ يَحْطُفُ أَبْصَارَهُمْ طَ كُلَّمَا آَضَاءَ لَهُمْ مَشْوَافِيهِ
وَإِذَا أَظْلَمَ عَلَيْهِمْ قَامُوا طَ وَلَوْ شَاءَ اللَّهُ لَدَهَبَ إِسْمَاعِيلُ
وَأَبْصَارِهِمْ طَ إِنَّ اللَّهَ عَلَىٰ كُلِّ شَيْءٍ قَدِيرٌ ٦٧

Mada

- Mfano wa kwanza kati ya miwili inayowaeleza wanafiki.
- Mfano wa pili wa wanafiki.

Maoni

^① Wanafiki walipewa uwezo wa kupata uwongofu, lakini waliukadhibisha. Waliponyimwa kuona, kusikia, kusema, na kukubali ukweli, macho yao, masikio yao na ndimi zao hazikuwafaa kitu.

^② "Kila kitu" kinarejelea kila kitu kinachowezekana kiko chini ya Uwezo wa Mwenyezi Mungu Mtukufu na kinafaa Utukufu Wake. Mambo yasiyowezekana kamwe kimantiki hayafai kuwa chini ya Uwezo wa Mwenyezi Mungu Mtukufu.

يَا أَيُّهَا النَّاسُ اعْبُدُوا إِرَبِّكُمُ الَّذِي خَلَقَكُمْ وَالَّذِينَ مِنْ قَبْلِكُمْ عَلَّمُوكُمْ تَشَقُّونَ ﴿٢١﴾

2:21 Enyi Watu! Mwabuduni Mola wenu Mlezi,^① aliye kuumbeni nyinyi na walio kabla yenu, kwa matumaini hayo ili mpate uchamungu.

الَّذِي جَعَلَ لَكُمُ الْأَرْضَ فِرَاشًا وَالسَّمَاءَ عِنْدَكُمْ وَأَنْزَلَ مِنَ السَّمَاءِ مَاءً فَأَخْرَجَ بِهِ مِنَ الشَّرَابِتِ رِزْقًا لَّكُمْ فَلَا تَجْعَلُوا إِلَهَكُمْ أَنْدَادًا وَأَنْتُمْ تَعْلَمُونَ ﴿٢٢﴾

2:22 Ambaye amekufanyieni ardhi kama tandiko, na mbingu kama dari, na akateremsha maji kutoka mbinguni. Kisha akaumba katika maji hayo matunda mbalimbali kwa ajili ya matumizi yenu, basi msimfanyie Mwenyezi Mungu washirika na hali nyinyi munajua.

وَإِنْ كُنْتُمْ فِي رَيْبٍ مِّمَّا نَزَّلْنَا عَلَى عَبْدِنَا فَاقْتُلُوا إِسْوَارَةً مِّنْ مِّثْلِهِ وَادْعُوا شَهِيدًا كُمْ مِّنْ دُونِ اللَّهِ إِنْ كُنْتُمْ صَدِيقِينَ ﴿٢٣﴾

2:23 Na ikiwa mna shaka na Kitabu hiki tulicho kiteremsha juu ya mja wetu, basi leteni sura moja mfano wake, na muwaite wasaidizi wenu wasiokuwa Mwenyezi Mungu ikiwa nyinyi ni wakweli.^②

فَإِنْ لَمْ تَفْعَلُوا وَلَنْ تَفْعَلُوا فَاتَّقُوا اللَّهَ الرَّحِيمَ وَقُوْدَهَا إِنَّ النَّاسَ وَالْحَجَارَةَ أُعْدَتُ لِلْكُفَّارِينَ ﴿٢٤﴾

2:24 Basi ikiwa hamuwezi kufanya hivi - na hamtaweza kufanya hivyo - basi uogopeni Moto ambao kuni zake ni watu na mawe; umeandaliwa^③ kwa makafiri^④.

Mada

- Amri ya kumwabudu Mwenyezi Mungu Mtukufu na sababu kwa nini anastahiki kuabudiwa.
- Changamoto inayohusiana na ukweli wa Quran na tamko kwamba changamoto hii kamwe haitakibiliwa na makafiri.

Maoni

^① Ibada ni heshima ya hali ya juu ambayo mtu anaitekeleza kwa kukubali na kutakidi kuwa yeye ni mtumwa na anaemuabudu kuwa anastahiki kuabudiwa. Hapa, neno "ibada" linajumuisha kuamini upweke wa Mwenyezi Mungu (tawhid) na aina nyingine zote za ibada.

^② Changamoto hii ni kwa ajili ya wanadamu mpaka Siku ya Hukumu. Leo, kuna makafiri wengi wanaosema kuwa Quran ilitungwa na Mtume Muhammad ﷺ, lakini hakuna aliyeweza kujitokeza na aya moja kama hiyo, na yejote aliyedai kuwa amefanya hivyo alifichuliwa ndani ya siku chache.

^③ Hii inaonyesha kuwa moto wa Jahannam tayari umeshaumbwa kama wakati uliopita umetumika hapa.

^④ Msemo kwa makafiri unaonyesha kwamba waumini, kwa fadhila za Mwenyezi Mungu Mtukufu, watalindwa na kubaki Motoni milele, kwani Jahannamu imeumbwa makhsusi kwa ajili ya makafiri.

2:25 **Wape** habari njema kwa wale waliokubali imani na wakafanya matendo mema ambao kwa ajili yao zipo bustani zipitazo mito chini yake. Watakapo pewa matunda katika bustani hizo watasema, “Hii ndiyo riziki ile ile tuliyopewa hapo awali,” na wao walipewa tunda (kabla) ambalo lilifanana na (tunda hili), na wao katika bustani hizo watakuwa na wake walio safi, na watakaa humo milele.

وَبَشِّرُ الَّذِينَ آمَنُوا وَعَمِلُوا الصَّلِحَاتِ أَنَّ لَهُمْ جُنْتٌ
تَجْرِي مِنْ تَحْتِهَا الْأَنْهَرُ كُلَّمَا رِزْقُهُمْ هَامَنْ شَرَّةٌ
شَرَّةٌ قَالُوا هَذِهِ الَّذِي سُرِّزْ قَنَاتِهِمْ قَبْلُ وَأَنْوَابِهِ
مُتَشَابِهًاتٍ وَلَهُمْ فِيهَا آزْوَاجٌ مُّطَهَّرَةٌ وَهُمْ فِيهَا
خَلِدُونَ ﴿١٥﴾

2:26 **Mwenyezi** Mungu haoni aibu^① ya kueleza chochote kuhusiana na mfano, iwe hata mbu au zaidi ya hapo. Kwa vyovyote vile, Waumini wanajua kwamba hii ni haki itokayo kwa Mola wao Mlezi, na ama makafiri wanasema: “Amek-usudia nini Mwenyezi Mungu kwa mfano huu?” Mwenyezi Mungu anawapoteza wengi kupitia hayo,^② na anawaongoza wengi ndani yake; na kwa hayo anawapoteza wasiotii.

إِنَّ اللَّهَ لَا يَسْتَحِي أَنْ يَصْرِيبَ مَثَلًا مَّا بَعْوَضَةً فَمَا
فُوقَهَا طَفَلًا مَا الَّذِينَ آمَنُوا فَيَعْلَمُونَ أَنَّهُ الْحَقُّ مِنْ
هَمْبِّهِمْ وَأَمَّا الَّذِينَ كَفَرُوا فَيَقُولُونَ مَاذَا آَأَرَادَ اللَّهُ
بِهِنَّا مَثَلًا يُبَصِّلُ بِهِ كَثِيرًا وَيَهْدِي بِهِ كَثِيرًا وَمَا
يُبَصِّلُ بِهِ إِلَّا فُسِيقُّينَ ﴿١٦﴾

2:27 **Wale** wanao vunja ahadi kwa Mwenyezi Mungu baada ya kuithibitisha, na wanakata aliyo amrisha Mwenyezi Mungu kuungwa, na wanaeneza ufisadi katika ardhi. Watu hawa ndio wenye hasara.

الَّذِينَ يُنْقُضُونَ عَهْدَ اللَّهِ مِنْ بَعْدِ مِيثَاقِهِ وَيَقْطَعُونَ
مَا أَمْرَاهُمْ بِهِ أَنْ يُنْهِيَ صَلَوةَ وَيُفْسِدُونَ فِي الْأَرْضِ
أُولَئِكَ هُمُ الْخَسِرُونَ ﴿١٧﴾

Mada

- Habari njema ya Pepo na neema za mbinguni kwa Muumini mtiifu.
- Makusudio ya mifano ya Quran na tofauti baina ya waumini na makafiri katika kuiamini.
- Dalili tatu za muasi: kuvunja ahadi, kukata mahusiano, na kueneza ufisadi.

Maoni

^① Unyenyekevu (hayā') unaweza kufafanuliwa kuwa ni hisia inayomzuia mtu kufanya kitendo kwa sababu ya kuogopa kudhalilishwa—maana hii ni dhahiri haimhusu Mwenyezi Mungu Mtukufu, kwa hiyo msemo hapa unamaanisha “kutojiepusha na kutoa mifano.”

^② Madhumuni ya kimsingi ya Quran ni mwongozo. Hata hivyo, wengi wanakuwa wapotofu kwa sababu ya kukataa, kudhihaki, au kutafsiri kimakosa Quran; huu ndio ufahamu wa upotofu kupitia Quran.

2:28 **Vipi** mnamkufuru Mwenyezi Mungu? ingawa mulikuwa hamna uhai; kisha akaku-peni uhai;^① Kisha atakufisheni; kisha atakufu-fueni; na kisha mtarejeshwa kwake.

كَيْفَ تَكُفُّرُونَ بِاللَّهِ وَكُنْتُمْ أَمْوَاتًا فَأَحْيَاكُمْ حُتْمًا
بُيَدِينَكُمْ شَهْرٌ يُحِيطُكُمْ شَهْرٌ إِلَيْهِ تُرْجَعُونَ

2:29 Yeye ndiye aliye kuumbieni kila kilicho-mo katika ardhi,^② kisha akakusudia kuzumba mbingu, na akazumba mbingu saba, na Yeye ana ujuzi kamili wa kila kitu.

هُوَ الَّذِي خَلَقَ لَكُمْ مَا فِي الْأَرْضِ جَيِّنًا شَهْرًا
اسْتَوَى إِلَى السَّمَاوَاتِ فَسُوْرُهُنَّ سَبْعَ سَوْرٍ وَهُوَ يَكْلِلُ
شَهْرًا عَلَيْهِمْ

٢٩

2:30 **Na** kumbuka Mola wako Mlezi alipo waambia Malaika,^③ “Mimi nitamweka katika ardhi Khalifa (naibu).” Wakasema: “Je! Utaweka juu yake atakayeleta fitna ndani yake na kumwaga damu, huku sisi tunakutukuzwa kwa sifa zako na tunataja utakatifu wako?” Akasema: Nayajua msiyo yajua.

وَإِذْ قَالَ رَبُّكَ لِلْمَلَائِكَةِ إِنِّي جَاعِلٌ فِي الْأَرْضِ
خَلِيفَةً قَالُوا أَتَجْعَلُ فِيهَا مَنْ يُغَيِّرُ فِيهَا وَيَسْفِكُ
الرِّمَاءَ وَنَحْنُ نُسَبِّحُ بِحَمْدِكَ وَنُقَدِّسُ لَكَ طَ
قَالَ إِنِّي أَعْلَمُ مَا لَا تَعْلَمُونَ

2:31 **Na** akamfundisha Adam majina ya kila kitu. Kisha baada ya kuwaonyesha Malaika, akawaambia: “Niambieni majina ya vitu hivi ikiwa nyinyi mnasema kweli.”^④

وَعَلِمَ آدَمَ إِلَّا سَيَّأَةً كُلَّهَا شَهْرٌ عَرَضَهُمْ عَلَى الْمَلَائِكَةِ
فَقَالَ آنِئُونِي بِإِسْمَاهُ لَآءُونَ كُنْتُمْ صَدِيقِيَنَ

Mada

- Ishara za Uweza wa Mwenyezi Mungu: kuumba watu na kuwafanya wafe na kuumbwa mbingu na ardhi.
- Kuumbwa kwa Mtume Ādam ﷺ, kumfanya Khalifa (makamu), na kumjaalia elimu.
- Mtume Ādam ﷺ kufundishwa elimu ya majina ('ilm al-asmā') na ubora wake juu ya malaika.

Maoni

^① Aya hii ina ushauri kwa Waislamu pia; hatukuwa chochote na bado Mwenyezi Mungu Mtukufu alitupa uhai, akatupa mahitaji ya maisha, na akatupa neema zake. Kwa hiyo kughairi na kukosa shukrani baada ya kunufaika na neema haitufai sisi.

^② Kutokana na hili ni wazi kwamba chochote ambacho Mwenyezi Mungu hakuhamisha kinajuzu (mubāh) na ni halali.

^③ Habari kwamba khalifa (makamu) atafanya ilitolewa kwa Malaika kwa njia ambayo inaonekana kama mashauriano. Ingawa kwa hakika, Mwenyezi Mungu Mtukufu hana haja yoyote ya kushauriana.

^④ Katika aya hii, Mwenyezi Mungu Mtukufu anadhihirisha kwamba elimu ndiyo sababu ya Mtume Ādam ﷺ kupewa ukuu juu ya Malaika; elimu ni kubwa zaidi kuliko ibada inayofanywa katika upweke.

2:32 Walisema “(Ewe Mwenyezi Mungu) umetakasika!! Sisi tunajua uliyo tufundisha.^① Hakika wewe ndiye Mjuzi, Mwenye hekima.”

الْعَلِيمُ الْحَكِيمُ^③

2:33 Akasema: “Ewe Adam! Waambie majina ya vitu hivi.” Basi (Adam) alipowaambia majina yake, (Mwenyezi Mungu) akasema: “(Enyi Malaika!) Je, sikukwambieni kwamba ninajua siri zote za mbingu na ardhi, na ninajua mnayo yatangaza na mliyo kuwa mkiyaficha?”

قَالَ يَا آدُمَ أَنْبِئْهُمْ بِأُسْمَائِهِمْ فَلَمَّا آتَيْنَاهُمْ بِأُسْمَائِهِمْ قَالَ أَلَمْ أَقُلْ لَكُمْ إِنِّي أَعْلَمُ مِغَيْبَ السَّمَاوَاتِ وَالْأَرْضِ
وَأَعْلَمُ مَا تَبْدُونَ وَمَا كُنْتُمْ تَكْسِبُونَ^④

2:34 Na kumbuka tulipowaamrisha Malaika: Msujudieni Adam, wakasujudu isipokuwa Iblīs.^② Alikataa na akaonyesha kiburi na akawa kafiri.

وَإِذْ قُلْنَا لِلْيَلِيلَكَةَ اسْجُدْ وَالْأَدَمَ فَسَجَدْ وَالْأَدَمَ
إِبْلِيسُ طَآبِي وَاسْتَكْبَرَ^٥ وَكَانَ مِنَ الْكُفَّارِ^٦

2:35 Na tukasema: Ewe Adam! Wewe na mkeo kaeni Peponi, na kuleni humo maridhawa popote mpendapo, lakini msiukaribie mti huu, la sivyo mtakuwa mionganoni mwa wanaoruka mipaka.”^③

وَقُلْنَا يَا آدُمَ اسْكُنْ أَنْتَ وَزَوْجُكَ الْجَنَّةَ وَكُلُّ مِنْهَا رَاغِدًا
حَيْثُ شِئْتُمَا وَلَا تَقْرَبَا هَذِهِ الشَّجَرَةِ فَتَكُونُوا مِنَ
الظَّالِمِينَ^٧

Mada

- Malaika wakisujudu mbele ya Mtume Ādam عليه السلام kwa mujibu wa Amri ya Mwenyezi Mungu, na kukataa na kiburi cha Shetani (*Iblīs*).
- Kuwasili kwa Mtume Adam Peponi na maelezo ya Shetani.

Maoni

^① Aya hii inaangazia heshima ya mwanadamu na ubora wa elimu. Zaidi ya hayo, kumnasibisha Mwenyezi Mungu na kufunza wengine elimu ni sahihi, lakini hatakiwi kuitwa mwalimu (mu'allim) kwa sababu neno hili linamuhusu mtu ambaye hutoa maarifa kwa wengine kama taaluma.

^② Malaika walisujudu sijida ya heshima mbele ya Mtume Ādam عليه السلام na hii ilifanyika kwa kuweka paji la uso juu ya ardhi, si kwa kuinamisha tu kichwa kidogo.

^③ Mwenyezi Mungu ndiye Mola Mlezi, na anaweza kuwashutubia wateule wake apendavyo; hakuna mwingine ana haki ya kufanya hili kuwa msingi wa kutumia kwa manabii maneno ambayo ni kinyume na heshima inayostahili na inayopaswa kuonyeshwa kwao.

2:36 Kwa hiyo Shetani aliwatelezesa hao wawili,^① na akawatoa katika waliokuwamo, na tukasema: "Shukeni! Mtakuwa maadui wenyewe kwa wenyewe, na mna makazi na riziki katika ardhi mpaka muda maalumu."

فَأَزَّهُمَا الشَّيْطَنُ عَنْهَا فَأَخْرَجَهُمَا كَانَا فِيهِ وَقُلْنَا
اَهِبُّطُوا بَعْضُكُمْ لِبَعْضٍ عَدُوٌّ وَلَكُمْ فِي الْأَرْضِ مُسْتَقْرَرٌ

مَتَاعٌ إِلَى حِينٍ^②

2:37 Kisha Adam akajifunza maneno kutoka kwa Mola wake Mlezi, basi Mwenyezi Mungu akamkulalia toba yake.^③ Hakika Yeye tu ndiye Mwingi wa kupokea toba na Mwingi wa kuhurumia.

فَتَلَقَّ أَدْمُرٌ مِّنْ سَرِّهِ گَلِيْتَ فَتَابَ عَلَيْهِ إِنَّهُ هُوَ التَّوَابُ
الرَّحِيمُ^④

2:38 Tukasema: "Shukeni kutoka Peponi, nyote,^⑤ Basi ukikujieni uwongofu kutoka Kwangu, basi wale watakaofuata uwongofu wangu hawataogopa wala hawatahuzuniha.

قُلْنَا اَهِبُّوا مِنْهَا جَحِيْمًا فَإِمَّا يَتَبَيَّنُكُمْ مِّنْهُمْ هُدًى فَمَنْ
تَبَعَ هُدًى اَفَلَا خُوفٌ عَلَيْهِمْ وَلَا هُمْ يَحْرَنُونَ^⑥

2:39 Na watakao kufuru na kuzikataa Aya zangu hao ndio watu wa Motoni, watakaa humo milele."

وَالَّذِينَ كَفَرُوا وَكَذَّبُوا بِآيَاتِنَا اُولَئِكَ اَصْحَبُ النَّارِ
هُمْ فِيهَا خَلِدُونَ^⑦

2:40 Enyi Watoto wa Ya'qub!^⑧ Kumbukeni^⑨ Neema yangu niliyo kupeni, na timizeni ahadi

لِيَبَيِّنَ اُسْرَاءَعِيلَ اذْ كُرُوفَانِعَتِيَ الَّتِي اَنْعَمْتُ عَلَيْكُمْ

بع

Mada

- Kushuka kwa Nabii Adam kwenye ardhi na Amri za Mwenyezi Mungu.
- Wana wa Israeli wakikumbushwa neema walizopewa, na kutajwa baadhi ya hukumu zilizowekwa kwao; yaani kutimiza viapo, kutofunika ukweli kwa uwongo, kutekeleza sala na zaka kwa wakati, n.k.

Maoni

^① Mbali na kisomo, kuhusisha dhambi kwa Mtume Adam عليه السلام kutoka kwa mtu mwenyewe ni marufuku; kwa kweli, kundi la wanazuoni wametangaza kufanya hivyo kuwa ni Kufr (ukafiri).

^② Wakati toba (tawba) inapohushishwa na Mwenyezi Mungu Mtukufu, ina maana ya "kukubali toba au Mwenyezi Mungu kurejea kwa mja Wake kwa Rehema Zake."

^③ Umbo la wingi ("Shukeni") lilitumika kuamrisha kushuka duniani, neno hili lilijumuisha Mtume Adam. عليه السلام Sayyida Hawwa na kizazi chao (katika mgongo wa Adam).

^④ Aya hii inawazungumzia Mayahudi kuanzia zama za kipenzi chetu Mtume Muhammad صلى الله عليه وسلم.

^⑤ Hapa "kumbukeni" haimaanishi kuzikumbuka na kuzitaja neema kwa maneno tu, bali ina maana kwamba shukrani ya neema inapaswa kuonyeshwa kuititia matendo pia kwa kumtii Mwenyezi Mungu, kwasababu kuacha shukrani ya neema ni kama kuisahau.

yangu; Nitatimiza ahadi yenu, na niogopeni mimi tu.

وَأَوْفُوا بِعَهْدِكُمْ وَإِيَّاهُ فَارْهُونَ ①

2:41 Na aminini Kitabu nilicho kiteremsha, kinachosadikisha mliyo nayo. Wala msiwe wa kwanza wa kuikataa, wala msiziuze Aya zangu kwa thamani ndogo, na niogopeni Mimi peke yangu.

وَأَمْنُوا بِهَا أَنْزَلْتُ مُصَدِّقًا لِمَا مَعَكُمْ وَلَا تُكُونُوا أَوَّلَ كَافِرِينَ وَلَا تَشْتَرُوا إِيمَانَكُمْ بِمَقْلِيلٍ وَإِيَّاهُ فَاتَّقُونَ ②

2:42 Na wala musichanganye kweli na uwongo, na wala msiifiche haki hali mnajua. ①

وَلَا تُنْسِو الْحَقَّ بِالْبَاطِلِ وَلَا تُنْسِو الْحَقَّ وَأَنْتُمْ تَعْلَمُونَ ③

2:43 Na simamisheni Sala, na toeni zaka, na inameni pamoja na wanao inama.

وَأَقِيمُوا الصَّلَاةَ وَأَتُوا الرَّزْكَ وَأُنْهِيَ عُوَامَّةُ الرُّكَعِينَ ④

2:44 Je! mnawaamrisha watu kwenye wema na mnajisahau hata nyinyi mnasoma Kitabu? Je hamna akili? ⑤

أَتَأُمْرُونَ النَّاسَ بِالْبِرِّ وَتَنْسُونَ أَنْفُسَكُمْ وَأَنْتُمْ تَتَلَوَّنَ الْكِتَابَ طَأْفَلًا تَعْقِلُونَ ⑥

2:45 Na tafuteni msaada kwa kusubiri na kwa Sala, ⑦ na hakika Swalah ni nzito isipokuwa kwa wanao nyenyekeea kwangu kutoka moyoni.

وَاسْتَعِينُوا بِالصَّبْرِ وَالصَّلَاةِ وَإِنَّهَا لَكَبِيرَةٌ إِلَّا عَلَى الْخَشِعِينَ ⑧

2:46 Ambao wana yakini kuwa watakutana na Mola wao Mlezi na kwamba watarejea kwake.

الَّذِينَ يَظْنُنُونَ أَنَّهُمْ مُلْقُوا أَرَبِّهِمْ وَأَنَّهُمْ إِلَيْهِ لَرَجُونَ ⑨

Mada

- Waisraeli wakiwaamuru wengine kutenda mema lakini wakijisahau wenyewe.
- Amri ya kutafuta msaada kutokana na subira na sala.

Maoni

① Aya hii inaeleza kwamba mtu yejote asichanganye uwongo katika ukweli, au kuficha ukweli, kwani hii inaleta uharibifu na kunyimwa. Ni lazima kwa mwenye kuijua haki kuifichua, na ni haramu kwake kuificha.

② Ingawa Aya hii iliteremshwa katika mazingira maalum, hukumu inayotokana nayo ni ya jumla, na ina funzo kwa kila mhubiri.

③ Uvumilivu huongeza nguvu za kiroho na kupitia sala, uhusiano wa mtu na Mwenyezi Mungu Mtukufu huimarika; vipengele vyote viwili huwezesha mtu kukabili na kukabiliana na shida.

2:47 Enyi Wana wa Ya'quub! Kumbukeni neema yangu niliyo kupeni na kwamba nime-wapa ubora juu ya ulimwengu wote katika zama hizo^①.

يَبْنِي إِسْرَائِيلَ أَذْكُرُوا نِعْمَتِي الَّتِي أَنْعَمْتُ عَلَيْكُمْ وَأَنِّي فَضَّلْتُكُمْ عَلَى الْعَالَمِينَ^②

2:48 Na iogopeni siku ambayo nafsi yoyote haitatosheleza nafsi nyingine kwa lolote, wala haitakubaliwa kwake maombezi, wala haitachukuliwa kwake fidia, wala hawatanusuri-wa.^③

وَاتَّقُوا يَوْمًا لَا تَجِدُنَّ فِي نَفْسٍ شَيْئًا وَلَا يُقْبَلُ مِنْهَا شَفَاعَةٌ وَلَا يُؤْمِنُ خَدْمُنَّهَا عَدْلٌ وَلَا هُمْ يُصْرُونَ^④

2:49 Na kumbukeni tulipo kupeni uwokozi kwa kaamu ya Firauni ambao walikuwa wakikupeni adhabu kali, wakiwachinja watoto wenu wa kiume na wakiwaacha hai mabinti zenu; na katika hayo ulikuwa mtihani mkubwa kutoka kwa Mola wenu Mlezi.

وَإِذْ جَاءَنَا يَعْنَانُكُمْ مِنْ أَلْفِ فِرْعَوْنَ يَسُومُونَكُمْ سُوءَ الْعَزَابِ يُذْهِبُونَ أَبْنَاءَكُمْ وَيَسْتَحْيِيُونَ نِسَاءَكُمْ وَفِي ذَلِكُمْ بَلَاءٌ عَظِيمٌ^⑤

2:50 Na (kumbukeni) tulipoipasua bahari kwa ajili yenu, tukakuokoeni na tukawazamisha watu wa Firauni huku mkitazama.

وَإِذْ قَرَّنَا بِكُمُ الْبَحْرَ فَأَنْجَبْنَاكُمْ وَأَغْرَقْنَا أَلْفَرْعَوْنَ وَأَنْثَمْتَنَا نَظَرُونَ^⑥

2:51 Na kumbuka tulipo muahidi Musa masiku arobaini,^⑦ kisha mkamuabudu ndama baada yake, na hakika mlikuwa madhalimu.

وَإِذْ دَعَنَا مُوسَى أَسْرَيْعَيْنَ لَيْلَةً ثُمَّ أَنْجَلْنَاكُمُ الْعِجْلَ مِنْ بَعْدِهِ وَأَنْتُمْ ظَلِيمُونَ^⑧

Mada

- Ukumbusho wa kina wa neema kwa Wayahudi.
- Amri kwa Mayahudi kutafakari juu ya Akhera.
- Udhalimu wa Firauni dhidi ya Waisraeli na wokovu wa Mwenyezi Mungu kwa unaokuja kupidia kwa Nabii Musa عَلَيْهِ السَّلَامُ.
- Kugawanyika kwa bahari kwa Waisraeli na kuzamishwa kwa jeshi la Firauni.
- Ahadi ya kupewa Taurati, Waisraeli wakiabudu ndama na toba yao.

Maoni

^① Waisraeli walipewa heshima hii katika zama hizo, baada ya hapo, kwa kuwasili kwa Mtume wa Mwisko هَلَّ اللَّهُ عَلَيْهِ وَاللَّهُ أَكْبَرُ ubora huu ulihamishiwa kwa taifa lake lililobarikiwa.

^② Siku ya Kiyama, kafiri hatapata faida yoyote kutoka kwa kafiri mwengine au hata kwa Muumini; uombezi siku hiyo utakuwa kwa Waumini tu.

^③ Baada ya kuangamizwa kwa Firauni na wafuasi wake, Mtume Mūsā عَلَيْهِ السَّلَامُ aliporudi Misri pamoja na taifa lake Mwenyezi Mungu aliahidi kumpa Taurati; na kwa ajili ya hili alimteulia mwanzoni muda wa siku thelathini, kisha zikaongezwa siku kumi zaidi.

2:52 Kisha tukakusameheni baada ya hayo ili mpate kushukuru.

شَمَّ عَفْوَنَا عَنْكُمْ مِّنْ بَعْدِ ذَلِكَ لَعَلَّكُمْ تَشْكُرُونَ ⑤٣

2:53 Na kumbukeni tulipo mpa Musa Kitabu na Upambanuo ili mpate uwongofu.

وَإِذَا تَيَّأْمَوْسَى الْكِتَابَ وَالْقُرْآنَ لَعَلَّكُمْ تَهْتَدُونَ ⑤٤

2:54 Na kumbuka Musa alipo waambia watu wake: “Enyi kaumu yangu! Hakika mmezid-hulumu nafsi zenu kwa kumuabudu ndama, basi (sasa) tubuni kwa Muumba wenu; basi waueni watu wenu.^① Haya ni bora kwenu kwa Muumba wenu.” Basi akakukubalieni toba yenu, hakika Yeye ni Mwingi wa kupokea toba, Mwingi wa kuhurumia.

وَإِذْ قَالَ مُوسَى لِقَوْمِهِ يَقُولُ مَا لَكُمْ ظَلَمْنَا إِنَّكُمْ أَنْفَسْكُمْ
بِإِتْخَادِكُمُ الْعِجْلَ فَتُوَبُوا إِلَىٰ بَارِئِكُمْ فَاقْتُلُوا
أَنْفَسْكُمْ ذَلِكُمْ خَيْرٌ لَّكُمْ إِنَّهَا بَارِئِكُمْ طَفَّاتٌ عَلَيْكُمْ
إِنَّهُ هُوَ التَّوَابُ الرَّحِيمُ ⑤٥

2:55 Na kumbukeni mliposema: “Ewe Musa! Hatutakuamini mpaka tumwone Mwenyezi Mungu waziwazi.” Kisha mukapigwa na radi mukiwa mnatazama.^②

وَإِذْ قَلَّتِمْ يَوْمُكُمْ لَنْ تُؤْمِنَ لَكَ حَتَّىٰ نَرَى اللَّهَ جَهَنَّمَ
فَاخْزَنَتُمُ الصُّعْقَةَ وَأَنْتُمْ تَنْظُرُونَ ⑤٦

2:56 Kisha tukakufufueni baada ya kufa kwenu ili mpate kushukuru.

شَمَّ بَعْثَنَتُكُمْ مِّنْ بَعْدِ مَوْتِكُمْ لَعَلَّكُمْ تَشْكُرُونَ ⑤٧

2:57 Na tukakutieni kivuli kwa wingu na tukakuteremshieni Mann na Salwa.^③ “Kulenii

وَظَلَّنَا عَلَيْكُمُ الْغَيَّامَ وَأَنْزَلْنَا عَلَيْكُمُ الْمَنَّ وَالسَّلَوَىٰ

Mada

- Torati ikitolewa kuwaongoza Waisraeli.
- Toba ya Waisraeli baada ya kumwabudu ndama.
- Mahitaji ya Waisraeli kumuona Mwenyezi Mungu Mtukufu kwa uwazi na matokeo yake.
- Kivuli cha wingu juu ya Waisraeli na kushuka kwa *Mann* na *Salwā*.

Maoni

^① Aya hii inadhihirisha jinsi ushirikina unavyomfanya muumini kuwa murtadi na hivyo adhabu yake ni kuuwawa, kwani amefanya uadui na Mwenyezi Mungu Mtukufu. Na ambaye amefanya uadui dhidi ya Mwenyezi Mungu basi kumuadhibu kwa mauti ndio jambo lenye hekima na manufaa ya wote.

^② Maelezo haya yanadhihirisha ukuu wa Mitume; Wana wa Israili waliposema: “Ewe Musa! Hakika sisi hatutakuamini ...” waliangamizwa kutokana na kutokumuheshimu kwao.

^③ *Mann* kilikuwa ni aina ya chakula kitamu (chepesi kama umande na ladha ya asali) na *Salwā* alikuwa ndege mdogo.

كُلُّوْا مِنْ طَيْبَاتِ مَا رَأَيْتُمْ وَمَا أَظْلَمُونَا وَلِكُنْ كَافِرُوا
Wala hawakutudhuru, bali walikuwa wanajidhulumu nafsi zao tu.

أَنْفُسَهُمْ يَظْلِمُونَ ﴿٥٦﴾

2:58 Na tulipo waambia: Ingieni katika mji huu, na kuleni popote mpendapo maridhawa, na ingieni kwa kusujudu mlangoni mkisema: ‘Tusamehewe dhambi zetu’; Tutakusameheni madhambi yenu, na hivi karibuni tutawazidhia wafanyao wema.

وَإِذْ قَنَّا دُخْلُوا هَذِهِ الْقَرَيْةَ فَكُلُّوْا مِنْهَا حِلْيَشْ شَعْشُمْ

رَغْدًا وَأَدْخُلُوا الْبَابَ سُجَّادًا وَقُلُّوا حَمَّةً تَغْفِرُ لَكُمْ

خَطِيمْ وَسَنَرِيْدُ الْمُحْسِنِينَ ﴿٥٧﴾

2:59 Kisha wale waliodhulumu wakabadilisha kauli isiyo kuwa walioambiwa,^① Basi tukawateremshia adhabu kutoka mbinguni kwasababu ya walivyokuwa wakiasi.

فَبَدَّلَ اللَّنِيْنَ ظَلَمُوا أَقْوَالَ غَيْرِ الَّذِيْنِ قَيْلَ لَهُمْ فَأَنْزَلْنَا

عَلَى الَّذِيْنَ ظَلَمُوا إِرْجَزًا مِنَ السَّمَاءِ بِمَا كَانُوا يَفْسُدُونَ ﴿٥٨﴾

2:60 Kumbuka wakati Musa alipoomba maji kwa ajili ya watu wake,^② Tukasema: Lipige jiwe kwa fimbo yako, mara chemchem kumi na mbili zikabubujika humo;^③ Kila kabile likajua mahali pao pa kunywea, na tukasema: Kuleni na kunywensi katika riziki za Mwenyezi Mungu, wala msitembee katika ardhi mkieneza ufsadi.”

وَإِذَا سَتَّقَ مُوسَى لِقَوْمِهِ فَقُلْنَا أَصْرِبْ بِعَصَالَ الْحَجَرِ

فَانْفَجَرَتِ مِنْهُ اثْنَتَيْ عَشْرَةَ عَيْنًا قَدْ عَلِمَ كُلُّ

أَنَّا إِنْ مَشَرَّبُهُمْ كُلُّوْا أَشْرَبُوا مِنْ رِزْقِ اللَّهِ وَلَا تَعْشُوا

فِي الْأَرْضِ مُفْسِدِيْنَ ﴿٥٩﴾

Mada

- Kuwaamuru Waisraeli waingie Misri au mji maalum, uasi wao na adhabu iliyofuata.
- Waisraeli wakitafuta maji jangwani na kupewa maji kwa muujiza wa Mtume Mūsa. عَلَيْهِ السَّلَامُ

Maoni

^① Wana wa Israeli waliamrisha kuingia huku wakisujudu na kusema: “ḥittah!” (tusamehewe dhambi zetu) lakini wakaasi amri zote mbili, wakijiburuta mlangoni kwa nyuma yao (wala hawakusujudu) na wakasema kwa dhihaka, “ḥabbatun fi sha‘ratin!” (tembe kwenye unywele), badala ya kuleta istighfar.

^② Aya hii inabitisha kwamba Mitume watukufu hutimiza mahitaji ya watu na hivyo basi msaada unaweza kutafutwa kutoka kwao.

^③ Kutoa maji kutoka kwenye jiwe ilikuwa ni muujiza mkubwa wa Mtume Mūsā, na Mtume wetu kipenzi صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ kufanya maji kububujika kutoka kwa vidole vyake vilivyobarikiwa ilikuwa muujiza mkubwa zaidi.

2:61 Na uliposema: Ewe Musa! Hatuwezi kamwe kuridhika na aina moja ya chakula,^① basi tuombee kwa Mola wako Mlezi ili tutoe mimea inayoota katika ardhi kama mchicha, tango, ngano, dengu na vitunguu. Akasema, “Je, mnatafuta kitu duni badala ya kilicho bora zaidi? Upendavyo Kaa katika eneo la Misri au katika mji; huko utapata kila ulichoomba.” Na kisha wakafanyiwa unyonge na umasikini,^② na wakawa wanastahiki ghadhabu ya Mwenyezi Mungu; Hayo ni kwa sababu walikuwa wakizikataa Aya za Mwenyezi Mungu, na walikuwa ni Manabii bila ya haki. Hayo ni kwa sababu waliasi na walikuwa wakiruka mipaka.

وَإِذْ قُلْنَا لِيُوسُى لَنْ نَصِيرَ عَلَى طَعَامِنَا وَاحِدٌ فَادْعُنَا
رَبَّكَ يُخْرِجُ لَنَا مِمَّا تَنْتَهِي إِلَيْهِ رُسُولُنَا مِنْ بَقِيلَهَا وَقَشَابِهَا
وَفُؤُمَهَا وَعَدَسَهَا وَبَصَلَهَا قَالَ أَتَسْتَبِيلُونَ الَّذِي هُوَ
أَدْنَى بِالَّذِي هُوَ خَيْرٌ طِهِطِوًا مُصْرًّا فَإِنَّكُمْ مَا
سَأَلْتُمْ طِهِطِوًا ضَرِبَتْ عَلَيْهِمُ الظِّلَّةُ وَالْمَسْكَنَةُ وَبَاعِرُو
بَعْضٌ مِنْ أَنْهَى طِهِطِوًا ذَلِكَ بِأَنَّهُمْ كَانُوا يَكْفُرُونَ بِأَيْتَ اللَّهِ وَ
يَقْتُلُونَ النَّبِيِّنَ بِغَيْرِ الْحَقِّ طِهِطِوًا بِمَا عَصَوْا وَكَانُوا

يَعْتَدُونَ ﴿٦﴾

2:62 Hakika walio amini na Mayahudi na Wakristo na Masabii (waabudu nyota) yejote atakaemuamini Mwenyezi Mungu na Siku ya Mwisho na akatenda mema, basi malipo yao yako kwa Mola wao Mlezi, wala hawatakua na hofu wala hawatahuzunika.

إِنَّ الَّذِينَ آمَنُوا وَالَّذِينَ هَادُوا وَالَّذِينَ رَأَوْا الصِّيَّنَ
مَنْ أَمْنَ بِاللَّهِ وَالْيَوْمِ الْآخِرِ وَعَمِلَ صَالِحَاتِهِمْ أَجْزَهُمْ
عِنْدَ رَبِّهِمْ وَلَا خَوْفٌ عَلَيْهِمْ وَلَا هُمْ يَحْزَنُونَ ﴿٦﴾

Mada

- Waisraeli wakitafuta vyakula vya ardhini badala ya Mann na Salwa ya mbinguni.
- Kufedheheshwa kwa Waisraeli na sababu zake.
- Nani anastahili thawabu kutoka kwa Mwenyezi Mungu?

Maoni

^① Haikuwa dhambi kwa Waisraeli kudai mboga, tango, au vyakula hivi vingine; lakini, kugeuka kutoka kwa neema za Mann na Salwa, ambazo hazihitaji jitihada yoyote na kuomba mazao ya dunia ilikuwa ni fikra ya hali ya chini. Mwenye uhusiano na wakuba, moyo wake, akili na fikra zake zinapaswa kuwa kubwa vile vile.

^② Waislamu wanapaswa kutafakari juu ya sababu za kuanguka kwa Waisraeli ambao wakati fulani walifikia kilele kikubwa, kwa kuchambua matendo yao wenyewe; na wanapaswa pia kutafakari kwa makini juu ya maisha yao ya zamani na ya sasa.

2:63 Na kumbukeni tulipochukua ahadi yenu, na tukauinua mlima Sinai juu ya vichwa vyenu, (na tukasema): Shikamaneni na Kitabu hiki tulicho kupeni,^① na kumbukeni yaliyoelezwa humo ili mpate kuwa wachamungu.

وَإِذَا أَخْرَجْنَا مِنَّا مُشَاجِلْمُ وَرَفَعْنَاهُ قُلْمُ الظُّورَ طَحْنُوا مَا
أَتَيْنَكُمْ بِقُوَّةٍ وَإِذْ كُرُوا مَا فِيهِ لَعَلَّكُمْ تَشَفَّعُونَ^②

2:64 Kisha mkageuka baada ya hayo, basi lau kuwa si fadhila ya Mwenyezi Mungu juu yenu na rehema yake, mngelei kuwa mionganini mwa walio khasirika.

ثُمَّ تَوَلَّ يُمْنُعُ مِنْ بَعْدِ ذَلِكَ فَلَوْلَا فَضْلُ اللَّهِ عَلَيْكُمْ وَ
سَرَاحَتْتُكُمْ لَكُنْتُمْ مِنَ الْخَسِيرِينَ^③

2:65 Na hakika nyinyi mnawajua walio dhulumu mionganini mwenu siku ya Sabato (Jumamosi). Basi tukawaambia: Kuweni manyani wadhalilifu.”

وَلَقَدْ عَلِمْتُمُ الَّذِينَ اعْتَدْ وَأَمْنَكْمُ فِي السَّبْتِ فَقُلْنَا لَهُمْ
كُوْنُوا قَرَدَةٌ خَسِيرُينَ^④

2:66 Basi tukayafanya hayo kuwa ni mazingatio kwa watu wa zama hizo na waliokuja baada yao, na nasaha kwa wachamungu.^⑤

فَجَعَلْنَاهُنَّا لَلْبَابِينَ يَدِيهَا وَمَا حَلْفَهَا وَمَوْعِظَةً
لِلْمُسْتَقِيْنَ^⑥

2:67 Na kumbuka Musa alipo waambia watu wake: Hakika Mwenyezi Mungu anakuamrisheni kuchinja ng'ombe; wakasema: Unatufanyia mzaha? Musa akasema, “Naomba

وَإِذْ قَالَ مُوسَى لِقَوْمَهِ إِنَّ اللَّهَ يَأْمُرُكُمْ أَنْ تَذْبَحُوا
بَقَرَةً قَالُوا أَتَتَخْذِنَاهُ زُواً طَقَالَ أَعُوذُ بِاللَّهِ أَنْ

Mada

- Shida zinazowapata Waisraeli kutoekana na kutozikubali Sheria za Taurati na mwenendo wao.
- Waisraeli wakivua samaki siku ya Sabato (Jumamosi), licha ya kukatazwa kufanya hivyo na hivyo hufanywa mfano wa.
- Amri ya Waisraeli kuchinja ng'ombe kuhusiana na mtu aliyeuawa na maswali yao yasiyo na maana.

Maoni

^① Hapa inaonekana kulazimishwa kutimiza ahadi; kumbuka, hakuna kulazimishwa katika kukubali Dini ya Uislamu; hata hivyo, baada ya kuikubali dini hiyo, mtu analazimika kushikamana na sheria zake. Hili lieleweke kwa mfano wa jinsi serikali haimlazimishi mtu kuingia katika nchi yake, lakini mtu anapoingia, serikali inamlazimisha kufuata sheria zake.

^② Visa vya Qurani vya adhabu vimetajwa ili tupate kuvizingatia; na mionganini mwa haki za Quran ni kwamba mtu aelekee katika kujirekebisha baada ya kusoma aya na visa hivi.

ulinzi kwa Mwenyezi Mungu kutokana na haya kuwa mimi niwe mionganoni mwa wajinga.”^①

أَكُونَ مِنَ الْجَهِلِينَ ﴿٤﴾

2:68 Wakasema: Tuombee kwa Mola wako Mlezi atueleze waziwazi ni ng’ombe wa namna gani. Akasema, “Mwenyezi Mungu anasema kuwa ni ng’ombe ambaye si mzee wala si mchanga sana, bali ni wa katikati baina ya hao. Basi fanyeni munavyoamrishwa.”^②

قَالُوا دُعْلَنَّا رَبَّكَ يُبَيِّنُ لَنَا مَا هَيَّ طَقَالِ إِنَّهُ يَقُولُ إِنَّهَا
بَقَرَةٌ لَّا فَارِضٌ وَلَا بَكَرٌ طَعَانٌ بَيْنَ ذَلِكَ طَقَافُلُوا
مَاتُؤْمِرُونَ ﴿٤٨﴾

2:69 Wakasema: Tuombee kwa Mola wako Mlezi atupambanulie rangi yake. Akasema: “Mwenyezi Mungu anasema ni ng’ombe wa manjano, rangi yake imekoza, anayewapendeza watazamaji.”

قَالُوا دُعْلَنَّا رَبَّكَ يُبَيِّنُ لَنَا مَا لَوْلَهَا طَقَالِ إِنَّهُ يَقُولُ
إِنَّهَا بَقَرَةٌ صَفْرَاءُ لَاقِعٌ لَوْلَهَا سُرُّ الظِّرِيرِينَ ﴿٤٩﴾

2:70 Wakasema: “Tuombee kwa Mola wako Mlezi atuelekeze waziwazi jinsi alivyo, bila shaka ng’ombe wamefanana. Mwenyezi Mungu akipenda basi tutapata uwongofu.”

قَالُوا دُعْلَنَّا رَبَّكَ يُبَيِّنُ لَنَا مَا هَيَّ إِنَّ الْبَقَرَ شَبَةً
عَلَيْنَا طَ وَإِنَّا إِنْ شَاءَ اللَّهُ لَمُهْتَدُونَ ﴿٥٠﴾

2:71 Musa akasema: “Allah anasema ni ng’ombe ambaye hatumiwi kulima ardhi wala kumwagia maji mimea, mzima, hana dosari.”^③ Wakajibu: “Sasa umeleta haki. Kisha wakam-chinja ng’ombe, ingawa hawakuwa karibu kufanya hivyo.

قَالَ إِنَّهُ يَقُولُ إِنَّهَا بَقَرَةٌ لَّا ذُو لُّثْبَرٍ أَلْسَنْصَرِ وَ
لَا تَسْقِي الْحُرْثَ جَمِيلَةٌ لَّا شَيْةٌ فِيهَا قَالُوا إِنَّا جُنْتَ
بِالْحَقِّ طَقَبَ حُوَّاهَا وَمَا كَادُوا يَفْعَلُونَ ﴿٥١﴾

2:72 Na kumbukeni mlipo muuwa mtu, kisha mkabishana baina yenu na hali Mwenyezi Mungu ni mwenye kuyatoa mliyo kuwa mkiyaficha.

وَإِذْ قَتَلْتُمْ نَفْسًا فَأَذْرَعْتُمْ فِيهَا طَ وَاللَّهُ مُحْرِجٌ مَا كُنْتُمْ
تَشْتَهِيُونَ ﴿٥٢﴾

Maoni

^① Manabii wametakasika na kusema uwongo, kudhihaki, na kuwafanya mzaha wengine; hata hivyo, ucheshi ni sifa ya kupendeza ambayo inaweza kupatikana kwao.

^② Maagizo ya kinabii yanapaswa kutiwa bila maswali. Kujaribu kutoa mantiki ya kibinafsi ni tabia ya watu wasio na heshima.

^③ Huu ni ukumbusho kwamba kuuliza maswali yasiyo ya lazima katika mambo ya dini kunaleta matatizo tu.

2:73 **Basi** tukasema: “Mpigeni maiti kwa sehemu ya ng’ombe.” Hivyo Mwenyezi Mungu atawafufua wafu, na anakuonyesheni Ishara zake ili mpate kufahamu.

فَقُلْنَا أَصْرِبُوهُ كُلُّهُ بِعَضْهَا ۖ كَذِلِكَ يُحِيِّ اللَّهُ الْمَوْتَىٰ وَ
يُرِيكُمْ أَيْتِهِ لَعْلَكُمْ تَعْقِلُونَ ②

2:74 **Kisha** mioyo yenu ikawa migumu baada ya hapo, hivyo ni kama mawe, bali ni migumu zaidi. Kwani mionganoni mwa mawe kuna yanay-otimbuka mito, na kuna mengine yanapasuka yakinatoka maji ndani yake, na kuna mengine huanguka kwa sababu ya khofu ya Mwenyezi Mungu, na Mwenyezi Mungu si mwene kughafilika na vitendo vyenu.

ثُمَّ قَسَطْ قُلُوبُكُمْ مِّنْ بَعْدِ ذِلْكَ فَهِيَ كَالْحَجَارَاتِ أَوْ
أَشَدُّ قَسْوَةً ۖ وَإِنَّ مِنَ الْحَجَارَاتِ لَيَأْتِيَنَّهُ جَرْمٌ مِّنْهُ الْأَنْهَرُ
وَإِنَّ مِنْهَا لَيَأْتِيَنَّهُ فَيَخْرُجُ مِنْهُ الْبَآءُ ۖ وَإِنَّ مِنْهَا لَيَأْتِيَنَّهُ
يَهِبِطُ مِنْ خُشْيَةِ اللَّهِ ۖ وَمَا اللَّهُ بِغَافِلٍ عَمَّا تَعْمَلُونَ ③

2:75 **Basi** Enyi Waumini! Je, muna matumaini haya ya kwamba wataamini kwa ajili yenu na hali lipo kundi mionganoni mwao linalosikiliza neno la Mwenyezi Mungu, kisha wangelibadili kwa makusudi hata baada ya kulifahamu? ②

أَفَتَطَعُونَ أَنْ يُؤْمِنُوا لَهُمْ وَقَدْ كَانَ فَرِيقٌ مِّنْهُمْ
يَسْمَعُونَ كَلِمَاتَ اللَّهِ ثُمَّ يَرْفُوْهُ مِنْ بَعْدِ مَا عَقَلُوا
وَهُمْ يَعْلَمُونَ ④

2:76 **Na** wanapokutana na Waumini husema: “Tumeamini,” na wanapo kuwa peke yao wao kwa wao husema “Je, munaeleza mbele yao ilimu ambayo Mwenyezi Mungu

وَإِذَا لَقُوا النَّاسَ إِذَا مَسُوا أَقْالُوكُمْ أَمْنًا ۖ وَإِذَا أَخْلَأْتُمْهُمْ إِلَى
بَعْضِ قَالُوكُمْ أَنْهِيَ شُوْرَهُمْ بِسَاقَتْهُمُ اللَّهُ عَلَيْكُمْ لِيَحَاجُوكُمْ

Mada

- Uthibitisho wa uwezo wa Mwenyezi Mungu wa kuwafufua wafu.
- Ugumu wa mioyo ya Wayahudi.
- Namna ambayo Wayahudi wangeficha ukweli.
- Unafiki wa Wayahudi.

Maoni

① Hii inaonyesha hatari ya moyo mgumu.

② Ufisadi wa mwanachuoni ni uharibifu zaidi kuliko ubaya unaofanywa na umma, kwani wao huchukua uwongofu kwa wanachuoni, wakifuata kauli zao, na kuchukua vitendo vyao kuwa ni mifano. Kwa hivyo, ikiwa wasomi wanafuata mafundisho au tabia potovu, ni vipi umma utabaki kuongozwa?

aliyokufunulieni ili waweke hoja juu yenu mbele ya Mola wenu Mlezi? Je, hamuna akili?”^①

بِهِ عَدَّ رَأِلْكُمْ طَ أَفَلَا تَعْقِلُونَ ﴿٤٧﴾

2:77 Je! hawajui kwamba Mwenyezi Mungu anayajua wanayo yaficha na wanayo yatangaza?

2:78 Na mionganoni mwao wamo watu wasiojua kusoma na kuandika ambao hawana elimu ya Kitabu ila kusoma kwa kumbukumbu au uwongo uliozushwa, na hawana isipokuwa kudhania tu.

2:79 Basi maangamivu ni kwa wale wanao andika Kitabu kwa mikono yao, kisha wakasema: Hiki kimetoka kwa Mwenyezi Mungu, ili kupata thamani ndogo. Basi maangamivu ni kwao kwa yale iliyoyaandika mikono yao, na maangamivu ni kwao kwa yale waliyo yachuma.

2:80 Na wakasema: "Hautatugusa Moto ila kwa siku chache zenyenye kuhesabika." Ewe Mtume kipenzi! Sema: Je! mmefunga ahadi na Mwenyezi Mungu? (Ikiwa ni hivyo) basi Mwenyezi Mungu hatavunja ahadi yake, au munamsingizia Mwenyezi Mungu msiyoyajua."

2:81 Hakika aliye chuma dhambi,^② na Dhambi

فَوَيْلٌ لِّلَّذِينَ يَكْتُبُونَ الْكِتَابَ بِاِيْدِيهِمْ ثُمَّ يَقُولُونَ هَذَا مِنْ عِنْدِ اللَّهِ لِيُشْتَرِوْ اِبْهَثَنَا قَلِيلًا فَوَيْلٌ لَّهُمْ مِّمَّا كَتَبْتُ اِيْدِيهِمْ وَوَيْلٌ لَّهُمْ مِّمَّا يَكْسِبُونَ ﴿٤٨﴾

وَقَالُوا لَنْ تَمَسَّنَا النَّارُ اِلَّا اَيَّامًا مَّا مُدُودَةٌ قُلْ اَتَخَرُّضُ عَنْ عَهْدِ اللَّهِ عَهْدَ اَفَلَنْ يُخْلِفَ اللَّهُ عَهْدَهُ اَمْ تَقُولُونَ عَلَى اللَّهِ مَا لَا تَعْلَمُونَ ﴿٤٩﴾

Mada

- Ni onyo kwa Mayahudi kwamba Mwenyezi Mungu Mtukufu anajua mambo yaliyo dhahiri na yaliyofichika.
- Hali ya kundi lisilo na elimu mionganoni mwa Wayahudi.
- Upotoshaji wa maandishi wa wanazuoni wa Kiyahudi na mawaidha yanayohusiana na hili.
- Itikadi ya uwongo ya Mayahudi kuhusu adhabu ya Jahannam.
- Sheria ya Mungu kuhusu malipo na adhabu.

Maoni

^① Hii inadhihirisha jinsi kuficha ukweli na kuficha sifa za Mtume Mpenzi صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ ilikuwa ni tabia ya Mayahudi.

^② Hapa “dhambi” maana yake ni ushirikina na ukafiri.

yake ikamzunguka,^① basi hao ndio watu wa Motoni, watacaa humo milele

أَصْحَبُ الْتَّارِيْخُ هُمْ فِيهَا خَلِدُوْنَ^{٨١}

2:82 Na wanao amini, na wakatenda mema, hao ndio watu wa Peponi, watacaa humo milele.

هُمْ فِيهَا خَلِدُوْنَ^{٨٢}

2:83 Na kumbuka tulipochukua ahadi kwa Wana wa Israeli: "Msimuabudu yejote isipokuwa Mwenyezi Mungu, na wafanyieni wema wazazi wawili na jamaa zenu na mayatima na masikini, na semenii na watu kwa wema,^② na simamisheni Sala na toeni zaka. Lakini nyinyi mligueka isipo kuwa wachache mionganii mwenu, na nyinyi (kwa vyovyote vile) ni wale wanao jitenga na amri za Mwenyezi Mungu.^③

وَإِذَا أَخْذَنَا مِيقَاتَقَبْنَى إِسْرَائِيلَ لَا تَعْبُدُوْنَ إِلَّا اللَّهُ قَبْرَهُ وَإِلَّا الَّذِينَ إِحْسَانًا وَذِي الْقُرْبَى وَالْيَتَامَى وَالْمَسَاكِينُ وَقُولُوا لِلنَّاسِ حُسْنًا وَآتَيْمُوا الصَّلَاةَ وَأَتُوا الرَّكْوَةَ شُمَّ تَوَلَّتُمْ إِلَّا قَلِيلًا مِنْكُمْ وَأَنْتُمْ مُعْرِضُونَ^{٨٣}

2:84 Na kumbukeni tulipokuapisheni kwamba hamtamwaga damu zenu, na wala msiwatoe watu wenu katika makazi yenu. Kisha mkakiri, na nyinyi mnashuhudia haya.

وَإِذَا أَخْذَنَا مِيقَاتَقَبْرَكُمْ لَا تَسْفَكُوْنَ دَمَاءَكُمْ وَلَا تُخْرِجُوْنَ أَنْفُسَكُمْ مِنْ دِيَارِكُمْ ثُمَّ أَقْرَرْتُمْ وَأَنْتُمْ تَشَهَدُوْنَ شُمَّ أَنْتُمْ هُوَ لَا تَقْتَلُوْنَ أَنْفُسَكُمْ وَتُخْرِجُوْنَ فَرِيقًا مِنْكُمْ

Mada

- Amri walizopewa Waisraeli wakati wa ahadi yao.
- Jinsi Waisraeli walivyopinga amri za Mungu.

Maoni

- ① Maana yake milango yote ya wokovu imefungwa kwa ajili yake na anakufa akiwa mshirikina au kafiri.
- ② Kuzungumza kwa adabu kunamaanisha kuhimiza mema na kukemea maovu kwa njia mbalimbali, ikiwa ni pamoja na kufundisha, kutoa miyahara, na kutoa ushauri.
- ③ Hii inaonesha ni tabia ya Waisraeli kugeuka na kuacha amri za Mwenyezi Mungu Mtukufu na kuvunja ahadi waliomuahidi.

kwenye makazi yao, mkisaidiana kwa dhambi na uadui dhidi yao, na wakukujieni mateka mnawakomboa, ijapokuwa awali mmeharimishiwa kuwafukuza. Basi je, mnaamini baadhi ya maamrisho ya Mwenyezi Mungu na mnayakataa mengine.^① Basi ni nini malipo ya mwenye kufanya hayo mionganini mwenu, isipokuwa kudhalilishwa katika maisha ya dunia,^② na Siku ya Kiyama watarudishwa kwenye adhabu kali, na Mwenyezi Mungu si mwenye kughafilika na vitendo vyenu.

مِنْ دِيَارِهِمْ نَّتَظَهِرُونَ عَلَيْهِمْ بِالْأَثْمِ وَالْعُدُوانِ طَ وَإِنْ يَأْتِيْكُمْ أَسْرَى تُفْدَوْهُمْ وَهُوَ مَحَرَّمٌ عَلَيْكُمْ إِخْرَاجُهُمْ أَفَتُؤْمِنُونَ بِعَيْنِ الْكِتَابِ وَتَكْفُرُونَ بِعَيْنِ فَيَا جَزَاءً مَّنْ يَفْعَلُ ذَلِكَ مِنْكُمْ إِلَّا خَرْجٌ فِي الْحَيَاةِ الدُّنْيَا وَبِيَوْمِ الْقِيَمَةِ يُرَدُّونَ إِلَى آشَدِ

الْعَذَابِ طَ وَمَا اللَّهُ بِغَافِلٍ عَمَّا تَعْمَلُونَ ^{٨٥}

2:86 Hawa ndio watu walio nunua uhai wa dunia kwa Akhera; basi hawatapunguziwa adhabu wala hawatanusuriwa.

أُولَئِكَ الَّذِينَ اشْتَرَوُ الْحَيَاةَ الدُّنْيَا بِالْآخِرَةِ فَلَا يُخَفِّفُ عَنْهُمُ الْعَذَابُ وَلَا هُمْ يُضْرُبُونَ ^{٨٦}

2:87 Na hakika tulimpa Musa Kitabu, na tukafuatisha baada yake Mitume, na tukampa Isa bin Maryam Ishara zilizo wazi na tukamsaidia kwa Roho Mtakatifu,^③ hivyo (enyi Wana wa Israeli!) Je! (haikuwa kawaida yenu kwamba) kila alipokujieni Mtume na yale ambayo hayapendwi na nafsi zenu, mlifanya kiburi, mlikadhibisha wengine, na wengine mkawaua.

وَلَقَدْ أَتَيْنَا مُوسَى الْكِتَابَ وَقَيْنَاءَ مِنْ بَعْدِهِ بِالرَّسُولِ وَأَتَيْنَا عِيسَى ابْنَ مَرْيَمَ الْبَيْتَ وَأَيَّدْنَاهُ بِرُوحِ الْقُدْسِ أَفَكُلَّمَا جَاءَكُمْ رَسُولٌ بِمَا لَمْ تَهُوَى أَنْفُسُكُمْ أُسْتَيْرِبْرُتُمْ فَقَرِيقًا كَذَبْتُمْ وَفَرِيقًا قَاتَلُونَ ^{٨٧}

Mada

■ Kufika mfululizo kwa manabii kati ya Waisraeli, na Wayahudi kuwaua.

Maoni

^① Ni lazima kuamini mafundisho yote ya Uislamu na kutekeleza maamrisho yake ni lazima. Hakuna mtu anayeepushwa na kufuata sheria za Uislamu; yejote anayejiona kuwa amesamehewa kutokana na hali yake ya kiroho au kitu kingine ni kafiri.

^② Kupinga dini kwa ajili ya kuunga mkono mtu fulani kunapelekea adhabu ya Akhera, bali pia ni sababu ya kudhalilika duniani.

^③ Mwenyezi Mungu Mtukufu alimsaidia Mtume ̄Isā kuitia kwa malaika mkuu Jibril - عَلَيْهِ السَّلَامُ - wale wanaopendwa na Mwenyezi Mungu Mtukufu wamepewa uwezo wa kuwasaidia wengine.

2:88 Na Mayahudi wakasema, "Miyo yetu imefunikwa." Bali Mwenyezi Mungu amewalaani kwa sababu ya ukafiri wao, na ni wachache tu mionganoni mwao wanaoamini.

وَقَالُوا قُلُّهُمْ بَلْ لَعْنَهُمُ اللَّهُ بِكُفْرِهِمْ فَقَلِيلًا
مَّا يُؤْمِنُونَ ⑧

2:89 Na kilipo wajia Kitabu hicho cha Mwenyezi Mungu kinachosadikisha yale waliyo nayo, na kabla ya hayo walikuwa wakitafuta ushindi juu ya makafiri kupidia Nabii huyu, basi alipowajia (Nabi huyu) ambaye walimtambua, wakamkanusha, basi laana ya Mwenyezi Mungu iwe juu ya wanao kanusha.

وَلَمَّا جَاءَهُمْ كِتَابٌ مِّنْ عَنْدِ اللَّهِ مُصَدِّقٌ لِمَا مَعَهُمْ وَ كَانُوا
مِنْ قَبْلٍ يُسَيِّرُهُنَّ عَلَى الظَّنِّينَ كَفَرُوا حَتَّىٰ جَاءَهُمْ
مَا عَرَفُوا كَفَرُوا بِهِ فَلَعْنَةُ اللَّهِ عَلَى الْكُفَّارِينَ ⑨

2:90 Ni ubaya ulioje walio jiuzia nafsi zao, nayo ni kukataa kwao aliyo yateremsha Mwenyezi Mungu, ⑩ kwa ajili ya husuda^② kwamba Mwenyezi Mungu kwa fadhila zake, huteremsha wahyi juu ya amtakaye katika waja wake, basi watu hawa wakawa wanastahiki ghadhabu juu ya ghadhabu, na iko adhabu ya kufedhehesha kwa makafiri.

بِئْسَمَا اشْتَرَوْا إِهْ أَنْفَسَهُمْ أَنْ يَلْغُفُوا بِإِيمَانِهِمْ
أَنْ يُنْزِلَ اللَّهُ مِنْ فَصْلِهِ عَلَىٰ مَنْ يَشَاءُ مِنْ عِبَادِهِ فَبَاعْدُ
بِغَضَبٍ عَلَىٰ غَضَبٍ وَلِلْكُفَّارِينَ عَذَابٌ مُّهِينٌ ⑩

2:91 Na wanapo ambiwa: Yaaminini aliyo yateremsha Mwenyezi Mungu. Wanasema: "Tunaamini tuliyo teremshiwa sisi. Na wanakataa isipokuwa taurati, na hali hiyo (Qurani) nayo ni haki inayosadikisha waliyo kuwa nayo. Ewe Mtume Mtume! sema:

وَإِذَا قِيلَ لَهُمْ أَمْنُوا بِإِيمَانِهِمْ قَالُوا أَنْزَلَ اللَّهُ أُنْزَلَ مِنْ بَيْنَ
أُنْزِلَ عَلَيْنَا وَيَكْفُرُونَ بِمَا وَرَأَوْا وَهُوَ الْحَقُّ مُصَدِّقاً
لِمَا مَعَهُمْ قُلْ فَلِمَ تَقْتُلُونَ أُنْبِيَاءَ اللَّهِ مِنْ قَبْلِ إِنْ

Mada

- Hali ya Mayahudi kabla na baada ya kuwasili kwa Mtume kipenzi صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ.
- Mayahudi kutoukubali Uislamu kwa sababu ya husuda.
- Uongo wa madai ya Mayahudi kwamba wanaiamini Taurati.

Maoni

① Ukarifiri badala ya Imani, dhambi badala ya wema, uasi badala ya utiifu, na ghadhabu ya Mwenyezi Mungu Mtukufu badala ya radhi yake ni biashara yenye hasara kubwa mno.

② Kutafuta mamlaka na cheo cha kidunia kunazua wivu moyoni; na wivu ni ugonjwa mbaya ambao unaweza kumpeleka mtu kwenye ukafiri.

“Enyi Mayahudi! Basi kwa nini mliwaua Mambii wa Mwenyezi Mungu hapo kabla, ikiwa nyinyi mlikuwa waumini?”^①

كُنْتُمْ مُّؤْمِنِينَ ٩١

2:92 Na hakika Musa alikujeni na Ishara zilizo wazi, kisha mkamuabudu ndama baada yake, na mkawa madhalimu.

وَلَقَدْ جَاءَكُمْ مُّوسَىٰ بِالْبُيُّنَاتِ ثُمَّ أَتَخَذُتُمُ الْعِجْلَ مِنْ
بَعْدِهِ وَأَنْتُمْ ظَلِيلُونَ ٩٢

2:93 Na tulipokuapisheni, na tukauinua mlima Sinai juu ya vichwa vyenu, (na tukasema) Shikamaneni kwa nguvu na tuliyo kupeni, na sikilizeni.”^② Wakasema: Tumesikia na tumeasi. Na nyoyo zao zikajaa ndama kwa ukafiri wao. Ewe Mtume Mpenzi! Sema: Ni ubaya ulioje inayokuamrisheni imani yenu ikiwa nyinyi ni Waumini.

وَإِذَا أَخْذَنَا مِثَاقَكُمْ وَرَفَعْنَا فَوْقَكُمُ الطُّورَ طُحْدُوا
مَا أَتَيْنَكُمْ بِقُوَّةٍ وَأَسْمَعْنَا طَقَالُوا سَمِعْنَا وَعَصَيْنَا وَ
أُشْرِبُوا فِي قُلُوبِهِمُ الْعِجْلَ بِكُفْرِهِمْ طُقْلِ بِعَسِيَا
يَأْمُرُكُمْ بِهِ إِيمَانُكُمْ إِنْ كُنْتُمْ مُّؤْمِنِينَ ٩٣

2:94 Ewe Mtume Mpenzi! Sema: Ikiwa nyumba ya Akhera iko kwa Mwenyezi Mungu kwa ajili yenu tu, bila ya watu wengine, basi tamanini mauti ikiwa nyinyi ni wakweli.”^③

قُلْ إِنْ كَانَتْ لَكُمُ الدَّارُ الْآخِرَةُ عِنْ دِرَرِ اللَّهِ خَالِصَةً مِنْ
دُونِ النَّاسِ فَتَتَنَّوُ الْمَوْتَ إِنْ كُنْتُمْ صَدِيقِينَ ٩٤

2:95 Na wala hawatatamani kifo kamwe kwa sababu ya maovu yao, na Mwenyezi Mungu anawajua vyema madhalimu.

وَلَنْ يَئْتِيَنَّهُ أَبَدًا إِبَاقَدَمَتْ أَيْدِيهِمْ طَوَالِلُهُ عَلَيْهِمْ
بِالظَّلِيلِينَ ٩٥

Mada

- Kuweka ushahidi dhidi ya Mayahudi kwa kuwataja Waisraeli walioabudu ndama.
- Kukanusha madai ya Mayahudi kwamba Pepo ni kwa ajili yao tu.

Maoni

^① Wana wa Israeli walioishi zama za Mtume ﷺ walikuwa hawajawaua Mitume, lakini walikubali kitendo cha wauaji na wangewatukuza, hivyo wakajumuisha mionganoni mwa wauaji.

^② Aya hii inaeleza jinsi kuamini Kitabu cha Mwenyezi Mungu Mtukufu kunajumuisha kuzingatia sheria zake zote na kufuata maamrisho yake yote.

^③ Kupenda kifo na kutamani kukutana na Mwenyezi Mungu Mtukufu ni sifa ya wachamungu, hata hivyo, kutamani kifo kutokana na changamoto za kidunia kunapinga subira, kunyenyeka, na kumtegemea Mwenyezi Mungu Mtukufu, na haijuzu.

2:96 Na hakika utawaona wanashinda watu wote kwa pupa ya kuishi; na mionganini mwa washirikina, mmoja wao anatamani lau atahu-ishwa miaka elfu moja.^① Na hayo ya kupewa maisha hayatakuwa muokozi na adhabu, na Mwenyezi Mungu anayaona wanayoyafanya.

وَلَتَجِدَنَّهُمْ أَحْرَصَ النَّاسَ عَلَى حَيَاةٍ وَمِنَ الْأَنْذِينِ
أَشَرَّ كُوَا يَوْمًا حَرْبُهُمْ لَوْيَعْمَرُ أَلْفَسَنَةٍ وَمَا
هُوَ بِإِرْزَاحٍ مِنَ الْعَذَابِ أَنْ يَعْمَرْ طَوَّافُهُ بَصِيرٌ
بِسَائِيْعَبْلُونَ^{٩٦}

2:97 Ewe Mtume kipenzi! Sema: Ambaye ni adui wa Jibril (na awe); Hakika ameiteremsha (Qur'ani) moyoni mwako kwa idhini ya Mwenyezi Mungu, inayosadikisha yaliokuwa kabla yake, na ni uwongofu na bishara kwa Waumini.

قُلْ مَنْ كَانَ عَدُوًّا لِّلْجِبْرِيلَ فَإِنَّهُ نَزَّلَهُ عَلَى قَلْبِكَ
بِإِذْنِ اللَّهِ مُصَدِّقًا لِّمَا بَيْنَ يَدَيْهِ وَهُنَّ إِلَيْهِ بُشْرًا
لِلْيَوْمِ الْمُنِيبِينَ^{٩٧}

2:98 Ambaye ni adui wa Mwenyezi Mungu, na Malaika wake, na Mitume wake, na Jibril, na Mikail, basi Mwenyezi Mungu ni adui wa makafiri.”^②

مَنْ كَانَ عَدُوًّا لِّلَّهِ وَمَلِكِتِهِ وَرَسُولِهِ وَجِبْرِيلَ وَ
مِيكَلَ فَإِنَّ اللَّهَ عَذُولٌ لِّلْكُفَّارِينَ^{٩٨}

2:99 Na kwa yakini tumekuteremshia Aya zilizo wazi, na hawazikatai ila waasi.

وَلَقَدْ أَنْزَلْنَا إِلَيْكَ آيَاتٍ بَيِّنَاتٍ وَمَا يَكْفُرُ بِهَا إِلَّا
الْفَسِقُونَ^{٩٩}

2:100 Na kila walipofunga ahadi, kundi mionganini mwao lilikivunja, bali wengi wao hawaamini.

أَوْ كُلَّبَا عَاهَدُوا عَاهَدًا أَنْبَأَنَّهُ فَرِيقٌ مِنْهُمْ بَلْ أَنْتُمْ فِيهِمْ
لَا يُؤْمِنُونَ^{١٠٠}

Mada

- Kutamani kwa Mayahudi na washirikina kubaki hai.
- Uadui wa Wayahudi kwa Malaika Jibril عَلَيْهِ السَّلَامُ.
- Uadui kwa waja wema wa Mwenyezi Mungu ni uadui kwa Mwenyezi Mungu Mtukufu.
- Mayahudi wakivunja ahadi ya kumwamini Mtume kipenzi صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ.

Maoni

^① Makafiri wanatamani maisha ya kidunia na wanakimbia mauti ambapo Muumini wa kweli atatamani maisha tu ili kuongeza amali zake njema na kukusanya malipo ya Akhera.

^② Uadui dhidi ya Manabii na Malaika watukufu ni kufuru na inaleta ghadhabu ya Mwenyezi Mungu. Uadui dhidi ya waja wapenzi wa Mwenyezi Mungu Mtukufu ni sawa na uadui kwa Mwenyezi Mungu Mtukufu.

2:101 Na alipowajia Mtume kutoka kwa Mwenyezi Mungu ambaye anasadikisha waliyo nayo, kundi moja katika Watu wa Kitabu walikitupa Kitabu cha Mwenyezi Mungu nyuma ya migongo yao kama kwamba hawajui lolote.^①

وَلَمَّا جَاءَهُمْ رَسُولٌ مِّنْ عِنْدِ اللَّهِ مُصَدِّقٌ لِّمَا مَعَهُمْ
نَبَذُ فِي قِيمٍ مِّنَ الَّذِينَ أَنْتُمْ تُوَلِّنَّكُمْ كِتَابَ اللَّهِ وَرَأَيْتُمْ
ظُهُورَ رَاهِمٍ كَانُوكُمْ لَا يَعْلَمُونَ^(١)

2:102 Na walifuata uchawi wanaousoma mashetani katika enzi ya Suleiman. Na Suleiman hakukufuru;^② bali walikufuru mashet'ani wakiwafundisha watu uchawi na yaliyoteremshwa kwa Malaika wawili, Harūt na Maruta, katika Baabil;^③ Na hao wawili hawakumfundisha ye yote mpaka waseme: "Sisi ni mtihani tu, basi msiharibu imani yenu." Wangejifunza (watu) kutoka kwa hao wawili (uchawi ambao) kupitia kwayo wangetenganisha baina ya mwanamme na mkewe, na kwa hili wasingeweza kumdhuru mtu ye yote bila ya amri ya Mwenyezi Mungu,^④ na walikuwa wakijifunza jambo ambalo lingewadhuru^⑤ na sio kuwanufaisha;

وَاتَّبَعُوا مَا تَشْوِلُ الشَّيَاطِينُ عَلَىٰ مُلْكِ سُلَيْمَانَ وَمَا كَفَرَ
سُلَيْمَانُ وَلِكُنَّ الشَّيَاطِينُ كُفَّرُوا إِعْلَمُونَ النَّاسُ السِّحْرُ
وَمَا أُنْزَلَ عَلَى الْمَلَكِينَ بِإِبْرَاهِيمَ هَارُوتَ وَمَارُوتَ وَ
مَا يَعْلَمُونَ مِنْ أَحَدٍ حَتَّىٰ يَقُولُ لَا إِلَهَ إِلَّا هُنْ فَتَّاهُ
فَلَا تَكُفُّرُ طَبَّاسَيْلَمُونَ مِنْهُمَا مَا يُقْرِئُونَ بِهِ بَيْنَ الْمُرْءَ
وَرَوْجِهِ طَبَّاسَيْلَمُونَ وَمَا هُمْ بِضَارَّيْنَ بِهِ مِنْ أَحَدٍ إِلَّا يَادُنْ
اللَّهِ طَبَّاسَيْلَمُونَ مَا يَضْرُهُمْ وَلَا يَنْعَهُمْ طَبَّاسَيْلَمُونَ وَلَقَدْ

Mada

- Kukanusha madai ya uwongo ya uchawi dhidi ya Mtume Sulaymān عَلَيْهِ السَّلَام na hadithi ya Hārūt na Mārūt.

Maoni

- ① Ingawa Mayahudi walikuwa na heshima kubwa kwa Taurati, hawakutii amri yake ya kumwamini Nabii wa Mwisho صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ, kwa hivyo ikawa ni kama wamekitupa kitabu nyuma ya migongo yao.
- ② Baadhi ya watu walimtu humu Mtume Sulaymān عَلَيْهِ السَّلَام ya uchawi. Tuhuma hii inakanushwa hapa.
- ③ Hārūt na Maruta ni Malaika, na Malaika wote hawana dhambi. Hadithi za ajabu zinazosambazwa juu yao zilitungwa na Mayahudi na ni uongo.
- ④ Sababu na athari hatimaye hutawaliwa na amri ya Mwenyezi Mungu Mtukufu; Mwenyezi Mungu Mtukufu akipenda, moto hautaunguza, maji hayatakata kiu, na dawa haitapona.
- ⑤ Ikiwa uchawi unaweza kuleta madhara, basi Aya za Quran bila shaka zinaweza kutibu. Vivyo hivyo, ikiwa makafiri wanaweza kuwadhuru wengine kwa uchawi, basi watu wateule wa Mwenyezi Mungu wanaweza kuwanufaisha watu kwa njia ya karama.

na bila shaka wanajua kwamba yejote aliye kubali mpango huu hana sehemu yoyote katika Akhera; na ni ubaya ulioje walichouzia nafsi zao; kama wangejua.

عَلَيْهِمُ الْكِنْ اشْتَرَاهُ مَالَهُ فِي الْآخِرَةِ مِنْ خَلَقٍ فَلَمْ يَسَّ
مَا شَرَوْا إِلَهَ أَنفُسُهُمْ طَلَّ كَانُوا يَعْلَمُونَ ﴿١٢﴾

2:103 Na lau wangeli amini na wakashika Uchamungu, basi malipo yatokayo kwa Mwenyezi Mungu ni bora; laiti wangejua.

وَلَوْ أَنَّهُمْ آمَنُوا أَتَقْوَى الْمُتُوبَةُ مِنْ عَمِدِ اللَّهِ حِيرَطَ لَوْ كَانُوا
يَعْلَمُونَ ﴿١٣﴾

2:104 Enyi wa umini! musiseme “Rā’inā” na semenii, “Undhurna!”^① na sikilizeni, na makafiri watapata adhabu iumizayo.

يَا أَيُّهَا النِّبِيُّنَ آمَنُوا لَا تَقُولُوا سَاعَةً قُلُّوا إِنْظَرُنَا
وَاسْمَعُوا وَلِلْكُفَّارِ يُنَزَّلُ عَذَابٌ أَلِيمٌ ﴿١٤﴾

2:105 (Enyi Waislamu!) Hawataki makafiri katika Watu wa Kitabu wala washirikina muteremshiwe wema wowote kutoka kwa Mola wenu Mlezi. Mwenyezi Mungu humchagua kwa rehema yake amtakaye, na Mwenyezi Mungu ni mwenye fadhila kubwa.

مَآ يَوْدَأُ الَّذِينَ كَفَرُوا مِنْ أَهْلِ الْكِتَابِ وَلَا الْمُشْرِكُونَ
أَنْ يُنَزَّلَ عَلَيْكُمْ مِنْ خَيْرٍ مِنْ رَزِّكُمْ وَاللَّهُ يَعْلَمُ
بِرَحْمَتِهِ مَنْ يَشَاءُ طَوَّلَ اللَّهُ ذُو الْفَضْلِ الْعَظِيمِ ﴿١٥﴾

2:106 Tunapoifuta Aya^② au tukiwasahaulisha watu, tunaleta Aya iliyo bora au inayofanana nayo. (Ewe msikilizaji!) Hujui kwamba Mwenyezi Mungu ni Muweza juu ya kila kitu?

مَآ نَسَّخْنَا مِنْ آيَةٍ أَوْ نُسِّهَا تَأْتِ بِخَيْرٍ مِنْهَا أَوْ مِثْلَهَا طَالَمْ
تَعْلَمُ أَنَّ اللَّهَ عَلَى كُلِّ شَيْءٍ قَدِيرٌ ﴿١٦﴾

Mada

- Ubora wa imani na uchamungu.
- Adabu ya kuzungumza na Mtume صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ.
- Urafiki wa Wayahudi na kuwatakia kwao wema waislamu ni uwongo.
- Ushahidi wa dhana ya kufutwa katika hukumu za kisheria za Kiislamu.

Maoni

^① Kuwaheshimu na heshima kwa manabii watukufu ni wajibu; hairuhusiwi kusema neno juu yao ambalo hata lina chembe ndogo ya uvunjifu wa heshima. Zaidi ya hayo, aya hiyo inaeleza jinsi Mwenyezi Mungu Mwenyewe anavyowafundisha watu adabu za Mahakama ya Mtume na kutangaza hukumu za taadhima na heshima

^② Kufuta (naskh) maana yake ni kukomesha matumizi ya hukumu ya awali kwa kuzingatia hukumu inayofuata; kwa uhalsia, inaeleza tu kikomo cha muda wa hukumu iliopita.

2:107 Hujui ya kwamba ufalme wa mbingu na ardhi ni wa Mwenyezi Mungu peke yake, na kwa Mwenyezi Mungu hamuna mlinzi wala msaidizi?①

أَلَمْ تَعْلَمُ أَنَّ اللَّهَ لَهُ مُلْكُ السَّمَاوَاتِ وَالْأَرْضِ وَمَا كُلُّمُ

مِنْ دُونِ اللَّهِ مِنْ وَلِيٍّ وَلَا نَصِيرٍ ②

2:108 Au munataka kumuuliza Mtume wenu jinsi Musa alivyoulizwa hapo awali? Na mwenye kubadilisha Imani kwa ukafiri basi amepotea njia iliyonyooka.

أَمْ تُرِيدُونَ أَنْ تُسْكُنَا رَسُولَكُمْ كَمَا سِلَّمَ مُوسَىٰ مِنْ قَبْلٍ

وَمَنْ يَتَبَدَّلُ الْكُفَّارُ إِلَّا يَبْيَانٌ فَقَدْ صَلَّ سَوَاءَ السَّيِّئُ ③

2:109 Wengi mionganini mwa Watu wa Kitabu walitaka kukugeuzieni kwenye ukafiri baada ya Imani kwa sababu ya husuda iliyomo ndani ya nafsi zao,② hata baada ya kuwabainikia ukweli. Basi wasameheni na waacheni mpaka Mwenyezi Mungu alete amri yake. Bila shaka Mwenyezi Mungu ni muweza juu ya kila kitu.

وَدَكْثِيرٌ مِنْ أَهْلِ الْكِتَابِ لَوْيَرْدُونْ كُلُّمُ مِنْ بَعْدِ

إِيمَانِكُمْ كُفَّارًا حَسَدًا مِنْ عِنْدِ أَنفُسِهِمْ مِنْ بَعْدِ مَا

تَبَيَّنَ لَهُمُ الْحَقُّ فَاعْفُوا وَاصْفُحُوا حَتَّىٰ يَأْتِيَ اللَّهُ بِآمِرٍ ④

إِنَّ اللَّهَ عَلَىٰ كُلِّ شَيْءٍ قَدِيرٌ ⑤

2:110 Na simamisheni Sala, na toeni zaka, na kheri yoyote mtakayo jitangulizia nafsi zenu mtaikuta kwa Mwenyezi Mungu. Hapana shaka, Mwenyezi Mungu anayaona yote mnayoafanya.

وَأَقِبُوا الصَّلَاةَ وَأَتُوا الرِّزْكَ وَمَا تَقْدِمُوا لَا تُنْفِكُمْ

مِنْ خَيْرٍ تَجِدُوهُ إِنَّ اللَّهَ بِمَا تَعْمَلُونَ بَصِيرٌ ⑥

2:111 Na (Watu wa Kitabu) wakasema: "Hatoingia Peponi isipokuwa yule aliye

وَقَالُوا لَنْ يَدْخُلُ الْجَنَّةَ إِلَّا مَنْ كَانَ هُودًّا أَوْ نَصَارَىٰ طَبْلَكَ

Mada

- Ni onyo kwa Mayahudi baada ya kumuuliza Mtume kipenzi صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ maswali yasiyo na maana.
- Mayahudi wanataka Waislamu wawe makafiri tena baada ya kugundua ukweli wa Uislamu.
- Hukumu kuhusu swala, zaka, na kutafakari juu ya matendo.
- Mawazo yaliozushwa ya Mayahudi na Wakristo kuhusu Pepo na Sheria ya Mwenyezi Mungu inayoihusu.

Maoni

① Hakuna awezaye kusaidia kinyume na amri ya Mwenyezi Mungu Mtukufu, hata hivyo, kwa idhini yake na kupewa uwezo kutoka kwake, wengine wanaweza kutoa msaada; kuna mifano mingi ya hili katika Quran na Hadith. Waja wema wa Mwenyezi Mungu kuwasaidia watu kumethibitishwa kwa njia ya mapokezi ya wengi (tawātur) na vilevile kwa kushuhudiwa na maelfu ya watu.

② Wivu ni tabia mbaya; sio tu kwamba mtu anaacha kufanya mema kwa sababu yake, lakini pia anajishughulisha na kuwazuia wengine kufanya mema.

Mayahudi au Mkristo.” Haya ni matamanio yao yaliyozushwa, sema: Leteni ushahidi wenu ikiwa nyinyi ni wakweli.”

أَمَانُهُمْ قُلْ هَاتُوا بِرَهَنُكُمْ إِنْ كُنْتُمْ صَدِيقِينَ ﴿١١﴾

٢٩

2:112 Lakini mwenye kuuinamisha uso wake kwa ajili ya Mwenyezi Mungu na akawa mwema, basi ujira wake uko kwa Mola wake Mlezi;^① hawatakuwa na khofu wala hawatahuzunika.

بَلِّيٌّ مَنْ أَسْلَمَ وَجْهَهُ لِلَّهِ وَهُوَ مُحْسِنٌ فَلَهُ أَجْرٌ إِنَّهُ عَنْ دَرِيَّةٍ

رَأَيْهِ وَلَا خَوْفٌ عَلَيْهِمْ وَلَا هُمْ يَحْزُنُونَ ﴿١٢﴾

2:113 Na Mayahudi wakasema: “Wakristo hawafuati chochote” na Wakristo wakasema, “Mayahudi hawafuati chochote,” huku wanasma Kitabu; Hivyo wajinga wakasema sawa na kauli yao, basi Siku ya Kiyama Mwenyezi Mungu atahukumu baina yao katika yale wanayo hitilafiana.

وَقَالَتِ الْيَهُودُ لَيْسَتِ النَّصْرَى عَلَى شَيْءٍ وَقَالَتِ

النَّصْرَى لِيَسْتِ الْيَهُودُ عَلَى شَيْءٍ وَهُمْ يَشْتُونَ الْكِتَابَ

كَذِيلَكَ قَالَ الَّذِينَ لَا يَعْلَمُونَ مِثْلَ قَوْلِهِمْ فَالَّهُ يَعْلَمُ

بِيَهُمْ يَوْمَ الْقِيَمَةِ فَيَمَا كَانُوا فِيهِ يَخْلِفُونَ ﴿١٣﴾

2:114 Na ni nani dhaalimu mkubwa kuliko yule anayezuia Misikiti ya Mwenyezi Mungu kutajwa jina lake humo.^② Na akajitahidi kuiharibu;^③ Watu hawa haikuwa kwao kuingia Misikitini ila kwa khofu. Kwao, kuna

وَمَنْ أَظْلَمُ مِنْ مَنْ نَعَمَ مسِجِدَ اللَّهِ أَنْ يُدْكَرَ فِيهَا أُسْنَةً

وَسَعَى فِي خَرَابِهَا أُولَئِكَ مَا كَانَ لَهُمْ أَنْ يَدْخُلُوهَا

إِلَّا حَارَبُوكُمْ لَهُمْ فِي الدُّنْيَا حُرْزٌ وَلَهُمْ فِي الْآخِرَةِ

Mada

- Maoni ya Mayahudi na Wakristo kuhusu wao kwa wao.
- Kuzuia Sala katika Misikiti na kujitahidi kuiharibu ni dhulma kubwa.

Maoni

^① Kigezo halisi cha kuingia Peponi ni imani thabiti na matendo mema; Mtu yejote kutoka zama yoyote mwenye imani na matendo mema ataingia Peponi. Hata hivyo, baada ya tangazo la utume na Mtume wa Mwisho، اللَّهُ عَلَيْهِ وَبَلَّهُ، imani ya asiyekubali utume wake si sawa, na hakuna kitendo kinachohesabiwa haki pasipo imani thabiti.

^② Kuzuia kumkumbuka Mwenyezi Mungu Mtukufu (dhikr) mahali popote ni uovu; hata hivyo, kosa ni kubwa zaidi msikitini, kwani Misikiti imejengwa kwa ajili ya kumwabudu na kumkumbuka Mwenyezi Mungu Mtukufu.

^③ Anayesababisha uharibifu wa msikitini kwa njia yoyote ile ni dhalimu. (Tazama Tafsir Shirat al-Jinān chini ya aya hii kwa maelezo zaidi.)

unyonge katika dunia hii na adhabu kali akhera.

عَذَابٌ عَظِيمٌ ﴿١٣﴾

2:115 **Na** Mashariki na Magharibi ni ya Mwenyezi Mungu peke yake, basi kokote munakoelekea, huko rehema ya Mwenyezi Mungu imewaelekea^① Hakika Mwenyezi Mungu ni mwenye wasaa, mjuzi.

وَإِلَهُ الْمَشْرِقُ وَالْمَغْرِبُ فَأَيْمَانًا تَوْلُوا قَمَّ وَجْهَ اللَّهِ إِنَّ اللَّهَ وَاسِعٌ عَلَيْهِمْ ﴿١٤﴾

2:116 **Na** (washirikina) wakasema, “Mwenyezi Mungu ana mwana,” Ametakasika. Bali ni vyake viliyyomo mbinguni na ardhini. Wote wamenyenyekea kwake.

وَقَالُوا تَخْدَالَ اللَّهُ وَلَدًا لَا سُبْحَانَهُ طَبْلَ لَهُ مَا فِي السَّمَاوَاتِ وَالْأَرْضِ كُلُّهُ لَهُ قُنْتُونَ ﴿١٥﴾

2:117 **Muumba** wa mbingu na ardhi bila mfano wowote uliotangulia,^② na anapo amua jambo basi huliambia tu “Kuwa” nalo likawa.^③

بَدِيعُ السَّمَاوَاتِ وَالْأَرْضِ طَرَاذَ أَذَاقَنِي أَمْرًا فَانْتَهَى يَقُولُ لَهُ كُنْ فَيَكُونُ ﴿١٦﴾

2:118 **Na** wajinga wakasema: Kwa nini Mwenyezi Mungu hasemi nasi au kwa nini haitufikii Ishara? Waliotangulia nao walisema mfano wa kauli yao hii, hivyo basi nyoyo zao

وَقَالَ الَّذِينَ لَا يَعْلَمُونَ لَوْلَا يُكَلِّمُنَا اللَّهُ أَوْ تَأْتِينَا آيَةً كَذِلِكَ قَالَ الَّذِينَ مِنْ قَبْلِهِمْ مِثْلَ قَوْلِهِمْ طَشَابَهَتْ

Mada

- Popote ulipo muelekeo wa swala, ibada ni ya Mwenyezi Mungu Mtukufu peke yake.
- Ukanushaji wa kumnasibisha mwana kwa Mwenyezi Mungu Mtukufu.
- Amri ya Mwenyezi Mungu Mtukufu inatekelezwa bila shaka.
- Kukanusha matakwa ya Mayahudi kuzungumza na Mwenyezi Mungu Mtukufu.

Maoni

^① ‘Wajh’ maana yake halisi ni uso; hata hivyo, Mwenyezi Mungu Mtukufu ametakasika na uso mfano wa uso wa viumbi, kwa hivyo aya hii inatokana na aya zisizo kuwa wazi maana yake (mutashabihāt), na Mwenyezi Mungu Mtukufu anajua zaidi kuhusu maana yake ya kweli.

^② *Badi'* maana yake ni “mtu anayeunda kitu kipyä ambacho hakijawahi kuwepo hapo awali.” Kabla ya Mwenyezi Mungu Mtukufu kuumba ardhi na mbingu, hapakuwa na ardhi au mbingu nyingine —Aliviumba kutokana na kutokuwepo.

^③ Mwenyezi Mungu hamtegemei mtu yejote kwa kazi yoyote. Uamuzi wake wa kuwateua malaika kwa ajili ya majukumu mbalimbali ni sehemu ya Hekima Yake na hautokani na haja.

Zimefanana.^① Hakika Sisi tumezibainisha Ishara kwa watu wa yakini.

قُتُوبُهُمْ قَدْ بَيَّنَا لِلْآيَتِ لِقَوْمٍ يُّوقِنُونَ^⑩

2:119 (Ewe Mtume kipenzi!) Hakika tulikutu-ma kwa haki kama mtoaji wa habari njema na mwonyajji, wala hutaulizwa kuhusu watu wa Motoni.

إِنَّا أَنْسَلْنَاكَ بِالْحَقِّ بَشِيرًا وَنَذِيرًا لَا تَسْعُلْ عَنْ

أَصْحَابِ الْجَنِّ^⑯

2:120 **Mayahudi** hawawi radhi nawe, wala Wakristo mpaka ufuate Dini yao.^② Sema: "Uwongofu wa Mwenyezi Mungu ndio uwongo-fu." Na (Ewe msikilizaji!) Ikiwa utafuata matamano yao, hata baada ya kukujia ujuzi,^③ basi hutapata mwokozi wala msaidizi kwa Mwenyezi Mungu.

وَلَنْ تَرْضِيَ عَنْكَ الْيَهُودُ وَلَا النَّصَارَى حَتَّىٰ شَتَّىٰ مَلَّتُهُمْ
قُلْ إِنَّ هُرَيْلِيَ اللَّهُ هُوَ الْهُدَىٰ وَلَئِنْ اتَّبَعْتَ أَهْوَاءَهُمْ

بَعْدَ الَّذِي جَاءَكَ مِنَ الْعِلْمِ لَا مَالَكَ مِنَ اللَّهِ مَنْ وَلِيَ وَ
لَا نَصِيرٌ^⑭

2:121 **Wale** tulio wapa Kitabu wanakisoma namna inavyopaswa, isomeke.^⑤ Watu hawa

أَلَّذِينَ أَتَيْنَاهُمُ الْكِتَبَ يَتَلَوَّهُ حَقَّ تِلَاقِهِ طُولِيَّكَ

Mada

- Maneno ya kufariji kwa Mtume kipenzi صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ wakati watu hawakukubali imani licha ya mahubiri yake.
- Tahadhari ya adhabu kwa kuwafuata Mayahudi na Wakristo.
- Wale wanaosoma Kitabu cha Mwenyezi Mungu Mtukufu kama inavyopaswa kusomwa.

Maoni

^① Uigaji wa makafiri kwa mujibu wa tabia zao za kijamii, kanuni za mavazi, na mwenendo wa jumla hauruhusiwi kwani hali ya dhahiri ni ishara ya hali ya ndani; dhahiri inaweza kuathiri hali ya ndani na hivyo kuepuka kabisa njia ya makafiri ni muhimu, ili hali yao ya dhahiri isije ikaathiri hali ya ndani ya Waislamu.

^② Kama umma, makafiri kamwe hawataridhika na Waislamu hata kama kwa nje wanaonekana tofauti mara nyingine; ni jambo la kusikitisha sana kwamba hata baada ya uzoefu mwingi unaoshuhudia ukweli huu, Waislamu bado hawazingatii.

^③ Hotuba hii si ya Mtume kipenzi صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ; Bali ni kwa kila msomaji au msikilizaji wa aya hii. Vinginevyo, inaonekana inazungumza na Mtume صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ, lakini makusudio ya hakika ni kuhutubia Ummah wake kupitia kwake, kwani Yeye hawezi kufuata matamanio ya Watu wa Kitabu.

^④ Kitabu cha Mwenyezi Mungu Mtukufu, yaani Quran, ina haki nyingi: kuheshimiwa, kupendwa, kusomwa, kueleweka, kuaminiwa, kuzingatiwa, na kufikishwa kwa wengine.

wanaiamini; na atakaye ikataa, basi hao watu ndio wenye hasara.

٢٩ ﴿٤﴾ يُؤْمِنُونَ بِهِ وَمَنْ يَكُفِرُ بِهِ فَأُولَئِكَ هُمُ الْخَسِرُونَ ﴾٤﴾

2:122 Enyi Wana wa Ya'quub! Kumbukeni neema yangu^① niliyokupeni, na kwamba nime-wapa ubora juu ya ulimwengu wote katika zama hizo.

لَيَبْيَقَ إِسْرَاءِيلَ أَدْكُرُوا نِعْمَتِي الَّتِي أَنْعَمْتُ عَلَيْكُمْ وَآتَيْتُكُمْ عَلَى الْعَلَيْمِينَ ﴾٢٣﴾

2:123 Na iogopeni siku ambayo nafsi yoyote haitatosheleza nafsi nyingine kwa lolote, na haitachukuliwa kutoka kwayo fidia, na hakuna maombi yoyote yatakayomfaa kafiri, na wao hawatanusuriwa.

وَاتَّقُوا إِيمَانًا لَا تَجِزُّ نَفْسٌ عَنْ نَفْسٍ شَيْئًا وَلَا يُقْبَلُ مُهَاجَدًا وَلَا تَنْفَعُهَا شَفَاعَةٌ وَلَا هُمْ يُنْصَرُونَ ﴾٢٤﴾

2:124 Na kumbuka Mola wake Mlezi alipo mtia mtihanini Ibrahim kwa baadhi ya maneno, naye akayatimiza. Akasema (Mwenyezi Mungu): "Mimi nitakufanya uwe kiongozi wa watu."^② Akasema (Ibrahim): Na katika vizazi vyangu pia? (Mwenyezi Mungu) akasema: "Ahadi yangu haiwafikii madhalimu.

وَإِذْ أَبْتَلَ إِبْرَاهِيمَ رَبَّهُ بِكَلِمَاتٍ قَاتَّهُمْ طَقَالَ إِنِّي جَاعِلُكَ لِلنَّاسِ إِمَامًا طَقَالَ وَمَنْ ذَرَّ إِيمَانِي طَقَالَ لَدَيْكَ الْعَهْدِ الظَّلِيمِينَ ﴾٢٥﴾

2:125 Na kumbuka tulipoifanya hiyo Nyumba (Ka'bah) kuwa ni pahali pa kukusanyika watu na amani, na Enyi Waislamu, na fanyeni sehemu aliposimama Ibraahim kuwa ni mahali

وَإِذْ جَعَلْنَا الْبَيْتَ مَثَابَةً لِلنَّاسِ وَأَمْنًا طَقَالَ تَخْذُلُ وَأَمْنٌ مَقَامِ إِبْرَاهِيمَ مُصَلِّي طَقَالَ عَهْدُنَا إِلَى إِبْرَاهِيمَ وَإِسْعَيْلَ أَنْ

Mada

- Ni ukumbusho wa neema kwa Mayahudi na amri ya wao kutafakari Akhera.
- Mtihani, kufaulu, na malipo ya Mtume Ibrāhīm عَلَيْهِ السَّلَامُ.
- Upekee wa Masjid al-Haram na amri ya kuuweka safi.

Maoni

^① Kutangaza neema ya Mwenyezi Mungu Mtukufu ni aina ya shukurani, kwa hivyo, kutaja mazazi ya Mtume yaliobarikiwa au kufanya mikusanyiko kwa madhumuni haya kunajumuishwa katika hukumu hii kwani ni ishara ya shukurani.

^② Hukumu na sheria za Kiislamu ni mitihani itokayo kwa Mwenyezi Mungu Mtukufu, na mwenye kusimama imara na kuzitekeleza inavyotakiwa, anastahiki malipo ya dunia na Akhera.

pa kuswalia^①, na tukasisitiza kwa Ibraahim na Isma'il kwamba ifanyeni nyumba yangu kuwa safi kwa ajili ya wale wanaoizunguka, wanaojitenga kwa ibada, na wanaorukuu na kusujudu.^②

طَهَرَ أَبِيَّتَ لِلظَّاهِرِينَ وَالْعَرِفِينَ وَالرُّكْعَ السُّجُودُ^{٢٥٥}

2:126 Na kumbuka Ibraahim alipoomba: Ewe Mola wangu Mlezi! Ufanye huu uwe mji wa amani, na uwaruzuku wakaazi wake katika matunda mbalimbali, wale wanaomuamini Mwenyezi Mungu na Siku ya Mwisho.”^③ Akasema (Mwenyezi Mungu): “Na atakayekufuru, basi nitamstarehesha kidogo. Kisha nitamsukumiza kwenye adhabu ya Moto. Na ni mahali pabaya sana pa kurudi.”

وَإِذْ قَالَ إِبْرَاهِيمُ رَبِّي اجْعَلْ هَذَا بَدْرَهُ أَمْنًا وَأَرْزُقْ أَهْلَهُ
مِنَ الشَّرَّاتِ مَنْ أَمْنَ مِنْهُمْ بِاللَّهِ وَالْيَوْمُ الْآخِرُ قَالَ وَ
مَنْ كَفَرَ فَأُمْتَغَهُ قَلِيلًا ثُمَّ أَضْطَرَهُ إِلَى عَذَابِ النَّارِ طَوِيلًا
بِسْمِ الرَّحْمَنِ الرَّحِيمِ^{٣٦٣}

2:127 Na Ibraahim na Ismail walipoinyanyua misingi ya Nyumba hii^④ (wakiomba), “Ewe Mola wetu! Tutaakabalie, hakika wewe ndiye Mwenye kusikia, Mjuzi.

وَإِذْ يَرْفَعُ إِبْرَاهِيمُ الْقَوَاعِدَ مِنَ الْبَيْتِ وَإِسْعِيلُ طَرَابَنَا^{٣٦٤}
تَقَبَّلُ مِنَّا إِنَّكَ أَنْتَ السَّمِيعُ الْعَلِيمُ^{٣٦٥}

Mada

- Dua ya Mtume Ibrāhīm عَلَيْهِ السَّلَام kwa Makkah.
- Ujenzi wa Ka'ba na dua za Nabii Ibrāhīm عَلَيْهِ السَّلَام na Nabii Ismā'īl عَلَيْهِ السَّلَام

Maoni

^① Jiwe lililobarikiwa na nyayo za kinabii huheshimiwa na kuinuliwa. Heshima na taadhima kwa mtume si kinyume na imani ya upweke wa Mwenyezi mungu (tawhid). Kwasababu heshima kwa sehemu aliposimama Mtume Ibrāhīm عَلَيْهِ السَّلَام inaonyeshwa wakati wa swalah yenyewe.

^② Ka'aba Tukufu na Masjid al-Haraam lazima ziwekwe safi kwa ajili ya mahujaji, wale wanaozunguka (kufanya twāwāf), wale wanaojitenga kwa ibada (i'tikāf), na wale wanaoswali. Hukumu hiyo hiyo pia inatumika kwa misikiti yote kwa ujumla.

^③ Leo, kukubaliwa dua hii ya Nabi Ibrahim inaonekana wazi na watu wote; kila aina ya chakula na matunda, kutoka duniani kote, yanapatikana hapa.

^④ Ujenzi wa masjid ni ibada kubwa na njia ya manabii watukufu.

2:128 Ewe Mola wetu Mlezi! Na utufanye sote wawili kuwa watiifu na uwajaalie kutokana na watoto wetu kuwa taifa linalotii kwako, na utuonyeshe njia za ibada^①, na utuletee rehemaya; Hakika Wewe ndiye Mwingi wa kupokea toba na Mwingi wa kuhurumia.

رَبَّنَا وَأَجْعَلْنَا مُسْلِمِينَ لَكَ وَمِنْ ذِرَيْتَنَا أَمَّةً مُّسْلِمَةً
لَكَ وَأَرَنَا مَنَاسِكَنَا وَثُبْ عَلَيْنَا إِنَّكَ أَنْتَ الشَّوَّابُ

الرَّحِيمُ
١٢٨

2:129 Ewe Mola wetu Mlezi, na uwalettee Mtume mionganini mwao. Anaye wasomea Aya zako, na anawafundisha Kitabu na hikima^②, na kuwatakasa. Hakika Wewe ndiye Mwenye kushinda, Mwenye hekima.”

رَبَّنَا وَأَبْعَثْ فِيهِمْ رَّاسُوْلًا مِّنْهُمْ يَشْرُوْعُ عَلَيْهِمْ أَيْتِكَ وَ
يُعَلِّمُهُمُ الْكِتَبَ وَالْحِكْمَةَ وَيُرِيْكِهِمْ طَ إِنَّكَ أَنْتَ الْعَزِيزُ

عَ الْحَكِيمُ
١٣٩

١٥
١٥

2:130 Na ni nani angejitenaga na Dini ya Ibrahim isipokuwa yule aliyejifanya mjinga. Na hakika tumemteuwa (Ibrahim) katika dunia hii. Na hakika yeche katika Akhera ni mionganini mwa watu wema.^③

وَمَنْ يَرْغَبُ عَنْ قِلَّةِ إِبْرَاهِيمَ إِلَّا مَنْ سَفَهَ نَفْسَهُ طَ وَلَقَدْ
أُصْطَفِيَ فِي الدُّنْيَا وَإِنَّهُ فِي الْآخِرَةِ لِمِنَ الصَّالِحِينَ^٤

إِذْ قَالَ لَهُ رَبُّهُ آمُسِيمٌ قَالَ أَسْلَمْ لِرَبِّ الْعَالَمِينَ^٥

Mada

- Dua ya Mtume Ibrāhīm عَلَيْهِ السَّلَام kwa ujio wa Mjumbe wa Mwisho.
- Dini ya Mtume Ibrāhīm عَلَيْهِ السَّلَام na ukuu wake.

Maoni

^① Kujifunza njia za ibada ni njia ya Mtume Ibrāhīm عَلَيْهِ السَّلَام; mtu anapaswa kuomba ili kupata hili na kujitahidi kwa hilo pia.

^② Aya hii inabainisha ukubwa wa Maswahaba waliofunzwa Kitabu, wakafunzwa hekima, na wakatakaswa na Mtume عَلَيْهِ وَسَلَام. Zaidi ya hayo, tunajifunza kwamba Quran nzima si rahisi kuielewa, vinginevyo Mtume kipenzi عَصَلَ اللَّهُ عَلَيْهِ وَالْهُ وَسَلَام. Zaidi ya hayo, tunajifunza kwamba Quran nzima si rahisi kuelewaka apelekwe kwa mwanachuoni aliyebobe; ukweli utadhihirika ndani ya dakika chache. Pia ni wazi kutokana na hili kwamba Hadith zinahitajika pamoja na Quran.

^③ Dalili ya dini ya kweli ni kuwa ni dini ya waliotangulia wema; kwani hizo ni dalili za uwongofu. Hapa, Mwenyezi Mungu Mtukufu ametangaza kwamba ushahidi wa ukweli wa Uislamu ni kwamba ni dini ya Mtume Ibrāhīm عَلَيْهِ السَّلَام.

2:132 Na Ibrahim na Ya'quub wakawausia wana wao kufuata Dini hii: "Enyi wanangu! Hakika Mwenyezi Mungu amekuteulieni Dini hii, basi msife ila mmekuwa Waislamu."^①

وَوَصَّىٰ بِهَاٰ إِبْرَاهِيمَ بْنَيْهِ وَيَعْقُوبَ طَلِبَنِيَّ إِنَّ اللَّهَ اصْطَفَى لِكُمُ الَّذِينَ فَلَاتَتُونَ إِلَّا وَأَنْتُم مُسْلِمُونَ ﴿٢٣﴾

2:133 (Enyi Mayahudi!) Je! Mlikuwepo wakati wa mauti ulipomfika Yaaqubu alipowaambia wanawe: Wanangu, ni nani mtakaemuabudu baada yangu? Wakasema: "Tutamuabudu Mungu wako, na Mungu wa baba zako Ibrahim, Ismail na Is-haq, Mungu Mmoja. Na sisi ni watifu Kwake."

أَمْ كُنْتُمْ شَهِدَنَ آءَ إِذْ حَضَرَ يَعْقُوبَ الْبَوْتُ لَا إِذْ قَالَ لِبْنَيْهِ مَا تَعْبُدُونَ مِنْ بَعْدِي طَلِبَنِيَّ قَالُوا نَعْبُدُ إِلَهَكَ وَإِلَهَ أَبَائِكَ إِبْرَاهِيمَ وَإِسْمَاعِيلَ وَإِسْحَاقَ إِلَهًا وَاحِدًا وَنَحْنُ لَهُ مُسْلِمُونَ ﴿٢٤﴾

2:134 Hilo ni taifa lililopita. Amali zao ni kwa ajili yao na vitendo vyenu ni kwa ajili yenu^②, wala hamutaulizwa juu ya vitendo vyao.

تَلَكَ أُمَّةٌ قَدْ خَلَتْ لَهَا مَا كَسَبَتْ وَلَكُمْ مَا كَسَبْتُمْ وَلَا تُسْأَلُونَ عَمَّا كَانُوا يَعْمَلُونَ ﴿٢٥﴾

2:135 Na Watu wa Kitabu wakasema: Kuweni Mayahudi au Manasara mtaupata uwongofu. Sema, "(Kamwe!) Bali sisi tunashika dini ya Ibrahim ambaye alikuwa amejeieka mbali na kila batili na hakuwa mionganini mwa washirikina.."^③

وَقَالُوا كُونُوا هُودًا أَوْ نَصَارَى تَهَتَّدُوا طَلْبُ مَلَةٍ إِبْرَاهِيمَ حَنِيفًا وَمَا كَانَ مِنَ الظُّرُفِكِينَ ﴿٢٦﴾

Mada

- Nabii Ibrāhīm na Nabii Ya'qūb عَلَيْهِ السَّلَام wakiwusia wana wao wasimame imara juu ya Dini ya Haki.
- Maelezo ya ushauri uliotolewa na Nabii Ya'qūb.
- Kila mtu ataona malipo na adhabu ya matendo yake kwa mujibu wa sheria ya uadilifu.
- Msisitizo wa kufuata dini ya Ibrāhīm عَلَيْهِ السَّلَام.

Maoni

^① Wazazi wasitoe tu ushauri au wosia wao kwa maelekezo ya fedha peke yake, bali wanapaswa kuwashauri watoto wao kuhusu imani sahihi, matendo mema, ukuu wa Uislamu, uthabiti, mwendelezo wa matendo mema, na kuepuka madhambi.

^② Amali za mtu binafsi zitamsaidia Akhera, lakini ikiwa mtu ana imani potovu, hatafaidika na vitendo vya wengine.

^③ Nabii Ibrāhīm عَلَيْهِ السَّلَام alikubaliwa na Mwenyezi Mungu Mtukufu kiasi kwamba dini zote zilionyesha fahari kuwa na uhusiano naye. Vile vile ni wazi kutoka katika aya hiyo kwamba kuwa katika watoto wa watu watukufu hakutoshi, isipokuwa kama matendo ya wazee hao watukufu nayo yataigwa.

2:136 **Enyi** Waislamu! Semeni, "Sisi tumemua-
mini Mwenyezi Mungu na yale yaliyo teremsh-
wa kwetu, na yaliyo teremshwa kwa Ibrahim,
na Ismail, na Is-haq, na Ya'kub, na watoto wao,
na aliyo pewa Musa na Isa, na waliyopewa
Manabii wengine kutoka kwa Mola wao Mlezi.
Hatutofautishi baina ya yelete kati yao (katika
kuwaamini)^① — na sisi tumenyenyekea kwa
Mwenyezi Mungu.

قُولُوا إِمَّا بِاللَّهِ وَمَا أُنْزِلَ إِلَيْنَا وَمَا أُنْزِلَ إِلَى إِبْرَاهِيمَ وَإِسْعَيْلَ وَإِسْلَحَ وَيَعْقُوبَ وَالْأَسْبَاطَ وَمَا أُوْتَى مُوسَى وَعِيسَى وَمَا أُوْتَى النَّبِيُّونَ مِنْ رَبِّهِمْ لَا نَفْرَقُ بَيْنَ أَهْلِ مِنْهُمْ وَنَحْنُ لَهُمُ الْمُسْلِمُونَ

2:137 **Basi** wakiamini kama mlivyo amini,
wamepata uwongofu, na wakikengeuka basi
wamo katika upinzani tu. Basi (ewe Mtume
kipenzi!) Hivi karibuni Mwenyezi Mungu
atakutoshea kukukinga na shari yao, naye ni
Mwenye kusikia, Mjuzi.

**فَإِنْ أَمْسَوْا إِيْشِيلَ مَا أَمْسَنْتُمْ بِهِ فَقَدِ اهْتَدَوْا وَإِنْ تَوَلُّو
فَإِنَّهُمْ فِي شَقَاقٍ فَسَيَكِيفُّهُمُ اللَّهُ وَهُوَ السَّمِيعُ**

العلیم ^(١٣٧)

2:138 **Na** tumechukua rangi ya Mwenyezi
Mungu.^② Ni rangi ya nani iliyo bora kuliko ya
Mwenyezi Mungu? Na sisi tunamuabudu
Yeye tu.

صِبْغَةَ اللَّهِ وَمَنْ أَحْسَنْ مِنَ اللَّهِ صِبْغَةً وَنَحْنُ لَهُ عِدُودُنَ

العديدون ^(١٣٨)

2:139 **Sema:** Je, mnabishana nasi juu ya
Mwenyezi Mungu, ijapokuwa Yeye ni Mola
wetu Mlezi na Mola wenu Mlezi, na sisi tuna
vitendo vyetu, na nyinyi muna vitendo vyenu,
na sisi tunamtakasia Yeye tu."

**قُلْ أَتَحَاجِجُونَا فِي اللَّهِ وَهُوَ بَيْنَا وَرَبُّكُمْ وَلَنَا آمِانًا
وَلَكُمْ آمِانًا وَنَحْنُ لَهُمُ الْمُحْلِصُونَ**

المحليصون ^(١٣٩)

Mada

- Dini ya manabii ndio dini pekee ya kweli.
- Imani ya Maswahaba رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُمْ ni ya kweli na ya kuigwa.
- Dini ya Mwenyezi Mungu Mtukufu ndiyo iliyo bora zaidi.
- Jibu kwa Mayahudi waliopinga utume wa Al-Muṣṭafā صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ

Maoni

^① Kwa hakika kuna tofauti ya daraja kati ya Mitume (kama ilivyoelezwa katika juzu ya tatu ya Quran), hata hivyo, hakuna tofauti baina yao katika suala la utume.

^② Usemi "rangi ya Mwenyezi Mungu" unamaanisha imani ya kweli ya dini yake.

2:140 (Enyi Watu wa Kitabu!) Je, mnasema kwamba Ibrahim, Isma'il, Is-haq, Ya'quub na watoto wao walikuwa Mayahudi au Wakristo? Sema: Je, mnajua zaidi au Mwenyezi Mungu? Na ni nani dhalimu mkubwa kuliko yule aliye na ushahidi kutoka kwa Mwenyezi Mungu na akauficha, na Mwenyezi Mungu si mwenye kughafilika na vitendo vyenu."

أَمْ تَقُولُونَ إِنَّ إِبْرَاهِيمَ وَإِسْعَيْلَ وَإِسْحَاقَ وَيَعْقُوبَ وَ
الْأَسْبَاطَ كَانُوا هُودًا أَوْ نَصَارَىٰ ۖ قُلْ إِنَّمَا أَعْلَمُ أَمْ
اللَّهُ وَمَنْ أَظْلَمُ مِمَّنْ كَتَمَ شَهَادَةً عَنْهَا مِنَ اللَّهِ وَمَا
اللَّهُ بِعَافِلٍ عَمَّا تَعْمَلُونَ ﴿١٤٠﴾

2:141 Hilo ni taifa lililopita; vitendo vyao ni vyao na vitendo vyenu ni kwa ajili yenu, wala hamtaulizwa juu ya vitendo vyao.^①

تَلَكَ أُمَّةٌ قَدْ خَلَتْ لَهَا مَا كَسَبَتْ وَلَكُمْ مَا كَسَبَتُمْ وَ
لَا تُسْكُنُونَ عَمَّا كَانُوا يَعْمَلُونَ ﴿١٤١﴾

١٤٢

Mada

- Kukanusha kuhusisha Uyahudi au Ukristo na Mtume Ibrāhīm عَنْهُ السَّلَامُ.
- Kila mtu ataona malipo na adhabu ya matendo yake kwa mujibu wa sheria ya haki.

Maoni

^① Katika haya kuna mazingatio kwa wale wanaojiepusha na matendo mema na wakaingia katika madhambi, huku wakitegemea wema wa wazazi wao, sheikh au mtu mwininge.

2:142 **Wapumbavu** mionganini mwa watu watase-ma,^① “Nani amewageuza Waislamu kutoka kibla chao walichokuwa wakikielekeea?” Sema, “Mashariki na Magharibi ni ya Mwenyezi Mungu. Humuongoza yule amtakaye katika njia iliyonyooka.

سَيِّقُولُ السَّفَهَا عَمَّنَ النَّاسُ مَا وَلَهُمْ عَنْ قَبْلَتِهِمْ
الَّتِي كَانُوا عَلَيْهَا طَقْلُ اللَّهِ الْمَشْرِقُ وَالْمَغْرِبُ يَهْدِي
مَنْ يَشَاءُ إِلَى صِرَاطٍ مُسْتَقِيمٍ^(١)

2:143 **Na** vivyo hivyo, tumekufanyeni umma bora ili muwe mashahidi juu ya watu, na Mtume huyu awe ni shahidi juu yenu. **Na** (Ewe Mtume wangu kipenzi) hatukukifanya Kibla ulichokuwa nacho awali, ila tumuone^② yule anayemfuata Mtume na anayerudi nyuma kwa visigino vyake, hayo yalikuwa mazito isipokuwa kwa wale aliowaongoza Mwenyezi Mungu.^③ Na wala haiwi ukuu wa Mwenyezi Mungu, kubatilisha imani yenu; hakika Mwenyezi Mungu ni mpole kwa watu, mwenye kuhurumia.

وَكَذَلِكَ جَعَلْنَاكُمْ أُمَّةً وَسَطَالِتُكُنُوا شَهِيدًا عَلَى
النَّاسِ وَيَكُونُ الرَّسُولُ عَلَيْكُمْ شَهِيدًا وَمَا جَعَلْنَا^(٢)
الْقِبْلَةَ الَّتِي كُنْتَ عَلَيْهَا إِلَّا لِنَعْلَمَ مَنْ يَتَّقِيمُ الرَّسُولَ مِنْ
يَّقِيلُ عَلَى عَقِبَيْهِ وَإِنْ كَانَتْ لَكِبِيرَةً إِلَّا عَلَى الَّذِينَ
هَدَى اللَّهُ وَمَا كَانَ اللَّهُ لِيُضِيعَ إِيمَانَكُمْ إِنَّ اللَّهَ
بِالنَّاسِ لَرَءُوفٌ رَّحِيمٌ^(٣)

2:144 **Tunaona** mara kwa mara ukinyanyua uso wako mbinguni; basi kwa hakika

قَدْ نَرَى تَقْلِبَ وَجْهَكَ فِي السَّمَاءِ حَتَّىٰ لَيَّثَكَ قِبْلَةً

Mada

- Habari ya ghaibu kuhusu ukosoaji wa Wayahudi juu ya kubadilishwa kwa Kibla na majibu yake.
- Umma wa Mtume wetu al-Mustafā^{صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ} kuwa Umma bora na mashahidi kwa watu siku ya hukumu.
- Sababu ya kubadili Kibla ilikuwa kutofautisha kati ya waumini na makafiri
- Amri ya kuifanya Ka'bah kuwa kibla ni kwa mapenzi na furaha ya Mtume wetu kipenzi^{صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ}.

Maoni

^① Aya inaeleza wale waliokuwa wakikosoa juu ya kuifanya Ka'bah tukufu kuwa Kibla (Baada ya Bayt al-Maqdis) ni wapumbavu. Mtu ambaye haelewii hekima ya maamrisho ya kidini na anakosoa isivyo haki ni mpumbavu, hata kama ana utaalamu na uhodari wa mambo katika hii dunia

^② Ingawa maana yake ni “Kujua,” wakati viunga vyake vinapotumika kwa ajili ya Mwenyezi Mungu Mtukufu katika muktadha wa siku zijazo, inamaanisha kwamba Mwenyezi Mungu Mtukufu anamjaribu mtu mbele ya wengine, au anadhihirisha tofauti mbele yao.

^③ Kuhisi kutoridhika ndani ya moyo baada ya kujua amri ya Mwenyezi Mungu Mtukufu ni dalili ya unafiki

tutakuelekeza kwenye Kibla unachokiridhia.^① Basi sasa elekeza uso wako upande wa Msikitii Mtakatifu (Masjid-ul-Haram). Na (enyi Waislamu) popote mlipo elekezeni nyuso zenu upande huo. Hakika, wale waliopewa kitabu, kwa hakika wanajua kuwa haya mabadiliko ni ukweli kutoka kwa Mola wao Mlezi^②- na Mwenyezi Mungu si mwenye kughafilika na matendo yao.

تَرَضِّهَا فَوْلٌ وَجَهَكَ شَطْرَ الْمَسْجِدِ الْحَرَامِ طَ وَ حَيْثُ مَا كُنْتُمْ فَوَلُوا وَ جُهَّلُمْ شَطْرَه طَ وَ إِنَّ الَّذِينَ أُوتُوا الْكِتَبَ لَيَعْلَمُونَ أَكَدُ الْحَقُّ مِنْ سَبِّهِمْ طَ وَ مَا لِلَّهِ بِغَافِلٍ عَمَّا يَعْمَلُونَ ۝

2:145 Hata kama ukiwaleta Watu wa Kitabu ishara zote, hawatofuata Kibla chako, wala wewe hutafuata Kibla chao,^③ wala baadhi yao hawatofuata Kibla cha wengineo. Na (Ewe msikilizaji)^④ kama utafuata matamanio yao, hata baada ya elimu kukufikia, basi hakika hapo utakuwa mionganini mwa wenye kudhulamu.

وَ لَيْلَنِ آتَيْتَ الَّذِينَ أُوتُوا الْكِتَبَ بِكُلِّ أَيَّةٍ مَّا تَبَعُوا قَبْلَتَكَ طَ وَ مَا أَنْتَ بِتَابِعٍ قَبْلَتَهُمْ طَ وَ مَا بَعْصُهُمْ بِتَابِعٍ قَبْلَهُ بَعِضٌ طَ وَ لَيْلَنِ اتَّبَعْتَ أَهْوَاءَهُمْ مِنْ بَعْدِ مَا جَاءَكَ مِنْ الْعِلْمِ لَا إِنَّكَ إِذَا لَمْ يَعْلَمْ ۝

2:146 Wale tulio wapa Kitabu, wanamtambua Mtume kama wanavyowatambua watoto wao. Na kundi mionganini mwao kwa makusudi. wanauficha ukweli.

الَّذِينَ أَتَيْتَهُمُ الْكِتَبَ يَعْرِفُونَهُ كَمَا يَعْرِفُونَ أَبْيَاءَهُمْ طَ وَ إِنَّ فِرِيقًا مِنْهُمْ لَيَكُسُونَ الْحَقَّ وَ هُمْ يَعْلَمُونَ ۝

Mada

- Hali ya kundi Fulani, kuhusu kubadilika kwa Qiblah na mzozo wa ndani wa Watu wa Kitabu unaohusiana na Kibla chao wenyewe.
- Hali ya Watu wa Kitabu kumtambua Mtume Kipenzi صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ Na kundi mionganini mwao linaloficha ukweli kwa makusudi

Maoni

- ① Mwenyezi Mungu anapenda kile anachokipendelea Mtume wake Kipenzi صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ na humtimizia lile analoliridhia.
- ② Watu wa Kitabu walijua kuwa mabadiliko ya Kibla yametoka kwa Mwenyezi Mungu Mtukufu kama vile maelezo haya yalivyoolezwa katika maandiko yao na kubainishiwa na Mitume yao.
- ③ Watu wa Kitabu, pamoja na ushahidi, hawakuamini Kibla cha Waislamu kwa sababu ya wivu, kwani Utume ulikuwa umeacha nasaba ya Wana wa Israel. Wivu ni uovu mbaya sana kwa sababu unamzuia mtu kuukubali ukweli.
- ④ Haya maelekezo si kwa ajili ya Mtume wetu Kipenzi صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ bali kila msomaji au msikilizaji wa hii aya. Au dhahiri imeelekezwa kwa Mtume صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ lakini inawahu su Waislamu kwa sababu ya Mtume صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ hawezi kufuata matamanio ya Watu wa Kitabu.

2:147 (Ewe Msikilizaji)^① Ukweli ni ule unaotoka kwa Mola wako Mlezi, basi usiwe mionganini mwa wenye shaka

الْحَقُّ مِنْ رَبِّكَ فَلَا تَكُونَنَّ مِنَ الْمُسْتَرِينَ ﴿١٤٧﴾

١٤٧

2:148 Na kila mmoja anao upande anaoelekea, basi shindaneni katika matendo mema.^② Mwenyezi Mungu atawakusanya wote popote mlipo. Hakika Mwenyezi Mungu ni muweza juu ya kila kitu.

وَ لِكُلِّ وِجْهَةٍ هُوَ مُوْلَيْهَا فَاسْتَقْوْدُ الْخَيْرَاتِ طَآئِنَّ مَا تَكُونُوا يَأْتِ بِكُمْ أَللَّهُ جَيْعَانٌ إِنَّ اللَّهَ عَلَى كُلِّ شَيْءٍ عَلِيمٌ

قدير

2:149 (Ewe Mtume wangu Kipenzi) popote unapotoka elekeza uso wako kwenye Msikiti Mtukufu, hakika huu ndiyo ukweli kutoka kwa Mola wako Mlezi Na Mwenyezi Mungu si mwenye kughafilika na vitendo vyenu.

وَ مِنْ حَيْثُ خَرَجْتَ فَوَلِّ وَ جَهَكَ شَطْرَ الْمُسْجِدِ الْحَرَامِ طَ وَ إِنَّهُ لِلْحَقِّ مِنْ رَبِّكَ طَ وَ مَا اللَّهُ بِغَافِلٍ عَمَّا تَعْمَلُونَ ﴿١٤٩﴾

2:150 (Mtume Kipenzi) popote unapotoka elekeza uso wako kwenye Msikiti Mtukufu. Na (Enyi Waislamu) popete mlipo elekezeni nyuso zenu huko, ili watu (Wayahudi) wasiwe na hoja dhidi yenu, isipokuwa wale wasiotenda haki mionganini mwao; Basi msiwaogope wao,

وَ مِنْ حَيْثُ خَرَجْتَ فَوَلِّ وَ جَهَكَ شَطْرَ الْمُسْجِدِ الْحَرَامِ طَ وَ حَيْثُ مَا كُنْتُمْ قَوْلُوا وَ جُوهَلُمْ شَطْرَهُ لِيَلَّا يَكُونَ لِلشَّاَسِ عَلَيْكُمْ حُجَّةٌ إِلَّا الَّذِينَ ظَلَمُوا مِنْهُمْ فَلَا تَحْشُوْهُمْ

Mada

- Katazo la kutilia shaka mabadiliko ya Qiblah na Amri nyinginezo za Mwenyezi Mungu.
- Sababu nyingine ya mabadiliko hayo ni kwamba, Qiblah kimeteuliwa kwa kila Umma; amri ya kushindana katika matendo mema.
- Kukabili uelekeo wa Ka'bah ni wa kila sehemu iwe safarini au laa.

Maoni

^① Haya maelekezo pia hayakulengwa kwa Mtume Kipenzi bali kwa kila mtu anayekutana na aya hii; au inaonekana imeelekezwa kwa Mtume lakini inawahu pia Waislamu kama ilivyo kwa Mtume kamwe hatotilia shaka amri ya Mwenyezi Mungu Mtukufu.

^② Hapa inaelezwa watu wasishindane wao kwa wao katika mambo ya mali, vyeo, umaarufu na kukubalika kwenye jamii, kwani hayo ni mambo ya kupita tu, wakati uchamungu, ibada na uadilifu ndiyo vitu vya kudumu na yanayostahiki juhudini zetu.

niogopeni Mimi,^① Ili niwatinizieni neema yangu na ili mpate kuongoka.

وَاحْشُوْنِي وَلَا تَمْعَنِي عَلَيْكُمْ وَلَعَلَّكُمْ تَهْتَدُونَ^{٥٦}

2:151 Kama tulivyomtuma kwenu, Mtume kutoka mionganini mwenu, anawasomea aya zetu, na anawatakasa, na anawafundisha Kitabu na hekima, na anawafundisha mliyokuwa hamyajui.^②

كَمَا أَرَسَلْنَا فِيْكُمْ رَسُولًا مِنْكُمْ يَتْلُو عَلَيْكُمْ آيَاتِنَا وَيُرِيكُمْ وَيُعَلِّمُكُمُ الْكِتَابَ وَالْحِكْمَةَ وَيُعَلِّمُكُمْ مَا لَمْ تَكُونُوا تَعْلَمُوْنَ^{٥٧}

2:152 Basi nikumbukeni, nami nitawakumbuka, na mnishukuru na wala msinikufuru.^③

فَادْكُرُوهُنِيْ أَذْكُرْكُمْ وَأَشْكُرْهُوْلِيْ وَلَا تَكُفُرُوهُنِيْ^{٥٨}

2:153 Enyi mliaoamini! Takeni msaada kwa subira na Sala^④. Hakika Mwenyezi Mungu yuko pamoja na wanaosubiri.

يَا أَيُّهَا الَّذِينَ آمَنُوا اسْتَعِيْبُوهُ إِلَيْهِمْ الصَّلَاةُ إِنَّ اللَّهَ مَعَ الصَّابِرِيْنَ^{٥٩}

2:154 Wala msiseme waliouwawa katika njia ya Mwenyezi Mungu, wamekufa. Bali wao wako

وَلَا تَقْرُبُوا إِلَيْنِيْ بِمَنْ يُقْتَلُ فِي سَبِيلِ اللَّهِ أَمْوَاتٌ بَلْ

Mada

- Kusudi la ujio wa Mtume uliobarikiwa
- Amri ya kumkumbuka Mwenyezi Mungu Mtukufu, kushukuru neema zake, na kujiepusha na kutokushukuru
- Amri ya kutafuta msaada kwa subira na Sala; ubora wa watu wenye subira.
- Sifa ya aliyekufa shahidi, ni kuwa hai, na kusema kuwa amekufa hairuhusiwi.

Maoni

^① Hofu ya Mwenyezi Mungu Mtukufu inatakiwa kuwa juu ya kila hofu na kutafuta radhi zake kutangulie juu ya furaha ya viumbe.

^② Kwa hakika, Mtume Kipenzi صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ hakufundisha tu mada za Qur'an tukufu na maagizo ya Mwenyezi Mungu bali anafundisha muongozo, mafanikio, hekima na elimu nyinginezo, kwani ye ye Mtume صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ ana ujuzi wote wa wale walotangulia kabla yake na walio baada yake.

^③ Neno, kufr hapa linamaanisha "kutokuwa na shukrani" Kwa sababu linatokea pamoja na "shukrani" (shukr). Ingawa inamaanisha "kutokuamini" pale linapotumika kupinga Uislamu au Imani.

^④ Kutafuta msaada kwa chanzo kisichokuwa Mwenyezi Mungu Mtukufu, siyo ushirikina (Kwa sababu chanzo kinazingatiwa kuwa ni njia tu na si msaidizi wa asili au kitu cha kuabudiwa).

hai ila nyinyi hamutambui.^①

أَحْيَا عَوْلَكِنْ لَا تَشْعُرُونَ^②

2:155 **Hakika** tutawajaribu kwa khofu na njaa; na upungufu wa mali, watu na matunda. Na wape bishara njema wale wanaosubiri.

وَلَنَبْلُونَكُم بِشَيْءٍ مِّنَ الْحَوْفِ وَالْجُوعِ وَنَقْصٍ مِّنَ الْمُوَالِ وَالْأَنْفُسِ وَالثَّمَرَاتِ طَوَّبَ اللَّهُ الصَّابِرِينَ^③

2:156 Wale ambaa ukiwasibu msiba husema, “Sisi ni wa Mwenyezi Mungu na hakika kwake tutarejea”

الَّذِينَ إِذَا آتَاهُمْ مُصِيرَةً قَالُوا إِنَّا لِلَّهِ وَإِنَّا إِلَيْهِ سَاجِدُونَ^④

2:157 Hawa ndio watu walio na baraka kutoka kwa Mola wao Mlezi na rehema zake. Na hawa ndio watu walioongoka.

أُولَئِكَ عَلَيْهِمْ صَلَوَاتٌ مِّنْ رَّبِّهِمْ وَرَاحِمَةٌ وَأُولَئِكَ هُمُ الْمُهَمَّدُونَ^⑤

2:158 **Hakika**, Safā na Marwah ni katika alama za Mwenyezi Mungu,^⑥ kwa hiyo yeyote anayefanya Hijja au Umrah, kwenye hii Nyumba Tukufu, basi hakuna dhambi kwake kutembea baina yao. Na yeyote yule atakayetenda mema kwa hiyari yake, basi Mwenyezi Mungu ni Mlipaji na Mjuzi wa Yote.

إِنَّ الصَّفَافَ الْبَرُّ وَمَنْ شَاءَ إِرْلَهُ فَمَنْ حَجَّ الْبَيْتَ أَوْ اعْتَرَفَ لِجَنَاحِهِ أَنْ يَطَّوَّفَ بِهِمَا وَمَنْ تَطَوَّعَ خَيْرًا فَإِنَّ اللَّهَ شَاكِرٌ عَلَيْهِمْ^⑦

2:159 **Hakika** wale wanaoficha Aya zilizo wazi

إِنَّ الَّذِينَ يُكْفِرُونَ مَا أَنْزَلْنَا مِنَ الْبَيْتِ وَالْهُدَىٰ وَمَنْ^⑧

Mada

- Mtu hujaribiwa kwa mitihani na kuna habari njema kwa mwenye subira.
- Ubora wa vilima vya Ṣafā na Marwah na kuondoa wasiwasi waliokuwa nao Waislamu.
- Onyo la laana kwa wanaoficha ukweli na ahadi ya msamaha kwa wanaotubu

Maoni

^① Waliokufa shahidi, bila ya shaka wako hai, ingawa hatuwezi kutambua kiwango kamili cha maisha yao. Kwa sababu hii, wanafanyiwa taratibu za kawaida na maagizo ya watu waliokufa.

^② Ṣafā na Marwah ilipata ukuu kutokana na kunasibishwa na Sayyidatunā Hājirah. Kihistoria, ni vilima viwili (haviko mbali na eneo la Ka'bah) ambapo katikati yake Bi Hājirah alitafuta maji. Leo hii, Waislamu wanaiga mapambano yake kama ibada ya Hijja na Umrah. Maeneo na vitu vinavyofungamana na watu wema huwa vitukufu katika dini, hii ni moja ya mifano mingi.

na uwongofu^① tulio wateremshia, ingawa tumeweka bayana kwa watu katika Kitabu; hao anawalaani Mwenyezi Mungu na wanawalaani wenyе kulaani.

بَعْدِ مَا بَيَّنَهُ لِلنَّاسِ فِي الْكِتَابِ إِلَيْكَ يَأْتُهُمُ اللَّهُ وَ
يَأْتُهُمُ الْعَذَابُ ﴿١٩﴾

2:160 Isipokuwa wale waliotubu na wakaten-geneza na wakadhihirisha (yaliyofichikana), basi hao nitawakubalia toba yao; na Mimi ni mwingi wa kupokea toba, Mwenye kurehemu.

إِلَّا الَّذِينَ تَابُوا وَاصْلَحُوا وَبَيَّنُوا فَأُولَئِكَ أَتُوبُ
عَلَيْهِمْ وَأَنَا التَّوَابُ الرَّحِيمُ ﴿٢٠﴾

2:161 **Hakika** waliokufuru na wakafa hali ya kuwa ni makafiri,^② hao iko juu yao laana ya Mwenyezi Mungu na Malaika, na ya watu wote^③.

إِنَّ الَّذِينَ كَفَرُوا وَمَا تُوَلُّهُمْ كُفَّارٌ أُولَئِكَ عَلَيْهِمْ
لَعْنَةُ اللَّهِ وَالْمَلِكَةِ وَالنَّاسِ أَجَمِيعُهُنَّ ﴿٢١﴾

2:162 Watacaa humo milele, adhabu yao haitapunguzwa, na wala hawatapewa muda wa kupumzika.

خَلِدِيهِنَّ فِيهَا لَا يُخَفَّ عَنْهُمُ الْعَذَابُ وَلَا هُمْ
يُنَظَّرُونَ ﴿٢٢﴾

2:163 **Na Mungu** wenu ni Mungu mmoja, hakuna Mungu mwingine ila yeye, Mwingi wa Rehema, Mwenye Kurehemu.

١٩
٣

Mada

- Onyo kwa waliokufa katika hali ya ukafiri
- Mwenyezi Mungu Mtukufu pekee ndiye anayestahiki kuabudiwa

Maoni

^① Kuficha mafundisho ya dini ni dhambi, iwe kwa kuyaficha pale yanapohitajika, au kuwaelekeza watu kimakosa. Kwa kweli, kufundisha mafundisho yasiyo sahihi huleta matokeo mabaya zaidi. Siku hizi, inaonekana kuna uhuni wa watu kutoa maoni kimakosa juu ya mambo ya Qur'an na Sunna; onyo katika Aya inawahu su watu wote wa aina hiyo.

^② Kuffār (Neno la Qur'an) ni wingi wa Kāfir (Makafiri).

^③ Kunyimwa hazina ya Imani wakati wa kifo ni hali mbaya zaidi, wakati kufa na imani ni mafanikio makubwa zaidi. Kwa hiyo kila Muislamu anapaswa kuogopa kifo kibaya licha ya kuwa na matendo mema, ibada na uchamungu.

2:164 **Hakika**, kuumbwa kwa mbingu na ardhi; ubadilishaji wa mchana na usiku, marikebu zipitazo baharini zikiwa zimebeba yale yanayowanufaisha watu; mvua anayoiteremsha Mwenyezi Mungu kutoka mbinguni, akaihuisha nayo ardhi baada ya kufa kwake; na akaeneza humo kila aina ya wanyama, na mabadiliko ya upopo na mawingu yanayo amrishwa kupita baina ya mbingu na ardhi^①- kwenye haya yote, bila shaka zipo ishara kwa wenye akili.^②

إِنَّ فِي خَلْقِ السَّمَاوَاتِ وَالْأَرْضِ وَاحْتِلَافِ الَّيْلِ وَالنَّهَارِ
وَالْفُلْكِ الَّتِي تَجْرِي فِي الْبَحْرِ بِمَا يُنَفِّعُ النَّاسَ وَمَا
أَنْزَلَ اللَّهُ مِنَ السَّمَاءِ مِنْ مَاءٍ فَأَحْيَا بِهِ الْأَرْضَ بَعْدَ
مَوْتِهَا وَبَثَّ فِيهَا مِنْ كُلِّ دَآبَةٍ وَتَصْرِيفِ الرِّيحِ وَ
السَّحَابِ الْمُسَخِّرِ بَيْنَ السَّمَاءِ وَالْأَرْضِ لَا يَلِيهِ لِقَوْمٌ
يَعْقِلُونَ^{١٦٤}

2:165 Na mionganini mwa watu wapo wanaofanya washirika katika ibada wasio kuwa Mwenyezi Mungu; **wanawapenda** kama wanavyompenda Mwenyezi Mungu; **lakini** kwa wale wanaoamini, wanampenda zaidi Mwenyezi Mungu. Na laiti madhalimu wangeiona hali, ambapo watashuhudia adhabu, kwani uweza ni wa Mwenyezi Mungu pekee, na Mwenyezi Mungu anaadhibu vikali.

وَمِنَ النَّاسِ مَنْ يَتَّخِذُ مِنْ دُونِ اللَّهِ أَنْدَادًا يُجْنِّبُنَاهُمْ
كَحْبِ اللَّهِ طَ وَالَّذِينَ آمَنُوا أَشَدُ حُبَّالِهِ طَ وَلَوْيَرَى
الَّذِينَ ظَلَمُوا إِذْ يَرُونَ الْعَذَابَ لَا نَقُوَّةَ لِلَّهِ جَيْعاً وَ
أَنَّ اللَّهَ شَرِيدُ الْعَذَابِ^{١٦٥}

2:166 **Walioufatuwa** watakapowakataa wale walioufauata, na wataona adhabu; na mafungamano yao yote yatakatika.^③

إِذْ تَبَرَّأَ الَّذِينَ أَتَيْعُوا مِنَ الَّذِينَ أَتَبَعُوا وَرَأَوْا الْعَذَابَ
وَتَقْطَعَتْ بِهِمُ الْأُسْبَابُ^{١٦٦}

Mada

- Dalili za Uweza na Rehema za Mwenyezi Mungu Mtukufu; amri ya kutafakari juu ishara hizi.
- Mapenzi ya washirikina kwa Miungu ya uongo
- Mapenzi ya waumini kwa Mwenyezi Mungu Mtukufu.
- Ni onyo kwa washirikina.
- Kukata tamaa na viongozi wa washirikina na kutoshirikiana kwao siku ya Kiyama

Maoni

- ^① Kutafakari kila jambo lililotajwa katika aya humfanya mtu azidiwe na maajabu ya nguvu za Mwenyezi Mungu.
- ^② Sayansi ni njia ya kupata utambuzi Fulani juu ya ukoo wa nguvu za Mwenyezi Mungu; utambuzi huu utaongezeka kwa kiwango cha kuongezeka utaalamu. Kama mtu atasoma sayansi kwa nia ya kuutumikia Uislamu na kufikia kiwango cha juu cha utambuzi wa Mwenyezi Mungu Mtukufu, basi hili lingekuwa ni tendo kubwa la ibada; hii ingethibitisha utiifu wa amri ya kutafakari juu ya uumbaji.
- ^③ Siku ya Hisabu, mafungamano ya makafiri yatakatika, wakati mafungamano baina ya watu wema na walioamini yatabaki imara.

٢٠
ع

2:167 Na wale waliowafuata wasasema, “Laiti tungeweza kurudi tukawakataa kama wao walivyotukataa sisi.^①” Hivyo Mwenyezi Mungu atawaonyesha vitendo vyao kuwa majuto yao wala hawatakuwa wenye kutoka motoni.

وَقَالَ الَّذِينَ اتَّبَعُوا وَأَنَّ لَنَا كُرْبَةً فَتَبَرَّأُ مِنْهُمْ كَمَا تَبَرَّعُوا مِنْنَا طَكْنَدْلِكْ يُرِيْهُمُ اللَّهُ أَعْمَالَهُمْ حَسَرَاتٍ عَلَيْهِمْ وَمَا هُمْ بِخَرِّجِينَ مِنَ النَّارِ^②

2:168 Enyi watu, kuleni vilivyomo katika ardhi, halali^② na safi,^③ na wala msifuate hatua za shetani. Hakika huyo ni adui wenu wa wazi kabisa.

يَا أَيُّهَا النَّاسُ كُلُّهُمْ مَا فِي الْأَرْضِ حَلَالًا كُلِّهِ لَا تَنْهَا وَلَا تَتَبَرَّعُوا خُطُواتِ الشَّيْطَنِ طَإِنَّهُ لَكُمْ عَدُوٌّ مُّبِينٌ^④

2:169 Yeye atawaamrisheni tu kufanya maovu na machafu, na mumsingizie Mwenyezi Mungu mambo msiyoyajua.

إِنَّمَا يَأْمُرُكُمْ بِالسُّرُورِ وَالْفُحْشَاءِ وَأَنْ تَقُولُوا عَلَى اللَّهِ مَا لَا تَعْلَمُونَ^⑤

2:170 Wanapoambiwa, “Fuateni aliyoyater-emsha Mwenyezi Mungu” husema, “sisi tutafuata tulio wakuta nayo baba zetu” Je hata ikiwa baba zao walikuwa hawaelewi kitu

وَإِذَا قِيلَ لَهُمْ أَتَتَّبَعُوا مَا أَنْزَلَ اللَّهُ قَالُوا بَلْ نَتَبَعُ مَا أَنْهَيْنَا عَلَيْهِ أَبَأْءَنَا أَوْ كَانَ أَبَأْ وَهُمْ لَا يَعْقِلُونَ شَيْئًا^⑥

Mada

- Amri ya kula halali na safi; na uharamu wa kufuata njia za shetani.
- Kazi ya shetani ni kuamrisha maovu, kukosa haya, na kumsingizia uongo Mwenyezi Mungu Mtukufu
- Washirikina wakiwafuata mababu zao kwa upofu, (bila kutafakari) na hukumu yake

Maoni

^① Kumbuka, majuto ya kweli juu Imani na matendo mema yatamgusa kafiri, lakini waumini pia watajutia upungufu wa matendo mema na matendo yoyote ya dhambi.

^② Katika Uislamu ulaji wa halali na kujiepusha na haramu kunasisitizwa sana; mtu hawezi kuwa mchamungu kwa kupata kipato cha haramu na kukitumia. Rushwa, riba, wizi, uporaji n.k ni mifano ya kipato cha haramu.

^③ “Halal na Tayyib” maana yake ni halali kuliwa (kama nyama ya mbuzi, mboga mboga, dengu n.k.) na vimepatikana katika njia inayoruhusiwa (si kwa rushwa au wizi).

wala hawakuongoka? ①

وَلَا يَهْتَدُونَ ②

2:171 Na mfano wa walio kufuru ni kama mfano wa yule ambaye anampigia kelele asiyeh sikia ila wito na sauti tu. (Hawa makafiri) ni viziwi, mabubu, na vipofu, kwa hiyo hawaelew. ②

وَمَثْلُ الَّذِينَ كَفَرُوا كَمْثِلِ الَّذِينَ يَعْنِي بِسَالَيْسَمْعُ اَلَّا

دُعَاءً عَوَّنَدَ آَغَ طُصْبَكُمْ عَنِ فَهُمْ لَا يَعْقِلُونَ ④

2:172 Enyi mliaoamini, kuleni katika vitu vizuri tulivyo waruzuku, na mumshukuru Mwenyezi Mungu; kama yeye pekee ndiye mnayemuabudu.

يَا أَيُّهَا الَّذِينَ آمَنُوا إِذْ أَكْتُوْمَنْ طَبِيتَ مَا رَأَيْتُمْ قَاتِلُمْ وَأَشْكُرُوا

لِلَّهِ أَنْ كُنْتُمْ إِيَّاهُ تَعْبُدُونَ ⑤

2:173 Yeye amewaharamishieni tu mzoga na damu, na nguruwe na mnyama ambae alitajiwa katika kuchinjwa kwake jina la asiyekwa Mwenyezi Mungu, ③ kwa hiyo kwa yeyote aliylazimika si kwa kutaka mwenyewe wala kuzidisha kiwango cha ulazima, hakuna dhambi juu yake; hakika Mwenyezi Mungu ni Mwingi wa Kusamehe, na Mwingi wa Rehema.

إِنَّمَا حَرَّمَ عَلَيْكُمُ الْبَيْتَةَ وَالدَّمَ وَلَحْمَ الْخِنْزِيرِ وَمَا

أَهْلَ بِهِ لِغَيْرِ اللَّهِ ۝ فَنِنْ اصْطَرَّ غَيْرَ بَاغِرٍ وَلَا عَادِ فَلَا إِشْ

عَلَيْهِ ۝ إِنَّ اللَّهَ عَفُوٌ رَّحِيمٌ ⑥

Mada

- Mfano wa jinsi makafiri wasivyokubali ukweli
- Amri ya kula vyakula vilivyo halali na kumshukuru Mwenyezi Mungu Mtukufu.
- Vyakula vilivyo haramu na ruhusa ya kutumia wakati wa dharura inayokubalika kisheria.

Maoni

① Kuwafuata wazee wakienda kinyume na sheria ni haramu. Pia kuwafuata wazee katika matendo ya dhambi, hairuhusiwi. Kwa mujibu wa hadithi moja, "hakuna ruhusa ya kumtii kiumbe katika kumuasi Mola Muumba" Baadhi hutumia kisingizio cha desturi ya wazee au mila za kikabilan wanapofuata matendo kinyume na Uislamu kwenye vifo, ndoa, urithi na mambo mengine; visingizio vya aina hiyo si sahihi na havikubaliki.

② Macho, masikio, ulimi, ni nyenzo za kuona, kusikia, na kuongea haki, na hiyo ndio faida yake halisi. Kwa kuwa makafiri hawanufaiki na faida ya hivi viungo, wanaelezewa kama viziwi, mabubu na vipofu.

③ Kumontaja yeyote asiyekwa Mwenyezi Mungu Mtukufu, wakati wa kitendo cha kuchinja, kutamfanya mnyama kuwa kibudu na haramu kuliwa. Aya hii haihusu kumnasibisha mnyama na mtu mwininge wakati wa uhai wake.

2:174 **Hakika**, wale wanaoficha yale Mwenyezi Mungu aliyyateremsha kwenye Kitabu,^① na badala yake wanachukuwa thamani ndogo, hao hawali matumboni mwao ila moto, wala Mwenyezi Mungu hatosema^② nao siku ya Kiyama wala hatawatakasa; na kuna adhabu chungu kwa ajili yao.

إِنَّ الَّذِينَ يُكْتُمُونَ مَا أَنْزَلَ اللَّهُ مِنَ الْكِتَابِ وَ
يَعْسِرُونَ بِهِ شَمَانًا قَلِيلًا لَا وَلِلَّهِ مَا يَأْكُلُونَ فِي بُطُونِهِمْ إِلَّا
النَّارُ وَلَا يَكِلُّهُمُ اللَّهُ يَوْمُ الْقِيَمَةِ وَلَا يُرَدُّ كُيُومُهُمْ وَلَهُمْ
عَذَابٌ أَلِيمٌ^③

2:175 Hao ndio walionunua upotofu badala ya uwongofu, na adhabu badala ya kusamehewa; hivi ni kwa kiasi gani wanaweza kuuvumilia moto?^④

أُولَئِكَ الَّذِينَ اشْتَرُوا الصَّلَةَ بِأَهْلِهِ وَالْعَذَابَ
بِالْمُغْفِرَةِ فَمَا أَصْبَرُوهُمْ عَلَى النَّارِ^⑤

2:176 Hii (adhabu) ni kwa sababu Mwenyezi Mungu ameteremsha Kitabu kwa haki. Na kwa hakika, wale waliohitilafiana katika Kitabu^④ wamo katika upinzani ulio mbali.

ذَلِكَ بِأَنَّ اللَّهَ نَزَّلَ الْكِتَابَ بِالْحَقِّ وَإِنَّ الَّذِينَ اخْتَلَفُوا
فِي الْكِتَابِ لَفِي شَقَاقٍ بَعِيْدٍ^⑥

2:177 **Uwema** hauko kwenye kuelekeza nyuso zenu Mashariki au Magharibi. Bali uwema wa kweli ni kwa wale wanaomuamini Mwenyezi Mungu na Siku ya Hukumu na malaika na Kitabu na Mitume, Na anawapa mali kwa

لَيْسَ الْبِرَّ أَنْ تُؤْتُوا وَجْهَكُمْ قَبْلَ الشُّرِقِ وَالْمَغْرِبِ
وَلِكِنَّ الْبِرَّ مَنْ أَمْنَى بِاللَّهِ وَالْيَوْمِ الْآخِرِ وَالْمَلِكَةَ وَ
الْكِتَابَ وَالْتَّبِيْنَ وَأَقَى الْمَالَ عَلَى حِجَّهِ ذَوِي الْقُرْبَى

Mada

- Adhabu kali za kuuza dini na sababu zake.
- Maelezo yanayohusiana na matendo mema; kukubali imani na kuwasaidia ndugu na yatima, kusimamisha swala, kutoa zaka n.k.

Maoni

^① Kuficha, kunahusisha kutowataarifu wengine juu ya yaliyoandikwa kwenye Kitabu, kutowasomea wengine, kutowaonyesha wengine, na pia kujaribu kuficha maana ya kweli kwa kutoa maelezo ya uongo.

^② Hii ina maanisha Mwenyezi Mungu hatoongea nao kwa huruma.

^③ “Mā” (ما) hapa inaweza kuelezewa kama hisia ya mshangao au inaweza kuelezea hali ya kuuliza swali.

^④ Hapa “Kitabu” ina maanisha, Qur'an au Torati; kwenye sehemu ya kwanza “kuhitalifiana” imemaanisha kutokbali, na kwenye sehemu ya pili, kutokukubali ipasavyo, kama ambavyo Wayahudi wasivyoikubali kabisa Qur'an, na wanadai kuikubali Torati, lakini pia hawakuikubali yote (ipasavyo).

mapenzi ya Mwenyezi Mungu jamaa na mayatima na maskini na wasafiri^①, na waombao na katika kuwaachia huru watumwa; na akasimamisha swala, na akatoa Zaka, na wanaotimiza ahadi yao wanapoahidi; na wale wenyе subira wakati wa majanga, shida na wakati wa Jihadi. Hao ndiyo wakweli.^② Na hao ndiyo wachamungu.

وَالْيَتَمِ وَالسَّكِينَ وَابْنَ السَّبِيلِ لَا وَالسَّائِلِينَ وَفِي
الرِّقَابِ وَأَقَامَ الصَّلَاةَ وَأَتَى الرَّكُوْةَ وَالْمُؤْمِنُ بِعِهْدِهِمْ
إِذَا عَاهَدُوا وَالصَّابِرِينَ فِي الْبَاسَاءِ وَالصَّرَاءِ وَجِينَ
الْبَاسِ طَوْلِيْكَ الَّذِينَ صَدَقُوا وَأُولَئِكَ هُمُ الْمُتَّقِنُونَ^④

2:178 Enyi mlionamini! Kulipiza kisasi kume-faradhishwa juu yenu katika waliouwawa.^③ Mtu huru kwa mtu huru, na mtumwa kwa mtumwa, na mwanamke kwa mwanamke. Basi yejote yule anayesamehewa na ndugu yake chochote basi afuatiliwe kwa wema, na yeye alipe kwa uzuri.^④ Hii ni kufanyiwa uwepesi kutoka kwa Mola wenu Mlezi na ni rehema. Basi yejote atakaevuka mipaka baada yake, atapata adhabu chungu.

يَا أَيُّهَا الَّذِينَ آمَنُوا كُتِبَ عَلَيْكُمُ الْقِصَاصُ فِي
الْقُتْلَى طَالْحُرْ بِالْحُرْ وَالْعَبْدُ بِالْعَبْدِ وَالْأُنْثُي
بِالْأُنْثِي طَفْلُنْ عَفِيَ لَهُ مِنْ أَخْيَهُ شَيْءٌ قَاتِلًا عَمَّا يُعْرُوفُ
وَأَدَاءُ إِلَيْهِ بِإِحْسَانٍ طَلِكَ تَحْفِيفُ مِنْ رَبِّكُمْ وَ
رَحْمَةً طَفْلُنْ اعْتَدَى بَعْدَ ذَلِكَ قَلَهُ عَذَابُ أَلِيمٍ^⑤

2:179 Na katika kulipiza kisasi kuna uhai kwa ajili yenu enyi wenyе akili Ili

وَلَكُمْ فِي الْقِصَاصِ حَيْوَةٌ يُؤْلِي إِلَى لُبَابٍ لَعْلَكُمْ

Mada

- Wajibu wa kulipiza kisasi na baadhi ya sheria za diyah.
- Faida kubwa ya kuamrisha kulipiza kisasi.

Maoni

- ① Ibn al-Sabil (Mwana wa njia) ni maneno ya kiarabu yenyе maana ya msafiri.
- ② Wale wanaoshikilia Imani sahihi, wakaswali na wakatoa sadaka na zaka na wakaishika subira, wakatimiza ahadi na wakatenda mema, ni wa kweli katika madai yao ya Imani. Mwenyezi Mungu Mtukufu atujaalie tuwe mionganini mwao.
- ③ “Qatlā” (neno la Qur'an) ni wingi wa neno “Qatīl” ambalo linamaanisha mtu aliyeuwawa.
- ④ Warithi wa mtu aliyeuwawa ikiwa wameridhika na fidia yao, basi wafuatilie kwa njia nzuri, na muuaji anapaswa kulipia fidia hiyo kwa njia ya amani.

msalimike.^①تَتَقْوَنَ^(٤٤)

2:180 Imefaradhishwa kwenu^②, kuwa umauti unapomfika yeote kati yenu, kama akiacha mali atoe wasia kwa wazazi wake na jamaa zake kwa uadilifu; hii ni wajibu juu ya wachamungu.

كُتِبَ عَلَيْكُمْ إِذَا حَضَرَ أَحَدُكُمُ الْمُوْتَ إِنْ تَرَكَ حَمِيرًا
الْوَصِيَّةُ لِلَّوَالِدَيْنِ وَالْأَقْرَبِينَ بِالْمَعْرُوفِ حَقَّا عَلَى
الْمُسْتَقِينَ^(٤٥)

2:181 Na atakaeubadilisha wasia baada ya kuusikia, basi dhambi yake ni juu ya wale ambao wameubadilisha.^③ Hakika Mwenyezi Mungu ni Mwenye Kusikia, Mjuzi.

فَمَنْ بَدَّلَهُ بَعْدَ مَا سَمِعَهُ فَإِنَّمَا إِثْمُهُ عَلَى الَّذِينَ
يُبَدِّلُونَهُ إِنَّ اللَّهَ سَيِّعُ عَلِيهِمْ^(٤٦)

2:182 Mwenye kuogopa upendeleo au dhambi kwa yule anayefanya wasia na akasuluhisha baina yao, basi hana dhambi juu yake.^④ Hakika Mwenyezi Mungu ni Mwingi wa kusamehe, Mwingi wa Kurehemu.

فَمَنْ خَافَ مِنْ مُّوْصِصَ جَنَّفَا وَإِنَّمَا أَصْلَحَ بَيْهُمْ فَلَا إِثْمُ
عَلَيْهِ إِنَّ اللَّهَ غَفُورٌ رَّحِيمٌ^(٤٧)

2:183 Enyi mliaoamini! Imefaradhishwa kwenu

يَا أَيُّهَا الَّذِينَ آمَنُوا كُتِبَ عَلَيْكُمُ الصِّيَامُ كَمَا كُتِبَ

٤٤

Mada

- Amri ya kutoa wasia na baadhi ya sheria zinazohusiana nazo.
- Wajibu wa kufunga; Msamaha kwa wagonjwa na wasafiri.

Maoni

^① Katika "kisasi" "kuna uhai" kwa sababu ni kizuizi cha mauaji, kwani wahalifu wanajua kuwa uhai wao unaweza kutolewa kama malipo. Ikiwa adhabu ya kifo itatolewa, watu watazingatia, na hii itakuwa njia ya kulinda maisha ya watu.

^② Wajibu huu ulikuwepo kabla ya kuteremshwa hukumu ya mirathi. Kwasababu wakati huo mali ilikuwa ikigawanywa kwa njia ya wasia tu. Hukumu ya mirathi ilipoteremshwa Wajibu wa kutoa wasia ulifutwa; ingawa, bado inaruhusiwa.

^③ Baada ya kutoa wasia, mtu ana haki ya kuubadilisha wakati wa uhai wake, lakini baada ya kifo chake, wasia (wa marehemu) hauwezi kubadilishwa na mtu mwagine.

^④ Endapo mwanachuoni, mtawala, mrithi au ndugu atagundua kuwa mtu anayekufa amemdhumu mtu kwa wasia wake, au si mwenye kufuata sheria za kiislamu na akamshawishi kubadili wasia, basi hatopata dhambi bali atastahili thawabu.

kufunga,^① kama ilivyofaradhishwa kwa wale waliotangulia kabla yenu, ili mpate kuwa wachamungu.

2:184 Siku maalumu za kuhesabika. Basi miongoni mwenu atakayekuwa mgonjwa au yuko safarini anaweza kulipa idadi ya hizo swaumu^② siku nyingine. Na kwa wale wasiweza kufunga watoe fidia kwa kumlisha masikini. Basi anayefanya wema zaidi kwa hiyari yake, basi hiyo ni bora kwake. Na kufunga ni bora kwenu, ikiwa mnatambua.

2:185 *Mwezi* wa Ramadhani,^③ ndiyo mwezi ulioteremshwa Qur'an; uongofu kwa watu na hoja zilizo wazi za uwongofu na upambanuzi; Basi yejote mionganoni mwenu, atakayeufikia mwezi huu, basi atimize swaumu yake. Na aliye mgonjwa au safarini. Basi atimize idadi hiyo ya swaumu katika siku nyingine. Mwenyezi Mungu anakutakieni yaliyo mepesi, wala hakutakieni ugumu, ili muweze kutimiza idadi ya swaumu, na mumtukuze Mwenyezi Mungu kwa kuwa

عَلَى الَّذِينَ مِنْ قَبْلِكُمْ لَعَلَّكُمْ تَتَّقُونَ ﴿٨﴾

أَيَّامَ مَعْدُودَاتٍ فَمَنْ كَانَ مِنْكُمْ مَرِيضًا أَوْ عَلَى سَفَرٍ
فَعِدَّهُ مِنْ أَيَّامٍ أُخْرَى وَعَلَى الَّذِينَ يُطِيقُونَهُ فِدْيَةٌ
طَاعَامٌ مُسْكِنٌ فَمَنْ تَطَوَّعَ خَيْرًا فَهُوَ حَمْيَلٌ وَأَنْ
تَصُومُوا حَمْيَلًا كُمْ إِنْ كُنْتُمْ تَعْلَمُونَ ﴿٩﴾

شَهْرٌ رَمَضَانَ الَّذِي أُنْزِلَ فِيهِ الْقُرْآنُ هُدًى لِلنَّاسِ وَ
بِئْسَتِهِ مِنَ الْهُدُى وَالْفُرْقَانِ ﴿١٠﴾ فَمَنْ شَهِدَ مِنْكُمُ الشَّهْرَ
فَلِيَصُمِّهُ وَمَنْ كَانَ مَرِيضًا أَوْ عَلَى سَفَرٍ فَعِدَّهُ مِنْ
أَيَّامٍ أُخْرَى يُرِيدُ اللَّهُ بِكُمُ الْيُسْرَ وَلَا يُرِيدُ بِكُمُ
الْعُسْرَ وَلِتُكِبِّلُوا الْعِدَّةَ وَلِتُكَبِّرُوا اللَّهَ عَلَى مَا هَدَى لَكُمْ

Mada

- Utukufu wa Ramadhani, sharti la kufunga, sheria za mgonjwa na msafiri

Maoni

- ① Aya hii inaelezea wajibu wa kufunga katika Uislamu. Katika sheria ya Uislamu, kufunga ni kujizuia kula, kunywa na tendo la ndoa (kujamiihana) kuanzia Alfajiri (inapoanza Alfajiri) mpaka jua linapozama kwa nia halisi ya kufunga.
- ② Mgonjwa anasamehewa ikiwa kufunga kunaweza kuzidisha hali yake au kuhatarisha maisha yake, na msafiri anasamehewa anaposafiri umbali wa km 92 (makadirio, Maili 57.5) au zaidi.
- ③ Ramadhani ndiyo mwezi pekee uliotajwa ndani ya Qur'an kwa jina, ilipata utukufu kwa sababu ya uhusiano wake na Qur'an. Hili linadhihirisha kuwa wakati au tukio lolote linapohusishwa na jambo linaloheshimiwa, basi litaheshimiwa mpaka siku ya Hukumu; hivyo siku na nyakati zilizohusishwa na Baraka za Mazazi ya Mtume na safari yake ya Meraji, zikaheshimiwa.

amekupeni uwongofu, na ili mpate kushukuru.^①

وَلَعَلَّكُمْ تَشْكُرُونَ^②

2:186 Na ‘Ewe Mtume Kipenzi’! Waja wangu wanapokuuliza kuhusu mimi, basi mimi niko karibu. Nakubali dua ya mwenye kuniomba anaponiomba,^③ basi watii amri yangu na waniamini Mimi ili wapate uwongofu.

وَإِذَا سَأَلَكَ عِبَادٍ عَنِّيْ قَرِيبٌ أَجِيبُ دَعْوَةَ
الدَّاعِ إِذَا دَعَانِ لَقْلِيْسْتَجِيْبُوا لِيْ وَلَيْسُ مُؤْمِنِيْ لَعَلَّهُمْ
يَرْشُدُونَ^④

2:187 Mmehalalishiwa usiku wa Saumu kuingiliana na wake zenu.^⑤ Wao ni nguo kwenu na nyie ni nguo kwao. Mwenyezi Mungu anajua mlikuwa mkizikhini nafsi zenu, kwa hiyo akakubali toba zenu na akawasameheni; kwa hiyo sasa mshiriki nao kwenye tendo la ndoa na tafuteni katika yale Mwenyezi Mungu aliyowaandikia;^⑥ na kuleni na kunyweni mpaka uzi mweupe (Alfajiri) ubainike kwenu kutoka kwenye uzi mweusi (usiku); kisha kamilisheni funga mpaka usiku.

أَحَلَّ لَكُمْ لَيْلَةَ الْصِّيَامِ الرَّفَثَ إِلَى زِيَامَكُمْ هُنَّ لِبَاسٌ
لَكُمْ وَأَنْتُمْ لِبَاسٌ لَهُنَّ طَعْلَمَ اللَّهُ أَنَّكُمْ كُنْتُمْ
تَخْتَانُونَ أَنْفُسَكُمْ فَتَابَ عَلَيْكُمْ وَعَفَّعَنْتُمْ فَأُنَئِ
بَاشِرُ وَهُنَّ وَابْتَغُوا مَا كَتَبَ اللَّهُ لَكُمْ وَكُلُّوَا وَاشْرُبُوا
حَتَّىٰ يَتَبَيَّنَ لَكُمُ الْحَيْطُ الْأَبْيَضُ مِنَ الْخَيْطِ الْأَسْوَدِ مِنَ

Mada

- Kukubalika kwa dua na kuhimiza utii wa sheria
- Hukumu ya tendo la ndoa wakati wa Ramadhan na wakati wa kufanya itikafu; sheria zinazohusiana na mlo wa daku (suhur).

Maoni

- ① Kukamilisha idadi ilioamrishwa, inamaanisha siku Ishirini na tisa au thelathini za kufunga. Maelezo ya “mumtukuze Mwenyezi Mungu” ni kuwa Mwenyezi Mungu amewafundisha hukumu za dini yake basi mumtukuze na mumshukuru kwa jambo hili.
- ② Kuomba dua maana yake ni mja kutaja haja yake, na Kukubali dua ni Mwenyezi Mungu kumuitikia mja wake kwa kusema (Labbayka ‘Abdi). Ama kupata alichokiomba ni jambo lengine.
- ③ “Rafath” maana yake halisi ni maneno ya ndani kati ya mume na mke yasiotajwa mbele ya wengine. Hapa ina maana ya kujamiihana.
- ④ Maana moja ya kutafuta, “kile alichomrisha Mwenyezi Mungu” ni kwamba, Wanandoa wajamiiiane kwa nia ya kupata Watoto, ili idadi ya Waislamu iongezeke na dini iimarishwe.

Na wala msiingiliane nao wakati mmekaa Itikafu msikitini.^① Hii ndiyo mipaka ya Mwenyezi Mungu, basi msiikaribie. Hivyo Mwenyezi Mungu anabainishaaya zake kwa watu ili wapate kuwa wachamungu.

الفَجْرِ شَهَّادِتُمُ الصِّيَامَ إِلَى أَلَيْلٍ ۝ وَلَا تُبَاشِرُوهُنَّ وَأَنْتُمْ عَكِفُونَ لِفِي الْمَسْجِدِ طَتْلُكَ حُدُودُ اللَّهِ فَلَا تَقْرُبُوهَا

كَذَلِكَ يَبْيَضُ اللَّهُو أَيْتَهُ لِلنَّاسِ لَعَلَّهُمْ يَتَّقُونَ ۝

2:188 **Wala** msiliane mali nyinyi kwa nyinyi kwa dhulma, na wala msizipeleke kesi zao kwa mahakimu ili mpate kula sehemu ya mali za watu kwa dhambi hali yakuwa mnajua.^②

وَلَا تَأْكُلُوا أَمْوَالَكُمْ بَيْنَكُمْ بِالْبَاطِلِ وَتَدْلُوْا بِهَا إِلَيْكُمْ الْحُكَمَ لِتَأْكُلُوا فِرِيقًا مِنْ أَمْوَالِ النَّاسِ بِالْإِلْثَمِ وَأَنْتُمْ

تَعْلَمُونَ ۝

2:189 **Wanakuuliza** juu ya mwezi mpya.^③ Sema. "Hizi ni alama za nyakati kwa ajili ya watu na Hija". **Wala** sio wema kuingia kwenye majumba kwa kuvunja kuta zake za nyuma, bali mwema ni mchamungu,^④ na ingieni majumbani kupitia milango yake, na

يَسْكُونَكُمْ عَنِ الْأَهْلَةِ قُلْ هُنَّ مَوَاقِعُهُ لِلنَّاسِ وَالْحَجَّ وَلَيْسَ الْبَرِّ بِأَنْ تَأْتُوا الْبُيُوتَ مِنْ طُهُورِهَا وَلَكِنَّ الْبَرِّ مِنْ أَنْ تَقْرُبُوهَا وَأُتُوا الْبُيُوتَ مِنْ أَبُوئِهَا وَاتَّقُوا اللَّهَ

Mada

- Ni haramu kula (kupata) mali ya watu bila ya haki, na kuwalazimisha waitwe kwenye mahakama ya sheria kwa ajili hiyo.
- Hekima za awamu za mwezi.
- Uchamungu ndio wema wa kweli.

Maoni

^① Aya inasema, inaruhusiwa kwa mume na mke kujamiiiana wakati wa usiku wa Ramadhani, endapo tu mmoja wao hafanyi itikafu; imeharamishwa mtu kujamiiiana wakati yuko itikafu.

^② Kufungua kesi ya uongo dhidi ya mtu kwa faida isiyo halali, ni marufuku, na kutoa rushwa, au kuwashawishi watu wenye mamlaka kwa faida isiyo halali, kuwadhuwu wengine kwenye mchakato, pia ni marufuku. Wale wanaofungamana na watu wenye mamlaka, wanapaswa kuzingatia hukumu ya Aya hii.

^③ Ahillah (Neno la Qur'an) ni wingi wa neno la Kiarabu, hilāl—Mwezi mpya unaoonekana mwanzoni mwa mwezi mwandamo.

^④ Aya hii iliteremka kutokana na desturi ya zama za ujinga; kudhani kuwa kitendo hakiruhusiwi wakati sheria inakiruhusu, hiyo ni njia ya wajinga. Kubuni mila potofu na kijiwekea vikawazo hairuhusiwi. Wala hairuhusiwi kulazimisha tendo ambalo halilazimishwa kisheria.

muogopeni Mwenyezi Mungu ili mpare kufaulu.

لَعَلَّكُمْ تُفْلِحُونَ ﴿١٩﴾

2:190 Na piganeni katika njia ya Mwenyezi Mungu na wale wanaokupigeni, na msivuke mipaka. Hakika Mwenyezi Mungu hawapendi wenyewe kuvuka mipaka.

وَقَاتِلُوا فِي سَبِيلِ اللَّهِ الَّذِينَ يُقَاتِلُونَكُمْ وَلَا تَعْتَدُوا إِنَّ اللَّهَ لَا يُحِبُّ الْمُعْتَدِلِينَ ﴿٢٠﴾

2:191 Na (wakati wa Jihadi) wauweni makafiri popote mutakapowakuta na watoeni sehemu^① waliyokutoeni; na fitina ni mbaya kuliko mauaji. Wala msipigane nao karibu na Msikit Mtukufu mpaka wakupigeni huko, wakikupigeni huko nanyi wauweni. Hivyo ndivyo yalivyo malipo ya makafiri.^②

وَاقْتُلُوهُمْ حَيْثُ ثَقْفُسُوهُمْ وَأَخْرِجُوهُمْ مِّنْ حَيْثُ أَخْرَجُوكُمْ وَالْفِتْنَةُ أَشَدُّ مِنَ الْقَتْلِ وَلَا تُقْتِلُوهُمْ عِنْدَ الْمَسْجِدِ الْحَرَامِ حَتَّىٰ يُقْتَلُوكُمْ فِيهِ فَإِنْ فَتَكُوكُمْ فَاقْتُلُوهُمْ طَكْلِكَ جَزَ آءُ الْكُفَّارِينَ ﴿٢١﴾

2:192 Kisha wakiacha basi Mwenyezi Mungu ni Mwingi wa Kusamehe na Mwenye Kurehemu.

فَإِنْ اتَّهَوْا فَإِنَّ اللَّهَ غَفُورٌ رَّحِيمٌ ﴿٢٢﴾

2:193 Na piganeni nao mpaka pasiwe na fitna,^③ na ibada iwe ya Mwenyezi Mungu. Kisha kama wakiacha basi adhabu kali itabaki kwa madhalimu tu.

وَلْقَتُلُوهُمْ حَتَّىٰ لَا تَكُونَ فِتْنَةً وَيُكُونَ الَّذِينَ يُلِهُ طَقْلِكَ اتَّهَوْا فَلَا عُدُوانَ إِلَّا عَلَى الظَّالِمِينَ ﴿٢٣﴾

2:194 Mwezi Mtukufu kwa mwezi Mtukufu, na vitu vitakatifu vimeekewa kisasi. Basi yule

الْشَّهْرُ الْحَرَامُ بِالشَّهْرِ الْحَرَامِ وَالْحُرُمَ مُتْ قَصَاضٍ طَقْلِكَ

Mada

- Amri ya Jihadi na kukataza kupita mipaka.
- Sheria ya kuwaua makafiri wakati wa Jihadi, na kukataza kuanzisha vita katika eneo tukufu (Haram).
- Amri ya Jihadi dhidi ya makafiri wa Arabuni mpaka ushirikina ufile ukomo.
- Kuwatumanisha Waislamu baada ya kupigana vita wakati wa mwezi mtukufu.

Maoni

- ① Hii inahusu hasa kuua makafiri katika mazingira ya kivita, na si amri isiyo na ukomo ya kuua kiholela katika kila hali bila kuzingatia amani au vita.
- ② Waislamu hawaruhusiwi kupigana ndani ya Eneo Tukufu la Haram kwani hii inapinga utukufu wa eneo hilo. Hata hivyo, kama makafiri wataanzisha vita dhidi ya Waislamu katika eneo hilo tukufu, basi inaruhusiwa kupambana nao.
- ③ Hapa fitnah maana yake ni ushirikina.

anayewashambulia nanyi mshambulieni kwa kadiri alivyo kushambulieni na mcheni Mwenyezi Mungu, na mjue kuwa Mwenyezi Mungu yu pamoja na wanaomcha.^①

فَمَنِ اعْتَدَى عَلَيْكُمْ فَاعْتَدُوا وَاعْلَمُوا بِشِلْ مَا اعْتَدَى
عَلَيْكُمْ وَاتَّقُوا اللَّهَ وَاعْلَمُوا أَنَّ اللَّهَ مَعَ الْمُتَّقِينَ ^(١٣)

2:195 Na toen katika njia ya Mwenyezi Mungu, wala msijitie katika maangamizo kwa mikono yenu, na mfanye wema, Hakika Mwenyezi Mungu anawapenda wafanyao wema.

وَأَنْفَقُوا فِي سَيِّلِ اللَّهِ وَلَا تُنَقِّوا بِأَيِّ يَنْعِيمٍ إِلَى الشَّهْلَكَةِ
وَأَحْسُنُوا إِنَّ اللَّهَ يُحِبُّ الْمُحْسِنِينَ ^(١٤) مع

2:196 Na kamilisheni Hijja na Umrah kwa ajili ya Mwenyezi Mungu. Basi, kama mumezuiliwa (kuingia Makka),^② basi (mtumeni ndani ya Haram) mnyama wa kuchinjwa anayepatikana kwa urahisi; na musinyoe vichwa vyenu mpaka mnyama wa kuchinjwa afike sehemu yake. Basi mionganoni mwenu atakayekuwa mgonjwa au ana maradhi ya kichwa, basi atoe fidiya kwa swaumu au sadaka au kuchinja mnyama.^③ Kisha mtakapokuwa katika amani, basi

وَأَتِمُوا الْحَجَّ وَالْعُرْمَةَ لِلَّهِ قَلْنَ أُحْصِرْتُمْ فَمَا أَسْبَسْرَمْنَ
الْهَدْيَ وَلَا تُحَلِّقُوا أُمُّا عُوْ سَكْمَ حَتَّى يَبْلُغَ الْهَدْيُ
مَحِلَّهُ فَمَنْ كَانَ مِنْكُمْ مَرِيضاً أَوْ بَهْ أَذْيَى مِنْ رَأْسِهِ
فَفَدِيَّتُهُ مِنْ صِيَامِ أَوْ صَدَقَةِ أَوْ نُسُكٍ فَإِذَا آتَيْتُمْ ^{وَقَنَة}

Mada

- Amri ya kutumia katika njia ya Mwenyezi Mungu na kuharamisha kujiangamiza
- Baadhi ya sheria na adabu zinazohusiana na Hijja na Umrah.
- Sheria ya kuzuiwa kuingia kwenye Hijja (ihṣār).
- Tamattu' and Qirān; Kuunganisha Hijja na Umrah katika safari moja.

Maoni

^① Zingatia ustaarabu wa hali ya juu, tabia njema, na kuepuka ukandamizaji katika Uislamu; pale adui anapokamatwa na mtu ana hisia kali za kulipiza kisasi, Waislamu wanaelekezwa kutumia uchamungu na haki ili kuepuka kuvuka mipaka katika kulipiza kisasi chao.

^② ihṣār maana yake ni kutoweza kutimiza Hijja au umra baada ya kufunga ehram kwasababu ya hofu ya kuvamiwa na adui au mnyama au kuzidiwa na maradhi.

^③ Jambo lilokatazwa kufanywa wakati wa ehram lenye kuwajibisha kuchinja, likifanywa kwa dharura ya ugonjwa, jeraha au maradhi kichwani, basi kuna hiari ya kutoa sadaka moja moja kwa maskini 6 au kuwalisha siku moja mara mbili kiasi cha kuwashibisha au kufunga siku 3 au kuchinja.

yeote atakayechukua faida ya kuunganisha Umrah na Hijja, ni lazima kwake, kuchinja manyama anaepatikana kwa urahisi; na asiyepata (uwezo wa kuchinja), basi afunge siku tatu wakati wa siku za Hijja na siku saba mtakaporudi majumbani mwenu. Hizi ni kumi kamili.^① Hii sheria ni kwa yule asiyekuwa mkazi wa Makka.^② Na mcheni Mwenyezi Mungu, na mjue kuwa Mwenyezi Mungu ni mkali wa kuadhibu.

فَمَنْ تَمَّتَّعَ بِالْعُرْمَةِ إِلَى الْحَجَّ فَمَا أُسْتَيْسَرَ مِنَ الْهُدُىٰ

فَمَنْ لَمْ يَحِدْ فَصِيَامُ ثَلَاثَةِ أَيَّامٍ فِي الْحَجَّ وَسَبْعَةٌ

إِذَا رَاجَعْتُمْ تِلْكَ عَشَرَةَ كَامِلَةً ذَلِكَ لِمَنْ لَمْ يَكُنْ

أَهْلَهُ حَاضِرٍ بِالْمَسْجِدِ الْحَرَامِ وَاتَّقُوا اللَّهَ وَاعْلَمُو

أَنَّ اللَّهَ شَدِيدُ الْعِقَابِ^{١٩٦}

2:197 **Hijja** ni miezi maalumu; basi mwenye kutia nia ya kufanya Hijja katika miezi hiyo, basi akiwa humo ndani ya Hijja pasitajwe mambo ya kujamiihana mbele ya wanawake, wala pasiwepo dhambi wala ugomvi. Na wema wowote mnaoufanya, Mwenyezi Mungu anaujua. **Na** chukueni masurufu, kwani masurufu iliyo bora, hakika ndiyo uchamungu; na niogopeni mimi, enyi watu wenye akili!^③

الْحَجُّ أَشْهُرٌ مَعْلُومٌ فَمَنْ فَرَضَ فِيهِنَّ الْحَجَّ فَلَا رَفَثٌ

وَلَا فُسُوقٌ وَلَا جَدَالٌ فِي الْحَجَّ وَمَا تَفَعَّلُوا مِنْ خَيْرٍ

يَعْلَمُهُ اللَّهُ وَتَرَوْدُوا فَإِنَّ خَيْرَ الرَّادِ التَّقْوَىٰ وَ

إِنَّقُونَ يَأْوِي إِلَى لَبَابٍ^{١٩٧}

2:198 **Hakuna** dhambi juu yenu kuitafuta fadhila ya Mola wenu Mlezi. Basi mtakaporudi kutoka Arafat, mkumbukeni Mwenyezi

لَيْسَ عَلَيْكُمْ جُنَاحٌ أَنْ تَبْتَغُوا فَضْلًا مِنْ رَبِّكُمْ فَلَا

Mada

- Nani ana ruhusa ya kufanya Hijja ya Tamattu' au Hijja ya Qirān?
- Baadhi ya makatazo ya Hijja.
- Uchamungu ni masurufu bora ya safari.
- Ruhusa ya kufanya biashara wakati wa Hijja na amri ya kumkumbuka Mwenyezi Mungu Mtukufu mara kwa mara

Maoni

^① Mwenye kuunganisha Hajj na Umra kwenye safari moja analazimika kuchinja kwa kutoa shukrani. Na kama hana uwezo wa kuchinja basi afunge siku 10. Afunge siku 3 baada ya kufunga ehraam kwanzia tarehe mosi Shawwal hadi tarehe 9 dhul hijja. Kisha amalize kufunga siku 7 baada ya tarehe 13 dhul hijja.

^② Hijja ya Tamattu na Qiraan (kuunganisha Hijja na Umra) ni kwa wale wanao kaa nje ya mipaka ya Miqaat. Ama kwa wale wanaoishi ndani ya mipaka ya Miqaat wanaruhusiwa tu kufanya Hijja ya Ifraad (Hijja peke yake bila ya kufanya Umra).

^③ Marejeo kwa "watu wenye akili" ina maana kuwa wenye akili ya kweli inahusisha kumcha Mwenyezi Mungu Mtukufu na kwa yule asiyemcha Mwenyezi Mungu Mtukufu, kimsingi hana akili.

Mungu penye Mash'ar-ul-Harām; na mkumbukeni yeye kama alivyowapa uwongofu, ingawa kabla ya hili mlikuwa mionganoni mwa waliopotea.

أَفَلَمْ يَرَوْا مِنْ عَرَفٍ فَادْكُرُوا اللَّهَعِنَدَالْمُشْعَرِالْحَرَامِ وَ
إِذْ كُرُوْكُهَاكَاهَدْلُكُمْ وَإِنْ كُنْتُمْ مِنْ قَبْلِهِ لِمِنَالضَّالِّيْنَ ⑯٨

2:199 Kisha, ‘Enyi watu wa Maquraishi,’ rudini kutoka sehemu ile ile wanayorudi wengine^①, na ombeni msamaha kwa Mwenyezi Mungu; hakika, Mwenyezi Mungu ni Mwingi wa Kusamehe, Mwingi wa Kurehemu.

ثُمَّ أَفِيْضُوا مِنْ حَيْثُ أَفَاضَ النَّاسُ وَاسْتَغْفِرُوا اللَّهَ إِنَّ
اللَّهَغَفُورُرَحِيمٌ ⑯٩

2:200 Kisha mkimaliza ibada zenu za Hijja, mkumbukeni Mwenyezi Mungu kama vile mlivyokuwa mkiwakumbuka baba zenu, bali mkumbukeni yeye zaidi ya hao.^② Na mionganoni mwa watu, mtu husema, “Ewe Mola wetu Mlezi! Tupe duniani”^③ na kwake yeye hana fungu katika Akhera.

فَإِذَا قَصَدُتُمْ مَنَاسِكُكُمْ فَادْكُرُوا اللَّهَ كَنِّيْتُكُمْ إِذَا عَلِمْتُمْ
أَشَدَّ ذُكْرًا طَقْنَالنَّاسِ مِنْ يَقُولُ رَبَّنَا آتَنَا فِي الدُّنْيَا
مَالَهُ فِي الْآخِرَةِ مِنْ خَلَاقِي ⑭

2:201 Na mmoja wao husema “ Ewe Mola wetu Mlezi! Utupe mema duniani na utupe mema akhera (pia), na utulinde na adhabu ya Moto”.

وَمِنْهُمْ مَنْ يَقُولُ رَبَّنَا آتَنَا فِي الدُّنْيَا حَسَنَةً وَّ
الْآخِرَةَ حَسَنَةً وَّقِنَاعَزَابَ النَّاسِ ⑯١٥

Mada

- Tofauti ya dua kati ya mtafutaji wa dunia na mtafutaji wa Akhera

Maoni

^① Watu wa Maquraishi wangeamua kusimama Muzdalifah badala ya kuungana na wengine huko Arafat. Baada ya wengine kurudi kutoka Arafat, Maquraishi wangerudi kutoka Muzdalifah kama kuonyesha kuwa wao ni bora kuliko wengine. Aya inawaamrisha Maquraishi kuwa wasimame Arafaat kama watu wengine na warudi pamoja nao. Sheria za kiislamu hazibadilili kwa makabila au vyeo vya kijamii; tajiri au maskini, mweupe au mweusi, Muarabu au asiyekuwa Muarabu, watu wote ni sawa katika kufuata sheria za Uislamu.

^② Katika enzi ya Ujinga, Waarabu wangewasifu wazee wao karibu na Ka'bah baada ya kuhiji. Uislamu umewafundisha kuwa, haya ni maonyesho yasiyo na maana, ya umaarufu na majivuno ambayo yanapaswa kubadilishwa na kumkumbuka Mwenyezi Mungu Mtukufu.

^③ Kumbuka, inaruhusiwa kwa Muumini kuomba dua kwa ajili ya kuboresha mambo yake ya kidunia. Kama hili likifanywa ili kuunga mkono Uislamu, basi dua yake itazingatiwa kuwa ni suala la dini. Lakini kuomba kwa ajili ya dunia peke yake na kusahau akhera ni jambo ambalo halimfai Muumini.

2:202 Hawa watu watapata sehemu katika yale waliyoyachuma na Mwenyezi Mungu ni Mwepesi wa Kuhesabu.

أُولَئِكَ لَهُمْ نَصِيبٌ مِّمَّا كَسَبُوا طَوْلَةٌ وَاللَّهُ سَرِيعُ الْحِسَابِ ﴿٢٣﴾

2:203 Na mtajeni Mwenyezi Mungu katika siku maalumu.^① Basi mwenye kufanya haraka kuondoka ndani ya siku mbili (katika Mina), hana dhambi juu yake^②, na mwenye kukaa (pia) juu yake hana dhambi. (Habari njema hii ni) kwa mwenye kumcha Mungu. Na mcheni Mwenyezi Mungu na mjue kuwa kwake mtakusanywa.

وَادْعُرُوا اللَّهَ فِي آيَاتِهِ مَدْعُودُاتٍ فَإِنْ تَعَجَّلَ فِي يَوْمِ مَيْتٍ فَلَا إِثْمَ عَلَيْهِ وَمَنْ تَأَخَّرَ فَلَا إِثْمَ عَلَيْهِ لَكِنْ اتَّقِ وَاتَّقُوا اللَّهَ وَاعْلَمُوا أَنَّكُمْ إِلَيْهِ تُحْشَرُونَ ﴿٢٤﴾

2:204 Na katika watu, yuko ambaye maneno yake yanakufurahisha katika maisha ya dunia na akamfanya Mwenyezi Mungu shahidi kwa yale yaliyo moyoni mwake, wakati yeze ndiye mkubwa wa ugomvi.

وَمِنَ النَّاسِ مَنْ يُعِجبُكَ قَوْلُهُ فِي الْحَيَاةِ الدُّنْيَا وَيُشَهِّدُ إِنَّ اللَّهَ عَلَىٰ مَا فِي قَلْبِهِ وَهُوَ أَلَّا يَخْصَمُ ﴿٢٥﴾

2:205 Na anapokengeuka hufanya juhud ya kueneza ufisadi katika ardhi, na kuharibu mimea na mifugo. Na Mwenyezi Mungu hapendi ufisadi.^③

وَإِذَا تَوَلَّ سَعْيَ فِي الْأَرْضِ لِيُفْسِدَ فِيهَا وَيُهَلِّكَ الْحَرَثَ وَالثَّسْلَ وَاللَّهُ لَا يُحِبُّ الْفَسَادَ ﴿٢٦﴾

Mada

- Hukumu zinazohusiana na kukaa Minā.
- Maovu sita ya mnafiki mmoja.

Maoni

^① Hapa “siku maalumu” inaongelea muda wa kuanzia Alfajir ya 9, Dhu’l Hijjah mpaka Alasiri ya 13, Dhu’l Hijjah (Siku za Tashriq). Kumdhukuru Mwenyezi Mungu Mtukufu, ina maana ya kuutangaza ukuu wa Mwenyezi Mungu (takbir) baada ya swala zilizofaradhishwa na wakati wa kuzipiga mawe nguzo. Maana ya Aya ni kuwa mujishughulishe na kumkumbuka Mwenyezi Mungu Mtukufu wakati wa kukaa huko Mina.

^② Hapa maana ya kuondoka Mina ndani ya siku mbili ni siku mbili baada ya siku ya 10 ya Dhu’l Hijjah. Kama mtu akirejea kutoka Mina, baada ya kurusha mawe siku ya 12, hakuna dhambi juu yake ingawa ni bora kurudi baada ya kupiga mawe kwenye nguzo siku ya 13.

^③ Ingawa Ayah hii iliteremshwa mwanzoni kuhusu mnafiki makhsusi, inatoa muongozo kwa watu wote wenye tabia kama hizo. Kwenye jamii yetu, watu wengi wanaonekana wenye adabu, wanaongea vizuri na wanyenyekemu, lakini wanapotosha kwa siri maagizo ya kidini, wanazua ugomvi mionganoni mwa watu, na kusambaratisha familia.

2:206 Na anapoambiwa. “Mche Mwenyezi Mungu!” basi ukaidi wake unamchochea kufanya dhambi zaidi, basi huyu inamtosha Jahan-nam na hakika hayo ni makazi mabaya. ①

وَإِذَا قِيلَ لَهُ أَتَقْ أَنَّهُ أَخَذَتْهُ الْعِزَّةُ بِالْإِلَهِ فَحَسِبَهُ جَهَنَّمَ
وَلَيْسَ الْهَادُونَ ②

2:207 Na mionganini mwa watu, yuko anayeuzua maisha yake kwa kutafuta radhi za Mwenyezi Mungu na Mwenyezi Mungu ni Mpole kwa waja wake.

وَمِنَ النَّاسِ مَنْ يَشْرِنِي نَفْسَهُ أَبْتِغَاءَ مَرْضَاتِ اللَّهِ وَاللهُ
رَاعُوفٌ بِالْعِبَادِ ③

2:208 Enyi mlionamini! Ingieni kwenye Uislamu kikamilifu, na wala msifuate nyayo za Shetani. Hakika, ye ye ni adui yenu wa wazi.

يَا أَيُّهَا النَّاسُ إِذْ آمَنُوا دُخُلُوا فِي السَّلَامِ كَافَةً وَلَا تَتَّبِعُو
خُطُواتِ الشَّيْطَنِ إِنَّهُ لَكُمْ عَدُوٌّ مُّبِينٌ ④

2:209 Na mkiteleza hata baada ya kukufikieni Aya zilizo wazi, basi jueni kuwa, Mwenyezi Mungu ni Mwenye Nguvu na Mwenye Hekima. ⑤

فَإِنْ زَلَّتُمْ مِّنْ بَعْدِ مَا جَاءَكُمُ الْبِيِّنُتُ فَاعْلَمُوا أَنَّ اللَّهَ
عَزِيزٌ حَكِيمٌ ⑥

2:210 Je! Wanangojea adhabu ya Mwenyezi Mungu iwasikie katika vivuli vya mawingu, na Malaika, na hukumu iwe imeshatolewa; na mambo yote yanarejea kwa Mwenyezi Mungu peke yake.

هَلْ يَنْظُرُونَ إِلَّا أَنْ يَأْتِيَهُمُ اللَّهُ فِي ظُلْلٍ مِّنَ الْعَمَاءِ وَ
الْمَلِئَةُ وَقُضِيَ الْأَمْرُ وَإِنَّ اللَّهَ تُرْجِعُ الْأُمُورُ ⑦

Mada

- Kuuza maisha ya mtu kwa ajili ya radhi za Mwenyezi Mungu Mtukufu ni biashara yenyeye faida.
- Amri ya kuzingatia kikamilifu Sheria ya Kiislamu.
- Kuupinga Uislamu licha ya dalili zilizo wazi ni kosa kubwa.
- Wale wanaaoacha Uislamu wanangojea adhabu ya Mwenyezi Mungu.

Maoni

① Kutokukubali kosa ni ishara ya unafiki, pale mnafiki anaporekebishwa hufanya ukaidi. Kwa mnafiki, kusahihishwa ni kushusha heshima yake. Isivyo bahati, unafiki umeenea ulimwenguni.

② Hii ina maana kuwa ni kosa kubwa kujiweka mbali na kuingia kwenye Uislamu kikamilifu, na kuchukua njia inayopinga Uislamu, licha ya uthibitisho wa wazi.

2:211 Waulize Wana Israili, tuliwapa ishara ngapi za wazi^①. Na mwenye kubadilisha neema ya Mwenyezi Mungu baada ya kumjia, basi hakika Mwenyezi Mungu ni mkali wa kuadhibu.^②

سَلْ بَنِي إِسْرَائِيلَ كَمَا أَتَيْنَاهُم مِّنْ آيَاتِنَا وَمَنْ يُبَدِّلْ نِعْمَةَ اللَّهِ مِنْ بَعْدِ مَا جَاءَهُ فَإِنَّ اللَّهَ شَدِيدُ الْعِقَابِ

2:212 Maisha ya dunia yamefanywa kuwa ya kuvutia kwa walio kufuru,^③ na wanawafanyia maskhara wale walioamini. Na wamchao Mwenyezi Mungu, watakuwa juu ya makafikri siku ya Kiyama.^④ Na Mwenyezi Mungu humruzku amtakaye bila ya hesabu.

نُّزِّلَ لِلَّذِينَ كَفَرُوا وَالْحَيُّوُاتُ الدُّنْيَا وَيَسْعَرُونَ مِنَ الظِّنَنِ أَمْنُوا وَالَّذِينَ أَنْقَذُوا فَوْقَهُمْ يَوْمَ الْقِيَامَةِ وَاللَّهُ يَرْزُقُ مَنْ يَشَاءُ بِغَيْرِ حِسَابٍ

2:213 Watu wote walikuwa umma mmoja. Basi Mwenyezi Mungu akawatuma Manabii wabashiri na waonyaji na akateremsha pamoja nao Kitabu kwa Haki, ili kuhukumu baina ya

كَانَ النَّاسُ أُمَّةً وَاحِدَةً فَبَعَثَ اللَّهُ النَّبِيِّنَ مُّبَشِّرِينَ وَمُنذِّرِينَ وَأَنْزَلَ مَعَهُمُ الْكِتَابَ بِالْحِقِّ لِيَحُكِّمَ بَيْنَ

Mada

- Kuwauliza Waisraili kuhusu dalili zilizo wazi.
- Onyo kwa wanao badilisha neema za Mwenyezi Mungu Mtukufu
- Kupambwa maisha ya dunia kwa ajili ya makafiri na kuwanyayua Waislamu juu ya makafikri siku ya Kiyama
- Sababu ya kuhitilafiana baina ya watu baada ya muongozo wa Mitume na mafundisho ya haki kwa Waislamu

Maoni

- ① Kumbukeni kuwauliza Waisraili kuhusu dalili zilizo wazi ni kwa ajili ya kuwanasihi na kuzikubali neema za Mwenyezi Mungu Mtukufu pamoja na makosa yao.
- ② “Neema ya Mwenyezi Mungu” inarejea kwenye Aya za Mwenyezi Mungu Mtukufu ambazo zina njia ya uwongovu na uokovu kutoptofu. Na mionganini mwa aya hizo ni zile zinazoleza sifa za Mtume wetu Kipenzi صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ na kuutaja Utume wake. Mayahudi na Wakristo kuzibadilisha kwao Aya hizi ni kama kubadilisha Neema ya Mwenyezi Mungu.
- ③ Maisha ya Dunia kufanywa kuwa ya kuvutia kwa makafiri maana yake ni kuwa wanayapenda maisha haya tu na kuyathamini, na kuyatamani. Kumbuka, maisha ya kidunia ni yale yanayotumika kwa kufuata matamanio ya nafsi, ambapo maisha yanayotumika kukusanya faida ya Akhera kwa fadhila ya Mwenyezi Mungu Mtukufu ni maisha ya kidini.
- ④ Kumdhihaki Muislamu maskini au kumdharaau Muumini ni vitendo vya makafiri. Kwa hiyo mtenda maovu au kafiri haheshimiki hata kama ni tajiri, wakati Muumini anaheshimika hata akiwa maskini bila ya kujali nasaba yake, maadamu yeze ni mchamungu.

watu katika yale waliokhitalifiana. Na wala hawakukhitalifiana ila wale waliopewa kitabu hicho baada ya kuwajia ishara zilizo wazi, kwa sababu ya uhasidi baina yao. Basi Mwenyezi Mungu kwa idhini yake, aliwaongoza wale walioamini kwenye haki katika mambo ambayo watu walikuwa wakikhitilafiana^①. Na Mwenyezi Mungu humuongoa njia iliyonyooka amtakaye.

2:214 Je! Mnadhani mtaingia^② peponi kabla hamjakabiliana na hali ya wale waliotangulia kabla yenu? Walipatwa na dhiki na machungu, na walitikiswa kwa nguvu mpaka Mtume na walio amini pamoja nae wakasema, “Nusura ya Mwenyezi Mungu itakuja lini?” Jueni, hakika nusura ya Mwenyezi Mungu iko karibu.

2:215 Wanakuuliza watoe nini? Sema; “Kheri munayoitoa ni kwa ajili ya wazazi na ndugu wa karibu na mayatima na maskini^③ na msafiri, na kheri yoyote mnayoifanya, hakika Mwenyezi Mungu anaijua.”

النَّاسُ فِيْمَا اخْتَلَفُوا فِيْهِ طَوْهُرٌ وَمَا اخْتَلَفَ فِيْهِ إِلَّا الَّذِينَ أُوتُوهُ مِنْ بَعْدِ مَا جَاءَهُمُ الْبَيِّنُاتُ بَعْيَادِهِمْ فَهُدَى اللَّهُ الَّذِينَ آمَنُوا إِلَيْهَا اخْتَلَفُوا فِيْهِ مِنَ الْحَقِّ بِإِذْنِهِ وَاللَّهُ يَعْلَمُ بِمَا يَصْنَعُونَ

أَمْ حَسِبْتُمْ أَنْ تَرْكُلُوا الْجَنَّةَ وَلَيَأْتِكُمْ مَثْلُ الَّذِينَ خَلَوْا مِنْ قَبْلِكُمْ مَمَّا شَاءُوا وَالصَّرَاطُ مُرْبُّلٌ لَوْا حَتَّى يَقُولَ الرَّسُولُ وَالَّذِينَ آمَنُوا مَعَهُ مَثْلُ نَصْرَ اللَّهِ أَلَا إِنَّ نَصْرَ اللَّهِ قَرِيبٌ

يَسْأَلُونَكَ مَاذَا يُفْقِدُونَ قُلْ مَا أَنْفَقْتُمْ مِنْ خَيْرٍ فَلَمَّا كَانُوا إِلَيْهِمْ وَالآتُوكَرْبَيْنَ وَالْيَسْمَى وَالسَّكِينَ وَابْنَ السَّبِيلِ وَمَا تَفَعَّلُوا مِنْ خَيْرٍ فَإِنَّ اللَّهَ بِهِ عَلِيمٌ

Mada

- Mitihani ya Waislamu na magumu ya umma waliyopita.
- Kiwango bora na sehemu za kutoa sadaka za hiyari.

Maoni

^① Kuhitilafiana kimsingi hakulaaniwi, ingawa kuhitilafiana na hukumu ya Mwenyezi Mungu Mtukufu na Mtume wake ، صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ ، na kuhitilafiana baada ya haki kuwekwa wazi, kumelaaniwa.

^② Aya hii iliteremshwa kuhusiana na Vita vya Handaki ambapo Waislamu walikabiliana na hali ya hewa ya baridi kali na njaa. Walishauriwa kuwa na Subira na wakakumbushwa kuwa walioeteuliwa na Mwenyezi Mungu daima hukabiliana na magumu.

^③ Aya hii inahusu sadaka ya hiyari. Haijuzu kutoa zaka na sadaka ya lazima kwa wazazi.

2:216 **Imefaradhishwa** juu yenu Jihadi ingawa kwenu haipendezi; na huenda mkachukia kitu nacho ni kheri kwenu; na huenda mkapenda kitu nacho ni shari kwenu; Na Mwenyezi Mungu anajua, na nyinyi hamjui.^①

كُتِبَ عَلَيْكُمُ اقْتَالُ وَهُوَ كُرْهَ لَكُمْ وَعَسَى أَنْ تَكْرُهُوا
شَيْئًا وَهُوَ خَيْرٌ لَكُمْ وَعَسَى أَنْ تُحْبُّو شَيْئًا وَهُوَ شَرٌّ
لَكُمْ طَوَّلَ اللَّهُ يَعْلَمُ وَأَنْتُمْ لَا تَعْلَمُونَ ﴿١٧﴾

2:217 **Wanakuuliza** kuhusu kufanya Jihadi katika mwezi mtukufu, sema; “Kupigana vita katika mwezi huu ni dhambi kubwa. Na kuzuilia njia ya Mwenyezi Mungu na kumkufuru, na kuzuilia kuingia kwenye Msikiti Mtukufu, na kuwafukuza wakaao humo ni dhambi kubwa zaidi mbele ya Mwenyezi Mungu^②; Na fitna ni mbaya zaidi kuliko kuua. Na wala hawataacha kupigana nanyi mpaka wakutoeni katika dini yenu kama wakiweza.^③ Na yeote mionogoni mwenu akiacha Dini yake na akafa hali ya kuwa ni kafiri, basi hao ndio ambaa amali zao zote zimebatilika duniani na Akhera; na hao

يَسْأَلُونَكُمْ عَنِ الشَّهْرِ الْحَرَامِ قِتَالٍ فِيهِ قُلْ قِتَالٌ فِيهِ
كَبِيرٌ وَصَدُّعَنْ سَبِيلِ اللَّهِ وَكُفَّارُهُ وَالسُّجُورُ
الْحَرَامُ وَإِخْرَاجُ أَهْلِهِ مِنْهُ أَكْبَرُ عِنْدَ اللَّهِ وَالْفِتْنَةُ
أَكْبَرُ مِنَ القَتْلِ وَلَا يَرَأُونَ يُقَاتَلُونَ كُمْ حَتَّىٰ يَرِدُوكُمْ
عَنْ دِينِكُمْ إِنِ اسْتَطَاعُوا ۖ وَمَنْ يَرِدَ مِنْكُمْ عَنْ دِينِهِ
فَيَمْسُتُ وَهُوَ كَافِرٌ فَأُولَئِكَ حَمِطْتُ أَعْيَانَهُمْ فِي الدُّنْيَا

Mada

- Kufaradhishwa Jihadi na nasaha kwa Waislamu.
- Ruhusa ya kufanya Jihadi katika mwezi mtukufu
- Adhabu ya mtu anayekufa katika hali ya kuritadi

Maoni

- ① Haipaswi kila wakati mtu kuamua zuri au baya kwa akili yake. Bali kigezo cha mwisho kiwe amri ya Mwenyezi Mungu Mtukufu. Alivyoamrisha Mwenyezi Mungu Mtukufu ni bora kwetu, na alivyokataza Mwenyezi Mungu Mtukufu si bora kwetu.
- ② Hii inathibitisha kuwa kuwakosoa wengine licha ya mwenyewe kuwa na makosa makubwa zaidi ni njia ya makafiri. Ugonjwa huu umezagaa sana kwenye zama zetu. Watu hukosoa na kusengenya ulimwengu mzima, wakati wao wenyewe wamejichafua na maovu makubwa zaidi.
- ③ Aya inaeleza jinsi makafiri watakavyowachukia Waislamu daima na kujitahidi kuwaondoa kwenye dini yao. Leo, taasisi nyingi za makafiri wanafanya kazi kwa njia za ubunifu kuwatenganisha Waislamu na Uislamu, kuharibu maadili yao, na kudhoofisha Imani yao.

ni watu wa motoni; watabaki humo milele.^①

وَالْآخِرَةِ وَأُولَئِكَ أَصْحَابُ التَّارِيْخِ هُمْ فِيهَا خَلِدُوْنَ^{٢٦١}

2:218 Hakika, wale walioamini, na wale walioacha majumba yao kwa ajili ya Mwenyezi Mungu na kupigana Jihadi katika njia ya Mwenyezi Mungu, hao wanataraji rehema za Mwenyezi Mungu.^② Na Mwenyezi Mungu ni Mwingi wa Kusamehe, Mwenye Kurehemu.

إِنَّ الَّذِينَ امْسَأَوْا إِلَى الْزِيْنَ هَاجَرُوا وَجَهْدُهُمْ فِيهَا خَلِدُوْنَ^{٢٦٢}

اللَّهُ أَوْلَئِكَ يَرْجُونَ رَحْمَتَ اللَّهِ وَاللَّهُ غَفُورٌ رَّحِيمٌ^{٢٦٣}

2:219 Wanakuuliza kuhusu pombe na kamari. Sema; “Ndani yake kuna dhambi kubwa na manufaa ya dunia kwa watu.” Na madhara yake ni makubwa kuliko manufaa yake **Na wanakuuliza** nini watoe (katika njia ya Mwenyezi Mungu)? Sema, “Ziada” Hivyo ndivyo, Mwenyezi Mungu anakubainishieni Aya ili mpate kutafakari.

بِسْمِ اللَّهِ الرَّحْمَنِ الرَّحِيمِ قُلْ فِيهِمَا آثَمُ كَيْرِرُوْ

مَنَافِعُ لِلنَّاسِ وَإِثْمُهَا أَكْبَرُ مِنْ نَفْعِهَا وَبِسْمِ اللَّهِ

مَا ذَيْنَقُونَ قُلْ الْعَفْوُ كُلُّ الْعَفْوُ كُلُّ لِكَبِيرٍ يَبْيَنُ اللَّهُ لَكُمُ الْأَيْتَ

لَعَلَّكُمْ تَتَفَكَّرُوْنَ^{٢٦٤}

فِي الدُّنْيَا وَالْآخِرَةِ وَبِسْمِ اللَّهِ عَنِ الْيَتَامَىٰ قُلْ

إِصْلَاحٌ لَّهُمْ خَيْرٌ وَإِنْ تُخَالِطُوهُمْ فَإِحْوَانُكُمْ وَاللَّهُ

Mada

- Wenye kuamini, kuhama, kufanya Jihadi na matendo kama hayo wana matumaini katika Rehema ya Mwenyezi Mungu.
- Marufuku ya pombe na kamari.
- Kiasi cha sadaka.
- Sheria ya kuunganisha mali ya mtu na mali ya yatima.

Maoni

^① Kumbuka, kuritadi ni kosa kubwa. Siku hizi, Waislamu wengi hawajui msingi wa kiitikadi, na hivyo hutamka kauli za kukufuru kwa urahisi katika nyakati za furaha au huzuni.

^② Matendo mema hayalazimishi malipo kutoka kwa Mwenyezi Mungu Mtukufu. Bali anawalipa viumbe kwa fadhila zake.

^③ Ingawa aya hii inataja kutengeneza mambo ya kifedha ya mayatima, inajumuisha masuala yote ya utengenezaji; tabia, matendo, malezi, na elimu. Yatima ni kama Watoto wa umma wa Kiislamu

anamjua mharibifu na mtengenezaji,^① na lau Mwenyezi Mungu angetaka angekutieni katika taabu. Hakika Mwenyezi Mungu ni Mwenye Nguvu, Mwenye Hekima.

يَعْلَمُ الْمُفْسِدَ مِنَ الْمُصْلِحِ طَوْلَ شَاءَ اللَّهُ لَا عَنْتَكُمْ طَ اِنَّ اللَّهَ عَزِيزٌ حَكِيمٌ^②

2:221 **Wala** msiwaoe wanawake washirikina mpaka waamini. Na hakika, mjakazi muumini ni bora kulilko mshrikina hata kama akiwavutia; na msiwaoze (wanawake waislamu) wanaume washirikina mpaka waamini. Na hakika, mtumwa mwanamume Muumini ni bora kuliko mshrikina,^③ hata kama akiwavutia. Hao wanaitia kwenye moto, na Mwenyezi Mungu anaitia kwenye pepo na msamaha kwa idhini yake; na anabainisha aya zake kwa watu ili wapate kunasihika.

وَلَا تُنَشِّكُهُوَالشُّرِيكَتِ حَتَّىٰ يُؤْمِنَ طَوْلَ مُشْرِكَةٍ وَلَا مَهْمَةٌ مُؤْمِنَةٌ حَيْثُ مِنْ مُشْرِكَةٍ وَلَوْأَعْجَبَتُمْ وَلَا تُنَشِّكُهُوَالشُّرِيكَيْنِ حَتَّىٰ يُؤْمِنَا طَوْلَ مُؤْمِنَ حَيْثُ مِنْ مُشْرِكٍ وَلَوْأَعْجَبَكُمْ أُولَئِكَ يَدْعُونَ إِلَى النَّارِ طَوْلَ مُشْرِكَةٍ وَاللَّهُ يَدْعُو إِلَى الْجَنَّةِ وَالْمُغْفَرَةِ بِإِذْنِهِ طَوْلَ مُشْرِكَةٍ وَيَبْيَسِينَ أَيْتِهِ لِلنَّاسِ لَعَلَّهُمْ يَتَذَكَّرُونَ^٤

2:222 **Na** wanakuuliza kuhusu hedhi. Sema “ni uchafu, basi jitengeni na wanawake wakati wa hedhi, na wala msiwakaribie mpaka watoharike.^④ Watakapokuwa wametoharika

وَيَسْأَلُوكُمْ عَنِ السَّجْعِينِ قُلْ هُوَ آذَنِي فَاعْتَزِلُوا النِّسَاءَ فِي الْمَحِيطِ وَلَا تَقْرُبُوهُنَّ حَتَّىٰ يَطْهُرُنَّ فَإِذَا تَطَهَّرْنَ

Mada

- Kuoana na mwanaume au mwanamke mshrikina ni haramu kabisa
- Sheria zinazohusiana na hedhi

Maoni

^① Kauli hii ni pana zaidi na inatosha katika kutoa muongozo kwa nyanja nyingi za Maisha. Katika jambo lolote ambalo linaweza kukusanywa ndani yake nia nzuri na mbaya, huenda watu wasijue kuhusu nia mbaya ya mtu lakini Mwenyezi Mungu Mtukufu anajua.

^② Kwa isivyo bahati, Pamoja na amri hii ya wazi ya Qur'an, mwenendo wa wanaume wa Kiislamu kuoa wanawake washirikina na wanawake wa Kiislamu kuolewa na makafiri unazidi kuongezeka. Lawama inawaangukia wahalifu na wazazi wao ambao kwa hiyari yao wamewatia watoto wao katika moto huu. Lawama pia zipo kwa watu wanaojiita wasomi, wafuasi wa uhuru, na waandishi wasio na dini ambao wanaunga mkono mila hii kwa kutia giza kurasa kwa maandishi yao.

^③ Ni haramu kuwaingilia wanawake katika hedhi zao. Ama kuzungumza nao na kula nao, na hata kula walichobakiza kwenye sahani zao, inaruhusiwa.

kabisa waendeeni kama vile Mwenyezi Mungu alivyowaamrisha. Na hakika Mwenyezi Mungu huwapenda wanaotubu sana, na huwapenda wanao takasika.

2:223 **Wake** zenu ni shamba lenu, basi njoomi kwenye shamba lenu kama mpendavyo^①, na jitangulizieni kheri nafsi zenu. Na mumche Mwenyezi Mungu na mjue kuwa mtakutana naye. Na (Ewe Mtume kipenzi) wape bishara waumini.

2:224 **Na** msilifanye jina la Mwenyezi Mungu kwa ajili ya viapo vyenu kuwa kizuizi katika kufanya mema na kuwa wachamungu na kupatanisha baina ya watu^②. Na Mwenyezi Mungu ni Mwenye Kusikia na Mwenye Kujua.

2:225 **Na** Mwenyezi Mungu hatawajibisheni kwa viapo vinyoyotolewa bila kukusudia^③, lakini atakushikeni kwa yale ambayo nyoyo zenu zimekusudia. Na Mwenyezi Mungu ni Mwingi wa Kusamehe, Mpole.

2:226 **Na** wale wanaoapa kuwa watajitenga na wake zao, wana muhula wa miezi minne; kama

فَاتُوهُنَّ مِنْ حَيْثُ أَمْرَكُمُ اللَّهُ طِ إِنَّ اللَّهَ يُحِبُّ التَّوَابِينَ وَ
يُحِبُّ الْمُسْتَهْرِئِينَ ^{٣٣}

نِسَاءٌ كُمْ حَرَثُكُمْ فَاتُوا حَرَثَكُمْ أَقْبَلْتُمْ وَ
قَدْرُ مُوَالَانْفِسِكُمْ وَاتَّقُوا اللَّهَ وَاعْلَمُوا أَنَّكُمْ مُلَاقُوهُ
وَبَشِّرُ الْمُؤْمِنِينَ ^{٣٤}

وَلَا تَجْعَلُوا اللَّهَ عُرْضَةً لِّا يُبَانِكُمْ أَنْ تَبْرُوَا وَ
تَتَّقُوا وَتُصْلِحُوا بَيْنَ النَّاسِ طِ وَاللَّهُ سَيِّدُ عَلِيهِمْ ^{٣٥}

لَا يُؤَاخِذُكُمُ اللَّهُ بِاللَّغْوِ فِي أَيْمَانِكُمْ وَلِكُنْ يُؤَاخِذُكُمْ
بِمَا كَسَبْتُ قُلُوبُكُمْ طِ وَاللَّهُ عَفُورٌ حَلِيمٌ ^{٣٦}

لِلَّذِينَ يُؤْلُونَ مِنْ نِسَاءِهِمْ تَرْبُصُ أَرْبَعَةُ أَشْهُرٍ ^{٣٧}

Mada

- Muongozo unaohusiana na mambo ya ndoa na amri ya kutenda mema.
- Kukataza kula kiapo cha kutotenda mema.
- Kiapo cha uongo kina malipo ya adhabu.
- Sheria za Kiislamu kwa wale wanaokula kiapo cha kutojamiiiana na wake zao (Ilā).

Maoni

^① Namna zote za kujamiiiana kwa uke, kwa mkeo, zinaruhusiwa.

^② Kama mtu akila kiapo ili kujiepusha na jambo jema, basi avunje kiapo hicho kwa kutenda wema na atoe kafara.

^③ Mtu hatakiwi kula viapo kupita kiasi. Kuna baadhi wana mazoea ya kutoa viapo, kwa kujua au kutokujua bila kujali ukweli na uwongo wa maneno yale. Hii haipendezi kabisa.

wakirudi ndani ya wakati huu basi Mwenyezi Mungu ni Mwingi wa Kusamehe, Mwenye Kurehemu.^①

2:227 Na wakiazimia kuwapa talaka basi Mwenyezi Mungu ni Mwenye Kusikia, Mwenye Kujua.

2:228 Na wanawake walioachwa wajizuie mpaka hedhi tatu zipite. Wala hairuhusiwi wao kuficha alichoumba Mwenyezi Mungu katika matumbo yao ikiwa wanamuamini Mwenyezi Mungu na siku ya Kiyama. Na waume zao wana haki ya kuwarejesha ndani ya muda huu kama wakitaka kufanya sulhu.^② Kwa mujibu wa sheria, wanawake wana haki juu ya wanaume kama ilivyo wao (wanaume) juu ya wanawake, na wanaume wana daraja zaidi kuliko wao. Na Mwenyezi Mungu ni Mwenye Kushinda, Mwenye Hekima.

٢٨
ج

2:229 Talaka ni mara mbili, kisha ni kushikilia kwa wema au kuachana kwa vizuri.^③ Na wala hairuhusiwi kuchukua chochote katika mlichowapa (wanawake), isipokuwa ikiwa wote

فَإِنْ فَآعْمُوا الظَّلَاقَ فَإِنَّ اللَّهَ سَيِّدُ الْعَالَمِينَ^{٢٢٧}

وَإِنْ عَزَّ مُوَالَطَّلَاقَ فَإِنَّ اللَّهَ سَيِّدُ الْعَالَمِينَ^{٢٢٨}

وَالْمَطَّلَقُ يَتَرَبَّصُ بِأَنْفُسِهِنَّ ثَلَاثَةُ قُرُونٌ وَلَا يَحْلُّ
لَهُنَّ أُنَيْكِتُمُّ مَا حَكَمَ اللَّهُ فِي أُمُّ حَادِهِنَّ إِنْ كُنَّ يُؤْمِنَّ
بِاللَّهِ وَالْيَوْمِ الْآخِرِ وَبِعُونَتِهِنَّ أَحَقُّ بِرَدَدِهِنَّ فِي ذَلِكَ
إِنْ أَرَادُوا اصْلَاحًا وَلَهُنَّ مِثْلُ الَّذِينَ عَلَيْهِنَّ
بِالْمَعْرُوفِ وَلِلْجَالِ عَلَيْهِنَّ دَرَاجَةٌ وَاللَّهُ عَزِيزٌ
حَكِيمٌ^{٢٢٩}

الظَّلَاقُ مَرْثِنٌ فَإِمْسَاكٌ بِمَعْرُوفٍ أَوْ تَسْرِيْحٌ بِإِحْسَانٍ
وَلَا يَحْلُّ لَكُمْ أَنْ تَأْخُذُوا مِمَّا أَتَيْمُوْهُنَّ شَيْئًا إِلَّا أَنْ

Mada

- Hukumu za muda wa kusubiri wanawake baada ya kupewa talaka (Eda) na kufuta talaka (rujū').
- Idadi ya talaka zinazoweza kubatilishwa.

Maoni

^① Hii inaitwa, *Ilā*, yaani, mume anakula kiapo kuwa hatoshiriki tendo la ndoa na mkewe au hatafanya hivyo kwa miezi minne; kama akivunja kiapo (akajamiihana naye) ndani ya miezi minne, kafara inakuwa ya lazima (na watabaki Pamoja), vinginevyo baada ya miezi minne kupita, mwanamke huyo anakuwa ametalikiwa kwa mujibu wa sheria.

^② Kutokana na maneno ya Aya hii, ni wazi kwamba kwa ajili ya kuunganishwa tena katika talaka inayoweza kubatilishwa, chaguo la mwanamume litatosha (makubaliano ya pande zote si lazima). Kuungana tena kwa ajili ya kulipiza kisasi au kumkandamiza mwanamke ni kitendo kiovu. Isivyo bahati, ujinga wa kuwaresa wanawake na familia zao kupitia ndoa, au kuunganishwa tena kwa nia mbaya ya kulipiza kisasi, bado ipo.

^③ “Kushikilia” maana yake ni kuwarudisha kwa kuungana tena, na kuachana kunamaanisha kuwataliki na kuruhusu muda wa eda kupita. Sheria imeelekeza namna ya adabu katika hali zote mbili; Leo, wengi hufanya kinyume na njia sahihi wanaposhikilia au kutiliki. Mwenyezi Mungu Mtukufu awaongoze.

wawili wakiogopa ya kwamba hawataweza kusimamia mipaka ya Mwenyezi Mungu, Kama mkiogopa kuwa hawataweza kusimamia mipaka ya Mwenyezi Mungu basi hakuna dhambi kwao kwa hiyo (fidia) ambayo mwanamke anaitoa ili apate uhuru. Hii ni mipaka ya Mwenyezi Mungu basi msivuke; na wanaovuka mipaka ya Mwenyezi Mungu, basi hao ni watu madhalimu.

يَخَافَا إِلَّا يُقِيمَاصْحَدُو دَالِهِ طِفَانُ خَفْتُمْ أَلَّا يُقِيمَاصْحَدُو دَالِهِ لَفَلَاجُنَاحَ عَلَيْهِمَا افْتَدَثْ بِهِ تِلْكَ حُدُودُ دَالِهِ فَلَا تَعْتَدُوهَا وَمَنْ يَتَعَدَّ حُدُودُ دَالِهِ فَأُولَئِكَ هُمُ الظَّالِمُونَ ﴿٢﴾

2:230 Ikiwa atamtaliki ‘mara tatu’ basi kisheria huyo mwanamke si halali kwake mpaka aolewe na mwanaume mwingine, ① ikiwa mume wa pili atamtaliki, basi hakuna dhambi kwa wote wawili (mume wa kwanza na mke) kurejeana kama wanadhani wasasimama ndani ya mipaka ya Mwenyezi Mungu. Na hii ndiyo mipaka ya Mwenyezi Mungu anayo ibainisha kwa watu wanaojua.

فَإِنْ طَلَقَهَا فَلَا تَحْلُلْ لَهُ مِنْ بَعْدِ حَتْتِ شَكْرَ حَزْوَجَغَيْرِهِ طِفَانُ طَلَقَهَا فَلَا جُنَاحَ عَلَيْهِمَا أَنْ يَتَرَاجَعَا إِنَّمَا أَنْ يُقِيمَاصْحَدُو دَالِهِ وَتِلْكَ حُدُودُ دَالِهِ يُبَيِّنُهَا الْقُوْمُ مَعْلُومُونَ ﴿٢٣﴾

2:231 Na mtakapowataliki wanawawake na wakakaribia kufikia mwisho wa muda wao (wa eda), warejeeni kwa wema au waachieni kwa wema; na msiwashikilie kuwatia dhiki ili mpate

وَإِذَا طَلَقْتُمُ النِّسَاءَ فَبَلَغْنَ أَجَلَهُنَّ فَآمُسْكُوهُنَّ بِمَعْرُوفٍ أَوْ سَرِّ حُوْهُنَّ بِمَعْرُوفٍ فَلَا تُمْسِكُوهُنَّ ضَرَارًا إِلَّا تَعْتَدُوا وَمَنْ يَفْعَلْ ذَلِكَ فَقَدْ ظَلَمَ نَفْسَهُ طِفَانُ

Mada

- Maelezo kuhusu khul’ah (mwanamke kutoa fidia ili apate uhuru)
- Baada ya talaka tatu, mwanamke haruhusiwi tena kuolewa na mume wa kwanza bila ya kufanya ‘Halalah’ kisheria (mwanamke kuolewa na mume mwingine na kuachwa na kumaliza eda yake).
- Amri ya kutenda wema wakati wa kuacha au kurejea, na kukataza dhulma dhidi ya wanawake.

Maoni

- ① Talaka tatu katika miezi mitatu au ndani ya mwezi mmoja au ndani ya siku moja au ndani ya kikao kimoja au ndani ya sentensi moja; kwa namna yeyote ile talaka zinapita na mke anakuwa haramu juu ya mume. Baada ya talaka tatu, bila kufuata taratibu za kisheria, ni haramu kabisa kwa mwanaume na mwanamke kushiriki tendo la ndoa wao kwa wao; wale watakaokiuka katazo hili na kupambania kurejeana kwao, wote wana dhambi sawa.

kuwadhulumu,^① na atakaye fanya hivyo amejid-hulumu mwenyewe. Na wala msizichukulie Aya za Mwenyezi Mungu kwa maskhara; na mkumbuke neema ya Mwenyezi Mungu iliyo juu yenu, na (mkumbuke) Kitabu na Hekima aliywateremshia ambapo humo anawanasihi. Na mcheni Mwenyezi Mungu na jueni kuwa Mwenyezi Mungu ni Mjuzi wa kila kitu.

وَلَا تَتَخُذْ وَآيِتَ اللَّهِ هُرْزُوا وَادْكُرْ وَانْعَمْتَ اللَّهُ عَلَيْكُمْ وَمَا آتَنَاكُمْ مِنَ الْكِتَبِ وَالْحِكْمَةِ يَعْظِمُكُمْ بِهِ طَوَّقُوا اللَّهَ وَاعْلَمُوا أَنَّ اللَّهَ يَعْلَمُ شَيْئاً عَلَيْهِمْ

٢٩
ج

2:232 Na mtakapowataliki wanawake na wakamaliza muda wa eda yao, basi, (Enyi walezi wa wanawake!) msiwazuie kuolewa na waume zao pale (wote) watapofikia makubaliano kwa kulingana na sheria. Hayo ananasiliwa nayo yule ambaye, mionganoni mwenu anamuamini Mwenyezi Mungu na siku ya Kiyama.^② Haya ni mema zaidi na safi kwenu na Mwenyezi Mungu anajua na nyinyi hamjui.^③

وَإِذَا طَلَقْتُمُ النِّسَاءَ فَبَلَغْنَ أَجَدْهُنَّ فَلَا تَعْصُلُوهُنَّ أَنْ يَئِكُنْ أَرْوَاجَهُنَّ إِذَا تَرَاضُوا بِهِمْ بِالْمَعْرُوفِ ذَلِكَ يُوَعْظِيهِمْ مَنْ كَانَ مِنْكُمْ يُؤْمِنُ بِاللَّهِ وَالْيَوْمِ الْآخِرِ ذَلِكُمْ أَرْكَلُكُمْ وَأَطْهَرُ طَوَّلَهُ يَعْلَمُ وَأَنْتُمْ لَا تَعْلَمُونَ

2:233 Akina mama wanyonyeshe watoto wao

وَالْوَالِدُتُ يُرْضِعُنَ أَوْلَادُهُنَّ حَوْلَيْنِ كَامِلَيْنِ لِسَنِ

Mada

- Wakati mwanaume na mwanamke wanapokubaliana kuoana tena baada ya kutalikiana, basi katika hali nyingi walezi hawana haki ya kupinga bila sababu.
- Baadhi ya hukumu za sheria kuhusiana na mtoto kunyonya

Maoni

^① Mwanamke aliyeachwa, mume ana chaguo la kuungana tena au kutengana kabla muda wa eda kuisha. Ingawa haruhusiwi kutumia haki hii kumdhulumu. Mwenye kufanya hivi anaidhulumu nafsi yake na ni kama anazidhihaki Aya za Mwenyezi Mungu. Watu wanaodhulumu wake zao na kupinga sheria, wakumbuke kuwa hata watu hawatambui, Mwenyezi Mungu Mtukufu hakika anaujua ukweli; Hakika Mwanadamu atajibu kwa Mwenyezi Mungu Mtukufu.

^② Kipindi cha eda cha mwanamke kinapoisha na akanuia kuolewa tena, iwe ni mtu yule yule (ambaye alimpa talaka chini ya talaka tatu) au mtu mwagine, walezi hawana haki ya kupinga kama kuna makubaliano ya pande zote.

^③ Hii inadhihirisha kuwa kufuata sheria hii ni njia bora na yenye usafi zaidi kwenu, kwa sababu mwanamke kutohana na uhusiano wa awali na mume wa kwanza anaweza akatenda dhambi na wakapata aibu na shida wanafamilia wote. Kwa hiyo, wanawake hawapaswi kuzuiwa kufuata chaguzi zao za ndoa (kuolewa tena).

kwa miaka miwili,^① ‘sheria hii ni’ kwa anaetaka kumaliza muda wa kunyonyesha. Baba wa mtoto, kwa mujibu wa ada, ana wajibu wa kuwapatia chakula na mavazi kina mama. Wala halazimishwi mtu ila kwa kadiri ya uwezo wake. Mama asiteswe kwa ajili ya mtoto wake, na baba asiteswe kwa ajili ya mtoto wake,^② na hii ‘sheria’ ni sawa sawa kwa yule anayemuwakilisha baba.^③ Basi ikiwa wazazi wawili wataamua kumuachisha mtoto ziwa kwa makubaliano na kushauriana, basi si dhambi juu yao. Na ikiwa mnataka watoto wenu wanyonyeshwe (na wanawake wengine), basi hakuna dhambi juu yenu endapo tu mnatoa kwa wema vile mlivyoahidi. Na mcheni Mwenyezi Mungu na Mwenyezi Mungu anayaona yote mnayoyatenda.

أَسَادُ أَنْ يُتِمَ الرَّضَاعَةَ طَ وَعَلَى الْمَوْلُودَ لَهُ رَدْ قُهْنَ وَ
كَسُوتُهُنَّ بِالْمَعْرُوفِ لَا تَكُفُ نَفْسٌ إِلَّا وَسَعَهَا
لَا تُقْنَأَ سَرَّ الْدَّاهِيَّ بِوَلَدِهَا وَلَا مُولُودَ لَهُ بِوَلَدِهِ وَعَلَى
الْوَارِثِ مِثْلُ ذَلِكَ فَإِنْ أَسَادَ افْصَالًا عَنْ تَرَاضٍ
مِنْهُمَا وَتَشَوَّرٍ فَلَا جُنَاحَ عَلَيْهِمَا طَ وَإِنْ أَسَادُتُمْ أَنْ
تَسْتَرِضُوا أَوْ لَدْ كُمْ فَلَا جُنَاحَ عَلَيْكُمْ إِذَا سَلَّمْتُمْ مَا
أَتَيْتُمْ بِالْمَعْرُوفِ طَ وَاتَّقُوا اللَّهَ وَاعْلَمُوا أَنَّ اللَّهَ بِهَا
تَعْمَلُونَ بِصَيْرٍ

2:234 **Wale** wanaokufa mionganini mwenu na wakaacha wake, hawa wake wajizue muda wa miezi minne na siku kumi.^④ Na wanapotimiza eda yao basi ‘Enyi walezi’ hapana ubaya kwenu kwa yale wanawake wanayojifanyia wenyewe

وَالَّذِينَ يُتَوَفَّونَ مِنْكُمْ وَبَيْنَ رُوُنَ آزْوَاجًا يَتَرَبَّصُنَ
بِأَنْفُسِهِنَّ أَرْبَعَةَ أَشْهُرٍ وَعَشْرًا فَإِذَا بَلَغُنَ أَجَلَهُنَّ
فَلَا جُنَاحَ عَلَيْكُمْ فِيمَا فَعَلْنَ فِي أَنْفُسِهِنَّ بِالْمَعْرُوفِ

Mada

■ Muda wa eda ya mjane

Maoni

^① Kwa maelezo zaidi ya sheria zinazohusu kumnyonyesha mtoto angalia Tafsiri ya sirat ‘al-Jinān’
^② Kumtesa mama ni kumlazimisha kunyonyesha na kumtesa baba ni kumkalifisha zaidi ya uwezo wake. Au maana yake ni kuwa mama asimtese mtoto wala baba. Mama kumtesa mtoto ni kutompa maziwa kwa wakati, au kutomuangalia vizuri, au kumuacha baada ya mtoto kumzoea. Na baba kumtesa mtoto ni kumtenganisha na mama aliyemzoea au kutotekeleza haki za mama kwa namna ambayo kwamba inaweza kumdhuru mtoto.

^③ Ikiwa baba amefariki, majukumu yake yanakabidhiwa kwa anayemwakilisha.

^④ Aya hii inabainisha kuwa muda wa eda ya mjane ni miezi minne na siku kumi; inakuwa hivi ikiwa atakufa siku ya kwanza ya mwezi mwandamo, vinginevyo muda utakuwa siku 130. (Angalia Tafsiri ya Sirat ‘al-Jinān’ kwa maelezo zaidi).

kwa mujibu wa sheria.^① Na Mwenyezi Mungu anajua munayoyatenda.

وَاللَّهُ يِبَاتُعْمَلُونَ خَيْرٌ^{٣٣٣}

2:235 Na wala hakuna dhambi juu yenu kupeleka posa kwa wanawake kwa ishara au mkayaficha moyoni mwenu. Mwenyezi Mungu anajua kuwa mtawataja, hata hivyo, msiwape ahadi kwa siri, isipokuwa semeni yale yaliyo katika sheria; na wala msiazimie kufunga ndoa mpaka kilichoandikwa (mda wa eda) kifike mda wake (wa kukamilika). Na jueni kuwa Mwenyezi Mungu anajua yaliyo ndani ya miyo yenu, basi mcheni yeye, na jueni kuwa Mwenyezi Mungu ni Mwingi wa Kusamehe, Mpole.^②

٢
١٢

وَلَا جُنَاحَ عَلَيْكُمْ فِيمَا عَرَضْتُمْ إِنْ خُطْبَةَ النِّسَاءِ أَوْ
أَكْتَبْتُمْ فِي آنفِسِكُمْ وَعَلِمَ اللَّهُ أَنَّكُمْ سَتَذَكُرُونَ هُنَّ وَ
لَكُنْ لَا تُؤْتُوا عِدْوَهُنَّ سِرًا إِلَّا أَنْ تَقُولُوا قَوْلًا مَعْرُوفًا وَ
لَا تَعْرِمُوا عَقْدَةَ النِّكَاحِ حَتَّى يَبْلُغَ الْكِتَبُ أَجَلَهُ وَ
أَعْلَمُو أَنَّ اللَّهَ يَعْلَمُ مَا فِي آنفِسِكُمْ فَاحْذَرُوهُ وَاعْلَمُو أَ
أَنَّ اللَّهَ غَفُورٌ حَلِيلٌ^{٣٣٤}

2:236 Mkiwapa talaka wanawake, hakuna sharti juu yenu maadamu hamjawagusa au kuwabainishia mahari na wapeni cha kuwaliwaza (nguo moja iliyokamilika)^③. Ni lazima kwa tajiri kutoa kulingana na uwezo wake na maskini kutoa kulingana na uwezo

لَا جُنَاحَ عَلَيْكُمْ إِنْ طَلَقْتُمُ النِّسَاءَ مَا مُحِمِّلُهُنَّ أَوْ
تَفِرِضُوا لَهُنَّ فَرِيضَةً وَمَيْتُوْهُنَّ عَلَى الْمُؤْسَعِ
قَدْرُهُ وَعَلَى الْمُقْتَرِقَدِرَهُ مَتَاعًا بِالْمَعْرُوفِ^{٣٣٥}

Mada

- Hukumu ya sheria zinazohusiana na ndoa kwa mjane katika kipindi cha kukaa eda
- Hukumu za sheria kuhusiana na mahari ya mwanamke.

Maoni

^① Wanawake wana haki ya kuamua mambo yao binafsi ndani ya mipaka ya sheria na hivyo, wanaweza kumchagua wenyewe wanaemtaka kuolewa nae, ingawa, kushauriana ni bora zaidi.

^② Kuoa, au kuposa waziwazi, au kutoa ahadi ya ndoa kwa mjane wakati wa muda wake wa eda ni haramu. Hata hivyo, kudhihirisha nia ya kutaka kuoa kwa ishara kwa kuzingazlia sheria si dhambi, kwa mfano kusema "Wewe ni mwanamke mwema sana" au kuweka tu nia ndani ya moyo bila ya kudhihirisha.

^③ Aya hii inabainisha kanuni chache kuhusu mahari. (Angalia Tafsiri ya Sirat al-Jinān kwa maelzo zaidi).

wake. Maliwaza kwa mujibu wa Sheria.^① Hii ni wajibu juu ya wafanyao mema.

حَقًا عَلَى الْمُحْسِنِينَ^②

2:237 Na kama mkiwapa talaka (wanawake) kabla ya kuwagusa (kuwaingilia) na mumeshawawekeea mahari pia, basi malipo ya nusu ya mahari mliongwa ni wajibu isipokuwa kama mwanamke atasamehe (sehemu ya mahari) au yeye (mume), ambaye mkono wake unashikilia kifungo cha ndoa, hutoa zaidi. (Enyi wanaume) utoaji wenu wa zaidi ni karibu na uchamungu.^② Na wala msisahau wema baina yenu. Hakika, Mwenyezi Mungu anaona yote mnayoyatenda.^③

وَإِنْ طَلَّقْتُمُوهُنَّ مِنْ قَبْلِ أَنْ تَمْسُوهُنَّ وَقَدْ فَرَضْتُمْ
لَهُنَّ فَرِيْضَةً فَصُفْ مَا فَرَضْتُمْ إِلَّا أَنْ يَعْفُونَ أَوْ يَعْفُوا
الَّذِي يَبِدِّعُ عَقْدَةَ النِّكَاحِ وَأَنْ تَعْفُوا أَقْرَبُ لِتَقْوَىٰ
وَلَا تَشْوِيْ الفَضْلَ بِيَكْلُمْ إِنَّ اللَّهَ يُحِبُّ الْمُعْلَمَينَ^④

2:238 **Zilindeni** Sala zote na haswa Sala ya katikati; na simameni kwa ajili ya Mwenyezi Mungu kwa unyenyekevu.

لَحْظُوا عَلَى الصَّلَوَاتِ وَالصَّلُوْةِ الْوُسْطِيِّ وَقُوْمُوا بِهِ
قِبَّيْنِ^⑤

2:239 **Ikiwa** muna khofu basi Kwa kutembea kwa miguu au mukiwa mmeepanda

فَإِنْ حِفْتُمْ فَرِجَالًا أَوْ رُكْبَانًا حَفَّذَ آمِنْتُمْ فَادْكُرُوا اللَّهَ^⑥

Mada

- Marufuku ya kuendeleza uadui baada ya talaka.
- Kwa ujumla kuchunga nyakati zote za sala na hasa sala ya Alasiri.
- Hukumu ya sheria kuhusu sala wakati wa hofu na njia zake.

Maoni

^① Aya hizi zinaangazia umuhimu wa elimu ya fiqhi, kwani haihusiani tu na maelezo ya sheria za ibada ('Ibādāt) ila pia inaongelea mambo yanayohusu maisha ya wanadamu (mu'āmalāt) kama vile biashara, ndoa, talaka, na urithi.

^② Msamaha kwa upande wa mwanamke ina maana kuwa asamehe nusu au mahari yote, ambapo kwa mume, inamaanisha asitake kurudishwa nusu ikiwa ameshatoa mahari kamili. "Kutoa zaidi," ina maanisha kutoa mahari kamili badala ya kutoa nusu.

^③ Suala la talaka ni kubwa sana ambapo kawaida pande zote hupofushwa na tamaa ya kulipiza kisasi, na wanaweza hata kutaka kuuana. Mwenyezi Mungu Mtukufu amelizungumzia hili kwa kuhimiza kuheshimiana katika hali hii, na haswa kwa mwanaume kwani mara nyingi madhara zaidi hutoka kwa mwanaume na familia yake.

(Swalini vile muwezavyo)^① kisha mukiwa katika amani, mkumbukeni Mwenyezi Mungu kama alivyokufundisheni yale muliokuwa hamuyajui.

2:240 Na wale mionganini mwenu wanaokufa huku wameacha wake, wausie kwa ajili ya wake zao kupata matumizi kwa muda wa mwaka mmoja bila ya kuwatoa ‘majumbani mwao’^② na kama wakiondoka kwa hiyari yao, basi hapana ubaya kwenu kwa yale wanayojifanyia wenyewe kwa mujibu wa sheria; na Mwenyezi Mungu ni Mwenye^③ Nguvu, Mwenye Hekima.

2:241 Na wanawake waliopewa talaka wapewe cha kuwalizaza kwa mujibu wa sheria.^④ Haya ni wajibu kwa wachamungu.

2:242 *Hivyo* Mwenyezi Mungu anakubainishieni Aya zake kwa uwazi ili mpate kufahamu

2:243 *Ewe* Mtume Kipenzi, hukuwaona wale waliotoka majumbani mwao kwa maelfu

كَمَا عَلِمْنَا مَا لَمْ تَكُونُوا تَعْلَمُونَ^{٢٣٩}

وَالَّذِينَ يُتَوَفَّوْنَ مِنْكُمْ وَيَرَوْنَ أَرْوَاجًا^{٢٤٠}
وَصَيَّةً لِأَرْوَاجِهِمْ مَتَاعًا إِلَى الْحَوْلِ غَيْرَ اخْرَاجٍ فَإِنْ
خَرَجْنَ فَلَا جُنَاحَ عَلَيْكُمْ فِي مَا فَعَلْنَ فِي أَنْفُسِهِنَّ مِنْ
مَعْرُوفٍ طَوَّلَ اللَّهُ عَزِيزٌ حَكِيمٌ^{٢٤١}

وَلِلَّهِ طَلَقْتِ مَتَاعًا بِالْمَعْرُوفِ حَقًا عَلَى النَّفِيقِينَ^{٢٤٢}

كُنْدِلَكْ بُيَّبِنَ اللَّهُ لَكُمْ أَيْتَهُ لَعَلَّكُمْ تَعْقِلُونَ^{٢٤٣}

أَكْمَلَ تَرَائِي الَّذِينَ خَرَجُوا مِنْ دِيَارِهِمْ وَهُمْ أُلُوفٌ^{٢٤٤}

Mada

- Hukumu iliyobadilishwa kuwa mwanaume anayekufa lazima amuachie pesa za chakula na matumizi ya mwaka mmoja mjane wake.
- Wajibu wa mume kutoa pesa za chakula na matumizi kwa mwanamke katika kipindi cha kukaa eda baada ya talaka.
- Madhumuni ya kutaja hukumu za eda na talaka
- Maelezo ya Waisraeli waliokimbia kwa kuogopa kifo

Maoni

^① Hapa imetajwa hukmu na njia ya kuswali katika hali ya hofu (maadui, Wanyama pori nk.) kama ilivyoeliza; kama hali ya hofu itasababisha kushindwa kukaa sehemu moja kwa swala, lazima ifanywe kwa kutembea au juu ya kipando, kwa njia yoyote ile inayowezekana.

^② Nyakati za mwanzo za Uislamu, muda wa eda ya mjane ulikuwa ni mwaka mzima. Anakaa nyumbani kwa mume wake mwaka mzima na kupokea pesa za chakula na matumizi. Hukumu ya kukaa eda mwaka mmoja ikabadilishwa na aya ya 234 ya Suratul Baqarah na hukumu ya kupewa pesa za chakula na matumizi kwa mwaka mzima ikabadilishwa baadaye kwa Aya ya urithi 12 ya Surat Annisaa.

^③ Neno hili limetoka kwa neno عزير ambalo lina maana tofauti kama vile mwenye kuheshimiwa, mwenye nguvu, na mwenye utukufu.

^④ Kwenye Aya hii inaelezwa wazi kuwa kipindi cha kukaa eda ya talaka, mume ana wajibu wa kutoa pesa za chakula na matumizi kwa mwanamke (mtaliki). Angalia Bahār-e-Shari'at Toleo la 2, Sehemu ya 8, "Taarifa za uboreshaji" kwa maelezo zaidi.

kwa kukhofia kifo? Basi Mwenyezi Mungu aliwaambia, "Kufeni"^①. Kisha akawapa maisha (tena). Hakika, Mwenyezi Mungu ni mwenye fadhila juu ya watu lakini wengi wa watu hawashukuru.

2:244 Na piganeni katika njia ya Mwenyezi Mungu na jueni kuwa Mwenyezi Mungu ni Mwenye Kusikia, Mwenye Kujua.

2:245 Ni nani atakaemkopesha Mwenyezi Mungu^② mkopo mwema, ili Mwenyezi Mungu amzidishie mzidisho mwangi? Na Mwenyezi Mungu hupunguza na kuzidisha; na kwake mtarejeshwa

2:246 Mtume Kipenzi, Je, hukuona kundi katika Wana wa Israeli, baada ya nyakati za Musa?^③ Pale walipomwambia Mtume wao, "Tuwекee mfalme ili tupigane katika njia ya Mwenyezi Mungu Je, Haitokuwa hivi, kama Jihadi ikiwijibishwa juu yenu basi hamtopigana Jihadi?" Wakasema," Kwa nini tusipigane katika njia ya Mwenyezi Mungu wakati

حَذَرَ الْمُؤْمِنُ فَقَالَ لَهُمُ اللَّهُ مُوْتَوْا ثُمَّ أَحْيَهُمْ إِنَّ اللَّهَ لَذُو قُصْلٍ عَلَى النَّاسِ وَلِكُنَّ أَكْثَرَ النَّاسِ لَا يَشْكُرُونَ^{٣٣}

وَقَاتَلُوا فِي سَبِيلِ اللَّهِ وَاعْلَمُوا أَنَّ اللَّهَ سَيِّدُ عَلَيْهِمْ^{٣٤}

مَنْ ذَا الَّذِي يُقْرِضُ اللَّهَ قَرْضًا حَسَنًا فَيُضِعَفَهُ لَهُ أَضْعَافًا

كَثِيرًا طَّوَالُهُ يَقْعِضُ وَيَبْطُطُ وَإِلَيْهِ تُرْجَعُونَ^{٣٥}

أَلَمْ تَرَ إِلَيَّ الْمُلَائِكَةِ مِنْ بَنِي إِسْرَائِيلَ مِنْ بَعْدِ مُوسَى مُرَادٌ

قَالُوا إِنَّا لَهُمْ بَعْثَلَنَّا مِلَكًا نَقَاتِلُ فِي سَبِيلِ اللَّهِ قَالَ

هُلْ عَسِيْتُمْ إِنْ كُتِبَ عَلَيْكُمُ الْقِتَالُ أَلَا تَقَاتِلُنَا طَقَلُوا

وَمَا نَا أَلَّا نَقَاتِلَ فِي سَبِيلِ اللَّهِ وَقَدْ أُخْرِجْنَا مِنْ

Mada

- Amri ya kufanya Jihadi katika njia ya Mwenyezi Mungu Mtukufu.
- Uhamasishaji wa kutumia katika njia ya Mwenyezi Mungu Mtukufu kwa ikhlasi na faida za kufanya hivyo.
- Kuwajibishwa kufanya Jihadi kwa Wana wa Israeli baada ya Nabii Musa عليه السلام na mwenendo wao.

Maoni

^① Hali hii inaelezewa jinsi mtu asivyoweza kujiokoa mwenyewe kwa kukimbia kutokana na hofu ya kifo, haina maana; kifo kilichoandikwa kitakuja kutokea tu. Mwanadamu anatakiwa kuridhika na matakwa ya Mwenyezi Mungu Mtukufu.

^② Kutumia katika njia ya Mwenyezi Mungu Mtukufu kwa ikhlasi kumefananishwa na mkopo; huu ni ukarimu wa hali ya juu kabisa wa Mwenyezi Mungu, kwani Mwanadamu ni kiumbe chake na mali ya mwanadadamu inatokana na Neema zake, Mwenyezi Mungu Mtukufu ndiye Mmiliki wa kweli, ambapo mwanadadamu ana umiliki kwa sababu ya neema za Mungu na bado mwanadadamu kutoa kwake kwa njia ya Mwenyezi Mungu Mtukufu, imeelezwa kuwa ni mkopo (mzuri).

^③ Baada ya kutolewa amri ya Jihadi imetajwa simulizi ya kuvutia inayoamsha ujasiri wa kufanya Jihadi.

Tumetolewa majumbani kwetu na watoto wetu.”^① Basi Jihadi ilipowajibishwa juu yao, waligeuka isipokuwa wachache tu miongan mwao. Na Mwenyezi Mungu anawajua vyema madhalimu.

2:247 Na Nabii wao akawaambia, “Hakika Mwenyezi Mungu amemfanya Ṭālūt kuwa mfalme wenu,”^② Wakasema. “Vipi atakuwa na ufalme juu yetu, na hali sisi tunastahili Ufalme zaidi kuliko yeye naye hakupewa wasaa wa mali.” Akasema, “Mwenyezi Mungu amemchagua yeye juu yenu na amemzidishia ukunjufu wa elimu na mwili.” Na Mwenyezi Mungu humpa ufalme wake yeyote amtakaye. Na Mwenyezi Mungu ni Mwenye wasaa, Mjuzi.

2:248 Na Nabii wao akawaambia, “Alama ya ufalme wake ni hii, kuwa itakujieni sanduku ambalo ndani yake mna utulivu wa nyoyo kutoka kwa Mola wenu Mlezi, na mabaki yale^③ yaliyoachwa kwa Mtukufu Musa na

﴿ دِيَارِنَا وَأَبْنَاءِنَا فَلَمَّا كُتِبَ عَلَيْهِمُ الْقِتَالُ تَوَلَّوْا إِلَّا قَلِيلًا مِّنْهُمْ طَوَّاهُ اللَّهُ عَلَيْهِم بِالظَّلَمِ إِنَّمَا يُنَزَّلُ مِنَ الْكِتَابِ مَا يُنَزَّلُ بِالْحِقْدَانِ ﴾

وَقَالَ لَهُمْ نَبِيُّهُمْ إِنَّ اللَّهَ قَدْ بَعَثَ لَكُمْ طَائُوتَ مَلِكًا قَالُوا أَنِّي يَكُونُ لَهُ الْمُلْكُ عَلَيْنَا وَنَحْنُ أَحَقُّ بِالْمُلْكِ مِنْهُ وَلَمْ يُؤْتَ سَعَةً مِّنَ الْمَالِ قَالَ إِنَّ اللَّهَ أَصْطَفَهُ عَلَيْكُمْ وَرَادَهُ بَسْطَةً فِي الْعِلْمِ وَالْجُسْمِ وَاللَّهُ يُؤْتِ مُلْكَهُ مَنْ يَشَاءُ طَوَّاهُ اللَّهُ وَاسْعَ عَلَيْهِمْ ﴿٢٤٧﴾

وَقَالَ لَهُمْ نَبِيُّهُمْ إِنَّ أَيَّةً مُلِكَهُ أَنْ يَأْتِيَكُمُ التَّابُوتُ فِيهِ سَكِينَةٌ مِّنْ رَّبِّكُمْ وَبَقِيَّةٌ مِّمَّا تَرَكَ الْمُؤْسِى وَالْهُرُونَ تَحِيلُهُ الْمَلِكَةُ إِنَّ فِي ذَلِكَ لَا يَةً لَّكُمْ

Mada

- Hadithi ya kumfanya Ṭālūt kuwa mfalme wa Waisrael.

Maoni

^① Wakati hali ya Imani na matendo ya Taifa inaharibika, mataifa yenyenye dhulma yanaachiliwa juu yao. Kwa kuzingatia Aya hii, mtu akitazama hali ya uharibifu wa imani na matendo ya Waislamu duniani kote huona uakisi wake wa wazi kabisa. Malengo ya Qur'an tukufu kwa masimilizi kama haya, si kwa madhumuni ya kihistoria tu, bali, lazima mtu pia ajifunze na kutafakari.

^② Neno (بَعْثَتْ) maana yake halisi ni kufanya kitu kisimame, ingawa, maana yake hubadilika kwa muktadha; hapa hili neno lina maana ya kutuma.

^③ Vitu vinavyomilikiwa na viumbe vipenzi vya Mwenyezi Mungu Mtukufu ni vitakatifu kama viatu vilivyobarikiwa vya Nabii Musa عَلَيْهِ السَّلَامُ kwenye sanduku (miongan mwa vitu vingine) ambavyo vilikuwa ni sababu ya baraka.

Mtukufu Harun^①, yamebebwa na Malaika. Hakika, kwenye hili kuna ishara kubwa kwenu, ikiwa nyinyi ni waumini.”

2:249 Basi Ṭālūt alipoondoka mjini na majeshi, alisema, “Hakika, Mwenyezi Mungu atawajaribu kwa mto,^② basi yejote atakayekunywa humo, hayupo pamoja nami, na asiyekunywa yu pamoja nami, isipokuwa atakaeteka kiasi cha konzi kwa mkono wake, basi walikunywa wote humo isipokuwa wachache tu mionganoni mwao. Kisha alipovuka mto (Ṭālūt) na waumini pamoja nae, walisema, “Sisi leo hii hatuna nguvu ya kumkabili Jalut na majeshi yake.” (Lakini) walio na yakini kuwa watakutana na Mwenyezi Mungu walisema, “Mara nydingi kundi dogo limeshinda kundi kubwa kwa amri ya Mwenyezi Mungu.^③ Na Mwenyezi Mungu yuko pamoja na wanaosubiri”

إِنْ كُنْتُمْ مُّؤْمِنِينَ ﴿٢٦﴾

٢٦

فَلَمَّا فَصَلَ طَلْوُتُ بِالْجُنُودِ قَالَ إِنَّ اللَّهَ مُبْتَلِيْكُمْ بِنَهْرٍ
فَمَنْ شَرِبَ مِنْهُ فَلَيْسَ مِنِّي ۝ وَ مَنْ لَمْ يَطْعَمْهُ فَإِنَّهُ
مِنِّي ۝ إِلَّا مَنِ اغْتَرَّ فَعْرَفَ بِيَهَا ۝ فَشَرِبُوا مِنْهُ إِلَّا قَلِيلًا
مِنْهُمْ فَلَمَّا جَاءَهُوَ وَالنِّينَ أَمْسَأَ مَعَهُ لَقَلُوًّا لَّا طَاقَةَ
لَنَّا لِيَوْمٍ بِجَالُوتٍ وَ جُنُودِهِ ۝ قَالَ الَّذِينَ يَظْنُونَ أَنَّهُمْ
مُّلْقُو اللَّهِ لَمْ مِنْ فِئَةٍ قَلِيلَةٌ غَلَبَتْ فِئَةً كَثِيرَةً بِإِذْنِ
اللَّهِ ۝ وَاللَّهُ مَعَ الصَّابِرِينَ ﴿٢٧﴾

Mada

- Jaribio la maji ya mto lililowakabili jeshi la Ṭālūt wakati wa safari ya Jihadi

Maoni

^① Baadhi ya wanavyuoni wanasesma kuwa Taboot-e-Sakinah, ilikuwa na mabaki ya wanazuoni wa taifa la Nabii Musa na Harun^{عليه السلام} kwa hiyo kwa neno ”ال“ wamekusudiwa hawa wanavyuoni, ambapo wengine wameelezea kuwa ni vitu vitakatifu vya Nabii Musa^{عليه السلام} na Harun^{عليه السلام}; na neno ”ال“ lilinasabishwa kwao kama ishara ya heshima.

^② Kisa hiki kinaleza jinsi ilivyo bora kuwajaribu watu kabla ya Jihadi, kwani kurudi nyuma au uoga wowote katikati ya vita kunaweza kuleta janga. Na ndio sababu ya kufanya mazoezi ya kina kwa jeshi na kuijandaa wakati wa amani kabla ya vita. Na pia kupitia mitihani midogo kabla ya mtihani mkubwa, huimarisha ujasiri wa mtu.

^③ Ikhlasi, shauku na hima ni sababu za kupata msaada wa Mwenyezi Mungu Mtukufu. Katika historia ya Kiislamu kuna mifano mingi ya makundi madogo kushinda makundi makubwa kama kwenye vita ya Badri ambapo Waislamu 313 walishinda kundi kubwa la makafiri karibu elfu moja. Katika vita vya Yarmūk, takriban Waislamu 50,000 walishinda jeshi la watu milioni moja.

2:250 Na walipomkabili Jalut na majeshi yake walisema, "Ewe Mola wetu Mlezi! Tumiminie subira na isimamishe imara miguu yetu na utunusuru dhidi ya kaumu ya makafiri."^①

2:251 Basi wakawashinda kwa idhini ya Mwenyezi Mungu. Na Dāwūd alimuua Jālūt na Mwenyezi Mungu akampa Ufalme na Hekima na akamfundisha aliyyotaka. Na lau kuwa Mwenyezi Mungu hawapambanishi watu kwa watu, basi hakika, ardhi ingeliharibika.^② Lakini, Mwenyezi Mungu ni mwenye fadhila juu ya walimwengu wote.

2:252 Hizi ni Aya za Mwenyezi Mungu, ambazo 'Mtume Kipenzi' Tunakusomea kwa haki. Na hakika, wewe ni mionganoni mwa Mitume.

وَلَمَّا بَرَزَ الْجَلُوتُ وَجْنُودُهُ قَالُوا إِنَّا أَفْرَغْنَا عَلَيْنَا
صَبَرًا وَثِقْتُمْ أَقْدَامَنَا وَأَنْصَرْنَا عَلَى الْقَوْمِ الْكُفَّارِينَ^{٢٥٣}

فَهَرَّ مُؤْمِنٌ بِإِذْنِ اللَّهِ قَدْ وَقْتَلَ دَاؤُدْ جَلُوتَ وَاتَّهَدَ اللَّهُ
الْمُلْكُ وَالْحِكْمَةُ وَعَلَيْهِ مِمَّا يَشَاءُ طَوْلَةً لَدْفَعَ اللَّهُ
النَّاسَ بَعْضَهُمْ بِعَيْنٍ لَفَسَدَتِ الْأَرْضُ وَلِكَنَّ اللَّهَ ذُو
فَضْلٍ عَلَى الْعَلَمِيَّنَ^{٢٥٤}

تِلْكَ أَيُّهُنَّ نَتْلُوهَا عَلَيْكَ بِالْحَقِّ طَوْلَةً لَمِنَ
الْبُرُّ سَلِينَ^{٢٥٥}

Mada

- Dua ya subira na uthabiti, na msaada wakati wa vita dhidi ya Jālūt na jeshi lake.
- Kushindwa kwa Jālūt na jeshi lake, kifo cha Jālūt; Mtume Dāwūd عَلَيْهِ السَّلَامُ akapewa Ufalme, Hekima na Elimu.
- Kuzuia ujisadi ni moja ya hekima za Jihadi
- Uthibitisho wa Utume wa Mtume Kipenzi صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ

Maoni

^① Kwenye vita, mtu asitegemee vitenda kazi tu bali anatakiwa kumuomba Mwenyezi Mungu Mtukufu subira, uthabiti na usaidizi dhidi ya adui ili apate msaada wa Mwenyezi Mungu Mtukufu.

^② Hapa imetajwa hekima ya Jihadi; Jihadi ina faida nyingi. Ikiwa magugu hayakung'olewa mazao huharibiwa, ikiwa molekuli ya kansa haijaa ndolewa, mwili utateseka, kama mwizi asipokamatwa, hakutakuwa na usalama; vivo hivyo ikiwa waasi hawajadhibitiwa kupitia Jihadi, watu wema wataishi kwa shida.

2:253 **Hao** ndio Mitume;^① tumewafadhilisha baadhi yao juu ya wengine; mionganoni mwao kuna ambaye Mwenyezi Mungu alisema nae, na kuna ambaye akamnyanya daraja nyingi juu ya wote.^② Na tukampa Isa mwana wa Maryam ishara zilizo wazi na tukamnusuru kwa Roho Takatifu. **Na** lau kama Mwenyezi Mungu angetaka wasingepigana walio kuwa baada yao baada ya kuwajia ishara zilizo wazi, lakini walihitalifiana, basi wapo kati yao walibakia kuwa waumini, na wengine wakawa makafiri. Na lau Mwenyezi Mungu angetaka, wasingepigana; lakini Mwenyezi Mungu hufanya atakavyo.^③

تَلْكَ الرُّسُلُ فَصَلَّيْنَا بَعْضُهُمْ عَلَى بَعْضٍ مِّنْهُمْ مَّنْ كَلَمَ اللَّهُ وَرَأَفَعَ بَعْضُهُمْ دَرَاجَتٍ وَاتَّبَعْنَا عَبِيسَى ابْنَ مَرْيَمَ الْبَيْتَ وَأَيَّدْنَاهُ بِرُوحِ الْقُدُسِ وَلَكَ شَاءَ اللَّهُ مَا أَقْتَلَ الَّذِينَ مِنْ بَعْدِهِمْ مَّنْ بَعْدِ مَا جَاءَ عَتْهُمُ الْبَيْتُ وَلَكِنْ أَخْتَلَعُوا فِيهِمْ مَّنْ أَمْنَ وَمِنْهُمْ مَّنْ كَفَرَ وَلَكَ شَاءَ اللَّهُ مَا أَقْتَلَتُو وَلَكِنَّ اللَّهَ يَعْلَمُ مَا يُرِيدُ

2:254 **Enyi** mlionamini! Toeni (kwenye njia ya Mwenyezi Mungu) katika riziki tulioaruzuku, kabla ya kufika Siku ambayo hapatakuwa na biashara, wala urafiki, wala uombezi (kwa makafiri)^④ Na makafiri ndio madhalimu.^⑤

يَا أَيُّهَا الَّذِينَ آمَنُوا إِنْفَقُوا مِمَّا رَزَقْنَاكُمْ مِّنْ قَبْلِ أَنْ يَأْتِيَ يَوْمٌ لَّا يَبْيَعُ فِيهِ وَلَا خَلَةٌ وَلَا شَفَاعَةٌ وَالْكُفَّارُ وَنَّهُمُ الظَّالِمُونَ

Mada

- Hadhi na ukuu wa Mitume na ubora wa Mitume watatu.
- Mwenyezi Mungu Mtukufu hufanya atakavyo.
- Kujiandaa kwa ajili ya Akhera kwa kutoa katika njia ya Mwenyezi Mungu Mtukufu.

Maoni

- ① Neno 'Rusul' ni wingi wa rasul (mjumbe).
- ② Mitume wote ni sawa katika utume. Hata hivyo, wengine wana cheo cha juu zaidi kuliko wengine. Na Nabii wa Mwisho Mtume wetu صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ ana daraja la juu zaidi kushinda wote.
- ③ Mwenyezi Mungu Mtukufu hufanya atakavyo; hakuna anaeweza kufanya chochote kinyume na matakwa yake katika utawala wake. Tumeamrishwa kusalimu amri kwa amri yake na kutenda kulingana na maamrisho yake.
- ④ Siku ya hesabu, mali iliotumika katika mema ndio itakayonufaisha, vivyo hivyo marafiki wema ndiyo pekee watakao mnufaisha mtu. Na uombezi pia utakuwepo kwa idhini ya Mwenyezi Mungu Mtukufu lakini kwa ajili ya Waislamu tu.
- ⑤ 'ظُلْمٌ' (dhulma au uonevu) maana yake halisi ni kuweka kitu pasi na mahala pake. Makafiri kuchukua ukafiri badala ya Imani, dhambi badala ya utiifu, na kukufuru badala ya kushukuru, ni dhulma yao. Kwa kuwa aina mbaya zaidi ya dhulma imetajwa katika Aya hii, makafiri wameitwa kuwa wao ndio madhalimu.

2:255 Mwenyezi Mungu, hapana mungu apasaye kuabudiwa kwa haki ila Yeye.^① Aliye hai, Mwenye Kuwasimamia wote. Hashikwi na kusinzia wala halali. Vilivyomo mbinguni na vilivyomo ardhini vyote ni vyake. Nani anawenza kuombea katika mahakama yake bila ya idhini yake? Anajua yaliyo mbele yao na yaliyo nyuma yao; na wao hawawezi kujua chochote kutokana na elimu yake ila kwa atakalo mwenyewe. Kiti chake kimeenea mbingu na ardhi; ulinzi wao hauwezi kumletea uchovu, na Yeye ndiye Aliyetukuka, Aliye Mkuu

اللَّهُ لَا إِلَهَ إِلَّا هُوَ حَمْدُ الْحَمْدُ لِلَّهِ سَنَةٌ وَسَنَةٌ
لَا تُؤْمِنُ طَلَةٌ مَا فِي السَّمَاوَاتِ وَمَا فِي الْأَرْضِ طَلَةٌ مَذَا
الَّذِي يَشْفَعُ عِنْدَهُ إِلَّا بِذِنِهِ طَعْلَمَ مَا بَيْنَ أَيْدِيهِمْ
وَمَا خَلْقُهُمْ وَلَا يُحِيطُونَ بِشَيْءٍ مِنْ عِلْمِهِ إِلَّا بِإِشَاعَةِ
وَسَعَ كُرْسِيُّهُ السَّمَاوَاتِ وَالْأَرْضَ وَلَا يَوْدُهُ حَفْظُهُمْ
وَهُوَ عَلَىٰ الْعَظِيمُ^{٥٥}

2:256 Hakuna kulazimisha katika dini.^② **Hakika** uwongofu umepambanuka na upotofu; kwa hiyo, **anayemkataa** shetani na kumuamini Mwenyezi Mungu, basi huyo ameshikilia kishikizo imara ambacho hakivunjiki. ^③ Na Mwenyezi Mungu ni Mwenye Kusikia, Mwenye Kujua.

لَا إِكْرَاهٌ فِي الدِّينِ قُلْ تَبَّيَّنَ الرُّشْدُ مِنَ الْغَيْرِ
فَمَنْ يَكْفُرُ بِالظَّاغُوتِ وَيُؤْمِنُ بِاللَّهِ فَقَدِ اسْتَوْسَكَ
بِالْعُرُورِ وَأَنْوَثَقَ لَا إِنْفِصَامَ لَهَا وَاللَّهُ سَيِّدُ الْعَالَمِينَ^{٥٦}

Mada

- Mambo muhimu ya kuhusiana na Uungu yametajwa katika Aya hii (Āyah al-Kursiyy).
- Hakuna kulazimisha katika kukubali dini.
- Uongofu umepambanuka vizuri na upotofu kwa Qur'an Tukufu.
- Ni muhimu kuwaepuka waovu na wapotovu ili kubaki imara juu ya Uislamu.

Maoni

- ① Aya hii inajulikana kama Āyat al-Kursiyy. Inafafanua Imani za msingi kuhusu Mwenyezi Mungu Mtukufu. Na kila mtu akitafakari zaidi katika aya hii imani zinazohusiana naye hubainika zaidi kwake.
- ② Kumbuka, asiyé Muislamu hawezi kulazimishwa Kusilimu, lakini muislamu anayejaribu kuacha uislamu atazuiliwa kinguvu kwani hii ni kudharau na kuvunja heshima uislamu na unapelekea machafuko na kuvuruga muundo wa jamii.
- ③ Kila mtu mpotovu na muovu huitwa al-Tāghūt. Neno hili linatumika pia kumaanisha shetani, mwaguzi, mchawi na sanamu. Katika Aya hii imeagizwa kujiepusha na al-Tāghūt kwasababu hawezi kubaki imara juu ya Uislamu ila yule ambaye atajiepusha kukaa na wapotovu, kusoma vitabu vyao na kusikiliza maneno yao, kwani mwenye kuendelea kuipigia kisu kamba yake ya imani utakuja wakati kamba yake itakatika.

2:257 Mwenyezi Mungu ndiye Mlinzi wa walio amini; Anawatoa kwenye giza na kuwain-giza kwenye nuru.^① Na walio kufuru walinzi wao ni mashetani, wanawatoa kwenye nuru na kuwaingiza gizani; Hao ndiyo watu wa Motoni watakaa humo milele.

اللَّهُ وَلِيُ الَّذِينَ آمَنُوا لَا يُخْرِجُهُم مِّنَ الظُّلْمَةِ
إِلَى النُّورِ هُوَ الَّذِينَ كَفَرُوا أَوْ لَيْلَهُمُ الطَّاغُوتُ
يُخْرِجُونَهُم مِّنَ النُّورِ إِلَى الظُّلْمَةِ طَوْلِيَّكَ
أَصْحَابُ النَّارِ هُمْ فِيهَا خَلِدُونَ^②

٢٣

2:258 Mtume Kipenzi, hukumuona yule aliyejohiana na Ibrahim kuhusu Mola wake Mlezi kwa sababu Mwenyezi Mungu alimpa Ufalme? Ibrahim aliposema “Mola wangu Mlezi ndiye anayehuisha na anayefisha.” Akasema, “Hata mimi nahuisha na kufisha”, Ibrahim akasema, “Mwenyezi Mungu hulichomozesha jua mashariki, basi wewe lichomozeshe magharibi” basi kafiri yule akafedheheka^② na Mwenyezi Mungu hawaongoi Madhalimu.

الَّمَّا تَرَى الَّذِي حَاجَ إِبْرَاهِيمَ فِي سَرِّهِ أَنَّ اللَّهَ أَنْشَأَ اللَّهُ
الْمُلْكَ إِذْ قَالَ إِبْرَاهِيمَ رَبِّيَ الَّذِي يُحِبُّ وَيُبِتُّ
قَالَ أَنَا أُحِبُّ وَأُمِيتُ قَالَ إِبْرَاهِيمَ فَإِنَّ اللَّهَ
يَأْتِي بِالشَّمْسِ مِنَ الْمِشْرِقِ فَاتِّبِعْهَا مِنَ الْمَغْرِبِ
فَبِهِتَ الَّذِي كَفَرَ طَوْلِيَّهُ لَا يَهْدِي الْقَوْمَ الظَّلِيمِينَ^③

٢٤

2:259 Au (hukumuona) yule aliyepita karibu na mji uliokwisha kuwa magofu.^③ Akasesma, “Mwenyezi Mungu ataufufuaje mji huu baada ya kufa kwake?” Basi Mwenyezi Mungu akamfisha kwa miaka mia kisha akamfufua. Akamuuliza, “Vipi umekaa hapa kwa muda gani?” Akajib; “Nimekaa hapa kwa siku moja

أَوْ كَالَّذِي مَرَّ عَلَى قَرْبَيْهِ وَهُوَ خَاوِيَّةٌ عَلَى عُرُوفِ شَهَادَةِ قَالَ
أَنِّي يُحِبُّ هَذِهِ الْأَنْوَافَ بَعْدَ مَوْنَهَا فَأَمَاتَهُ اللَّهُ مَائَةً عَامَّاً
ثُمَّ بَعْثَةَ طَقَالَ كَمْ لَبِثْتَ طَقَالَ لَبِثْتَ يَوْمًا أَوْ بَعْضَ
يَوْمٍ طَقَالَ بَلَ لَبِثْتَ مِائَةً عَامَّاً فَانْظُرْ إِلَى طَعَامَكَ وَ

٢٥

Mada

- Mwenyezi Mungu Mtukufu ndiye Mlinzi wa Waislamu, na Mashetani ni wasaidizi wa makafiri
- Mahojiano kati ya Mtume ibrahim عَلَيْهِ السَّلَامُ na Mfalme Namrūd.
- Kifo cha Nabii ‘Uzayr عَلَيْهِ السَّلَامُ na ufufuo wake

Maoni

- ① Giza linahusu ukafiri na nuru inahusu Imani; kwa kuwa kuna aina nyingi za ukafiri, na Uislamu ni dini moja, neno la Kiarabu katika Aya lenye maana ya nuru limetumika la umoja na lenye maana ya giza limetumika la wingi.
- ② Huu ni Ushahidi wa mjadala wa haki katika akida na imani; hii ndiyo njia ya Mitume, kwa hiyo mjadala wa namna hii si mbaya. Ama tabia mbaya zinazohusiana na mjadala kama kuonyesha kiburi, kufanya uadui na kutokubali ukweli ndizo ambazo wamezikataa wanavyuoni watukufu.
- ③ Kwa mujibu wa wanavyuoni wengi wa Tafsiri, mtu huyo ni Nabii ‘Uzayr عَلَيْهِ السَّلَامُ na mji ni Jerusalem.

au sehemu tu katika siku”, Akasema “(Hapana) bali umekaa hapa miaka mia moja, hebu angalia chakula chako na kinywaji chako, bado havijatoa harufu mbaya, na mtazame punda wako (aliyekuwa ameoza) na (yote haya yalifanyika) ili tukufanye uwe ni Ishara kwa watu. Na itazame jinsi tutavyoinua mifupa na kuivesha nyama”. Basi (hili suala) lilipomdhihirikia, akasema; “Najua kwamba Mwenyezi Mungu ni Muweza juu ya kila kitu.”

2:260 Na Ibrahim aliposema, Ewe Mola wangu Mlezi, nionyeshe jinsi utakavyowafufua wafu? Mwenyezi Mungu akasema, “Je, huna yakini?” Ibrahim akasema, “Bila ya shaka, lakini nataka moyo wangu upate utulivu”^① Mwenyezi Mungu akasema, “Chukua ndege wanne na uwazoezeshe kwako, kisha weka kipande cha kila mmoja wao juu ya kila mlima kisha waite, watakujia kwa haraka. Na jua kuwa Mwenyezi Mungu ni Mwenye nguvu, Mwenye hekima. ^②

2:261 **Mfano** wa wanaotoa mali katika njia ya Mwenyezi Mungu ni kama mfano wa punje

شَرِّا إِكَ لَمْ يَتَسَنَّهُ وَانْظُرْ إِلَى حَمَارِكَ قَتْ وَلَنْجَعَلَكَ
أَيَّةً لِّتَنَاسٍ وَانْظُرْ إِلَى الْعُظَامِ كَيْفَ تُنْشِرُ هَاشَمَ نَجْسُوْهَا
لَحْبَانًا طَفَلَةً أَتَبَيَّنَ لَهُ قَالَ أَعْلَمُ أَنَّ اللَّهَ عَلَى كُلِّ شَيْءٍ
قَدِيرٌ^③

فَإِذْ قَالَ إِبْرَاهِيمُ سَرِّبْ أَرِنِي كَيْفَ تُحْمِي الْبَوْنَى طَقَالَ
أَوَلَمْ تُؤْمِنْ طَقَالَ بَلِي وَلَكِنْ لَيَطْمَئِنَّ قَلْبِي طَقَالَ
فَخُذْ أَرْبَعَةً مِّنَ الطَّيْرِ فَصُرْهُنَّ إِلَيْكَ ثُمَّ اجْعَلْ عَلَى كُلِّ
جَبَلٍ مِّنْهُنَّ جُرْعَاءً ثُمَّ ادْعُهُنَّ يَا تَبَيَّنَ كَسْعَيَا طَوْأَلْمَ
أَنَّ اللَّهَ عَزِيزٌ حَكِيمٌ^④

مَثْلُ الَّذِينَ يُنْقُضُونَ أَمْوَالَهُمْ فِي سَبِيلِ اللَّهِ كَمْثُلَ حَبَّةٍ

Mada

- Kisa cha Nabii Ibrāhīm عَلَيْهِ السَّلَام na ndege wanne kuhuishwa.
- Mfano wa wanaotoa katika njia ya Mwenyezi Mungu.

Maoni

- ① Aya hii inasimulia simulizi ya ufufuo ambayo inaelezea Nguvu kubwa ya Mwenyezi Mungu Mtukufu.
- ② Hili linadhihirisha ukweli kwamba Manabii na Mitume wana daraja kubwa kwenye Mahakama ya Mwenyezi Mungu Mtukufu kwa sababu Mwenyezi Mungu Mtukufu hutekeleza matakwa yao na hujibu maombi yao kiasi cha kuwahuisha wafu kwa dua zao.

iliyotoa^① mashuke saba, katika kila shuke zimo punje mia; na Mwenyezi Mungu humzidishia amtakaye. Na Mwenyezi Mungu ni Mwenye wasaa, Mjuzi. ^②

أَنْبَتْتُ سَبْعَ سَنَابِلَ فِي كُلِّ سُبْلَةٍ مِائَةً حَبَّةً طَوَّ وَاللهُ يُصْعِفُ لِمَنْ يَشَاءُ طَوَّ وَاللهُ وَاسْعَ عَلَيْمٌ ^(٦١)

2:262 **Wale** wanaotoa mali katika njia ya Mwenyezi Mungu, kisha hawafuatishi walichotoa kwa kukumbusha hisani wala kwa maudhi,^③ basi ujira wao uko kwa Mola wao Mlezi; na wala hawatakuwa na hofu wala hawatahuzunika.

أَلَّذِينَ يُنْفِقُونَ أَمْوَالَهُمْ فِي سَبِيلِ اللَّهِ شَمَّ لَا يُنْهَى عَوْنَ مَا أَنْفَقُوا مَنَّا وَلَا آذَى لَهُمْ أَجْرُهُمْ عِنْدَ رَبِّهِمْ وَلَا خُوفٌ عَلَيْهِمْ وَلَا هُمْ يَحْزُنُونَ ^(٦٢)

2:263 **Neno** jema na msamaha ni bora kuliko sadaka inayofuatiwa na maudhi. Na Mwenyezi Mungu ni Mwenye kujitosha, Mpole.

قَوْلٌ مَعْرُوفٌ وَمَغْفِرَةٌ خَيْرٌ مِنْ صَدَقَةٍ يَتَّبَعُهَا آذَى وَاللهُ عَنِّي حَلِيمٌ ^(٦٣)

2:264 **Enyi** Mlioamnini! Msibatilishe sadaka zenu kwa kukumbusha hisani^④ na maudhi, **kama yule** anayetoa mali yake kwa kuwaonyesha watu na wala hamuamini

يَا أَيُّهَا الَّذِينَ آمَنُوا لَا تُطْلُو أَصْدَاقَتُمْ بِالْمِنْ وَلَا آذَى كَالَّذِي يُنْفِقُ مَالَهُ سِرَاعَةَ النَّاسِ وَلَا يُؤْمِنُ

Mada

- Masharti mawili ya kukubaliwa sadaka; Kutomkumbusha mtu hisani na kutomuudhi.
- Neno jema ni bora kuliko kuudhi baada ya kutoa sadaka.
- Kukatazwa kubatilisha Sadaka kwa kukumbushana neema na kuudhi.
- Mfano wa watoao sadaka kwa kujionyesha.

Maoni

^① Aya hii inataja sadaka kwa ujumla, bila ya kukhususisha sadaka za wajibu au za hiyari. Kutoa katika jambo lolote jema ni kutoa katika njia ya Mwenyezi Mungu Mtukufu, mfano kumsaidia mwanachuoni au mwanafunzi au kumnunulua mtu maskini chakula, mavazi, dawa au kutimiza mahitaji yake.

^② Matendo mema ni sawa. Ingawa thawabu yake hutofautiana kulingana na iklasi ya mtu na nia yake.

^③ Hairuhusiwi kabisa kumkumbusha mpokeaji sadaka hisani na kumuudhi; kukumbusha hisani ni kuelezea msaada mbele ya wengine na kumuaibisha. Na kumuudhi ni kusema, “Ulikuwa mtu maskini, ulifilisika na mhiti sana, nikakushika mkono na nikakusaidea” au kwa kumshinikiza.

^④ Kama mwenye kuomba asipopewa chochote, basi angalau aongeleshwe kwa uzuri ili asiudhike. Ikiwa anasisitiza au kutumia lugha ya matusi, msamehe. Ni bora mtu asitoe chochote na aseme kwa uzuri na kusamehe makosa kuliko kutoa sadaka kisha kumuaibisha aliyepewa mbele ya wengine na kumuudhi.

Mwenyezi Mungu na Siku ya Mwisho; mfano wake ni kama jabali laini ambalo juu yake kuna udongo, likanyeshewa na mvua kubwa ikalia-chacha jabali safi; watu hawa hawatokuwa na mamlaka juu ya chochote walichokichuma katika matendo yao ① na Mwenyezi Mungu hawaongoi makafiri.

بِاللَّهِ وَالْيَوْمِ الْآخِرِ فَسَلَّمَ كَمَثُلِ صَفْوَانِ عَلَيْهِ
تُرَابٌ فَأَصَابَهُ وَأِلْفَ فَتَرَ كَهْ سَلْدَانًا لَا يَقْدِرُونَ
عَلَى شَيْءٍ مِّمَّا كَسَبُوا وَاللَّهُ لَا يَهْدِي النَّاسَ
الْكُفَّارِينَ ②

2:265 **Mfano** wa wale wanaotoa mali zao kwa kutafuta radhi za Mwenyezi Mungu na kuzipa nguvu roho zao, ni kama mfano wa bustani iliyo mahali pa juu; ikaifikia mvua kubwa basi ikazalisha matunda maradufu. Ikiwa haifikiwi na mvua kubwa, basi mvua nyepesi hutosha, na Mwenyezi Mungu anayaona yote mnayo-fanya. ③

وَمَثْلُ الَّذِينَ يُنْفِقُونَ أَمْوَالَهُمْ أَبْغَاءَ مَرْضَاتِ اللَّهِ
وَتَشْبِيهُتَا مِنْ أَنْفُسِهِمْ كَمَثُلِ جَنَّةٍ بِرَبُوٰةٍ أَصَابَهَا
وَأِلْفَ فَاتَتْ أَكْلَهَا ضُعْفَيْنِ ۝ قَاتِلٌ لَمْ يُصِبْهَا وَأِلْفَ قَاتِلٌ
وَاللَّهُ يَعْلَمُ بِمَا تَعْمَلُونَ بَصِيرٌ ④

2:266 **Je**, kuna yeote mionganini mwenu angependa kuwa na bustani ya mitende na mizabibu ipitayo mito kati yake, anayo ndani yake kuna kila aina ya matunda; na uzee umemfikia na ana watoto wanyonge, kisha ikashambuliwa na kimbunga cha moto,

أَيُّهُدُّ أَحَدُ كُمْ أَنْ تَكُونَ لَهُ جَنَّةٌ مِّنْ تَخْيِيلٍ وَأَعْنَابٍ
تَجْرِي مِنْ تَحْتِهَا الْأَنْهَرُ لَهُ فِيهَا مِنْ كُلِّ الشَّرَابِ
وَأَصَابَهُ الْكَبَرُ وَلَهُ ذِرَاءٌ صَعَافَاءٌ فَأَصَابَهَا آغْصَاصٌ

Mada

- Mfano wa wanao toa sadaka kwa kutaka radhi ya Mwenyezi Mungu Mtukufu.
- Mfano wa wale wanaotoa sadaka kwa kujionyesha.

Maoni

① Kutoa sadaka kwa uwazi na kwa siri inaruhusiwa, lakini mtu anatakiwa kuzingatia hali ya moyo. Kwa isivyo bahati, matendo maovu kama kujionyesha, kukumbushana hisani na kuudhi yameenea katika jamii zetu. Kutumia mabango au kuchapisha Habari na picha kutangaza sadaka za mtu limekuwa jambo la kawaida. Vivo hivyo, ikiwa mtu atamsaidia mwana familia, atamshinikiza Maisha yake yote na kumdhalilisha mbele ya wengine vile atakavyo. Hiki ni kitendo kiovu kabisa.

② Aya hii inasimulia mfano wa wale ambaa hutoa kwa ajili ya kutaka radhi za Mwenyezi Mungu tu, na kuwa na msimamo juu ya imani. kama vile ardhi yenye rutuba inavyozaa matunda iwe mvua kubwa au nyepesi, ndiyoo sadaka ya ikhlasi inaongezwa na Mwenyezi Mungu Mtukufu ikiwa ni kiasi kikubwa au kidogo. Katika baraza la Mwenyezi Mungu Mtukufu hali ya moyo inazingatiwa, sio tu kiasi cha mali.

hiyo bustani nzima ikaungua. Hivyo, Mwenyezi Mungu anakubainishieni Aya zake ili mpate kutafakari. ①

فِيهِ نَارٌ فَاحْتَرَقُتْ كَذِلِكَ يُبَيِّنُ اللَّهُ لَكُمُ الْآيَتِ
لَعَلَّكُمْ تَتَبَكَّرُونَ ۝

٣٦

2:267 Enyi mliaoamini! Toeni katika njia ya Mwenyezi Mungu katika vile vizuri mlivyovichuma na katika vile tulivyokutoleeni katika ardhii, na msikusudie (kutoa) vilivyo vibaya hali nyinyi wenyewe (lau mungevipewa) musingevipokea ila kwa kufumba macho. ② Na mujue kuwa Mwenyezi Mungu ni Mwenye kujitosha, na Mwenye Kusifiwa,

يَا أَيُّهَا النَّاسُ إِذَا أَنْفَقُوا مِنْ طَبِيعَتِهِمْ
وَمِمَّا أَخْرَجَ جَنَانَكُمْ مِّنَ الْأَرْضِ وَلَا تَمِيمُوا الْحَيَاةَ
مِنْهُ تُنْفِقُونَ وَلَسْتُمْ بِإِخْرَاجِهِ إِلَّا أَنْ تَعْمَضُوا فِيهِ
وَاعْلَمُوا أَنَّ اللَّهَ عَنِّي حَيْدُرٌ

2:268 Shetani anakutieni khofu ya ufukara na anakuamrishi na machafu ③ na Mwenyezi Mungu anakuahidini msamaha na fadhlila kutoka kwake; na Mwenyezi Mungu ni Mwenye wasaa, Mjuzi.

الشَّيْطَانُ يَعْدُ كُمْ أَفْقَرَ وَيَأْمُرُ كُمْ بِالْفَحْشَاءِ وَاللَّهُ
يَعْدُ كُمْ مَغْفِرَةً وَمَهْوَ وَفَضْلًا وَاللَّهُ وَاسِعٌ عَلَيْهِ ۝

2:269 Yeye humpa hekima amtakaye, na aliyepewa hekima, hakika amepewa kheri

يُؤْقَدُ الْحِكْمَةُ مَنْ يَسْأَعُ وَمَنْ يُؤْتَ الْحِكْمَةَ فَقَدْ أُوتَى

Mada

- Amri ya kutoa mali safi na halali katika njia ya Mwenyezi Mungu.
- Katazo la kutoa mali yenye dosari na duni katika njia ya Mwenyezi Mungu Mtukufu.
- Kumtishia mtu anayetoa katika njia ya Mwenyezi Mungu Mtukufu kwa umasikini, ni kazi ya shetani.
- Ubora wa elimu na hekima.

Maoni

① Allahu Akbar! ni mfano wenyewe kuogopesha kiasi gani; ikiwa tu tutaelewa na kuokoa amali zetu, sala, dhikr, usomaji wa Qur'an, kuimba Qasida, Hajj, Umrah na sadaka kutokana na uharibifu wa kujionyesha. Na tuanze kutafakari kuhusu amali zetu.

② Wengi hutumia vitu vizuri kwa ajili yao wenyewe, lakini inapokuja kwenye suala la kutoa katika njia ya Mwenyezi Mungu Mtukufu, wanatoa vitu visiviyotumika au vitu duni. Kuna somo kwenye Aya hii kwa watu kama hao. Kama kitu ni kizuri na mtu hakipendi tu, hakuna madhara kukitoa, ila kama hakipendi kwa sababu siyo kizuri au kina dosari, hilo ni la kulaumiwa.

③ Shetani ananong'oneza kwamba mkitumia au kutoa sadaka mtakuwa masikini au fukara, basi msitoe; Hii ni hila hatari inayotumiwa na shetani dhidi ya wale wanaotoa kwa njia ya Mwenyezi Mungu Mtukufu. Cha kushangaza ni kwamba watu hao hao watatumia kupita kiasi katika mila za ndoa halali na haramu na mambo mengine ya Maisha.

nyingi. Na hawakubali nasaha ila wenye akili.

خَيْرًا كَثِيرًا وَمَا يَذَّكَّرُ إِلَّا مَا لَبَابٌ ⑯

2:270 Na kile mnachotoa au nadhiri mnazoweka, Mwenyezi Mungu anajua. Na madhalimu hawana msaidizi.

وَمَا أَنْفَقْتُمْ مِنْ نَفَقَةٍ أَوْ نَدَرَةٍ تُمْ مَنْ نَذَرْنَا فَإِنَّ اللَّهَ
يَعْلَمُهُ طَ وَمَا الظَّالِمِينَ مِنْ أَنْصَارِي ⑭

2:271 Ikiwa mnatoa sadaka kwa uwazi, basi hiyo ni amali njema ilioje, na kama mkiificha na kuwapa masikini, basi hivyo ni bora kwenu; ① Na Yeye (Mwenyezi Mungu) atawafutia baadhi ya dhambi zenu, na Mwenyezi Mungu anazo habari za matendo yenu.

إِنْ تُبْدِي وَالصَّدَقَاتِ فَنِعْمَاهُنَّ وَإِنْ تُخْفِي هَاوَ تُؤْتُوهَا
الْفَقَرَاءُ أَعْفَهُمْ حَيْرَانٌ لَكُمْ وَيُكَفِّرُ عَنْكُمْ مِنْ سَيِّئَاتِكُمْ
وَإِنَّ اللَّهَ بِمَا تَعْمَلُونَ خَبِيرٌ ⑫

2:272 Si juu yako wewe kuwaongoa, ② hakika Mwenyezi Mungu humuongoa amtakaye. Na kheri yoyote mnayotoa basi hiyo ni faida kwenu. Na toeni kwa kutaka radhi za Mwenyezi Mungu. Na kheri yoyote mtakaotoa mtalipwa kikamilifu, wala hamtadhulumiwa.

لَيْسَ عَلَيْكَ هُدًى لَهُمْ وَلَكِنَّ اللَّهَ يَهْدِي مَنْ يَشَاءُ ط
وَمَا تُنْفِقُوا مِنْ خَيْرٍ فَلَا نُنْقِسُكُمْ وَمَا تُنْفِقُونَ إِلَّا
أَبْتَغَاءَ وَجْهِ اللَّهِ طَ وَمَا تُنْفِقُوا مِنْ خَيْرٍ يُوَفَّ إِلَيْكُمْ
وَأَنْتُمْ لَا تُظْلَمُونَ ⑪

2:273 Kwa mafakiri, waliozuiliwa katika njia ya Mwenyezi Mungu; hawana uwezo wa

لِلْفُقَرَاءِ الَّذِينَ أُحْصِرُوا فِي سَيِّئِ الْأَيَّامِ لَا يَسْتَطِعُونَ

Mada

- Hakuna sadaka wala nadhiri inayofichika kwa Mwenyezi Mungu Mtukufu.
- Kutoa sadaka hadharani au kwa siri inaruhusiwa.
- Kumwongoza mtu ni katika mamlaka ya Mwenyezi Mungu Mtukufu.
- Kutoa sadaka kwa kutaka radhi za Mwenyezi Mungu Mtukufu manufaa yake yanarudi kwa mtoaji.
- Wale masikini amabao hawaombi chochote kwa sababu ya kujiheshimu wanastahili zaidi kupewa sadaka.

Maoni

① Hukumu hii inakusanya takriban amali zote kwamba inaruhusiwa kutenda kwa kudhihirisha na kwa kuficha, lakini kufanya jambo hadharani kwa kujionyesha ni haramu, na kufanya hivyo kwa kuhamasisha wengine ni thawabu. Viongozi wa dini na wanavyuoni wanafanya mambo mengi hadharani ili kuhamasisha wafuasi wao.

② Mtume kipenzi صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ ametumwa kuwa ni mbashiri, mwonyaji, mwitaji anayelingania kwenye wokovu. Wajibu wake unatimizwa kwa kuwalika watu. Kujitahidi zaidi ya hili si wajibu wake.

kusafiri katika ardhi. Asiye wajua huwadhania kuwa ni matajiri kutokana na kukwepa kwao kuomba.^① Utawatambua kwa alama zao; ^② hawang'ang'anali kwa kuomba, na kheri yoyote mnayoitoa basi hakika Mwenyezi Mungu anaijua.

2:274 **Wale** wanaotoa mali zao usiku na mchana kwa siri na dhahiri, watapata malipo kwa Mola wao Mlezi, wala hawatakuwa na hofu wala hawatahuzunika.

2:275 **Wale** wanaokula riba hawatasimama siku ya Kiyama ila kama yule aliyeingiwa na wazimu baada ya kuguswa na shetani. Hayo ni kwa sababu walisema: "Biashara ni kama riba tu" na Mwenyezi Mungu ameihalalisha biashara na ameihamlisha riba. Basi yule aliyefikiwa na mawaidha kutoka kwa Mola wake Mlezi, kisha akaacha, basi yale yalijotangulia ni halali kwake; na jambo lake ni kwa Mwenyezi Mungu. Na wenye kurudia basi

صَرْبًا فِي الْأَرْضِ نُّيَحْسِبُهُمُ الْجَاهِلُ أَغْنِيَاءَ مِنْ
الشَّعْفِ تَعْرِفُهُمْ بِسِيمِهِمْ لَا يَسْكُونَ النَّاسُ الْحَافَّاً
وَمَا تُنْتَقِدُ أَمْنٌ خَيْرٌ فَإِنَّ اللَّهَ بِهِ عَلِيهِمْ^{٢٧٤}

الَّذِينَ يُنْفَقُونَ أَمْوَالَهُمْ بِأَثَلٍ وَالنَّهَايَةُ
عَلَانِيَةٌ فَلَهُمْ أَجْرٌ هُمْ عِنْدَ رَبِّهِمْ وَلَا خُوفٌ عَلَيْهِمْ
وَلَا هُمْ يَحْرَنُونَ^{٢٧٥}

الَّذِينَ يَأْكُلُونَ الرِّبَا لَا يَقُومُونَ إِلَّا كَمَا يَقُولُ
الَّذِي يَتَخَطَّلُهُ الشَّيْطَانُ مِنَ الْمَسِ طَلِكَ بِأَنَّهُمْ
قَالُوا إِنَّمَا الْبَيْعُ مِثْلُ الرِّبَا وَأَحَلَ اللَّهُ الْبَيْعَ وَ حَرَمَ
الرِّبَا فَمَنْ جَاءَهُ مَوْعِظَةٌ مِنْ رَبِّهِ فَأَنْتَ هُنَّ فَلَهُ
مَارِسَلَفٌ وَأَمْرَةٌ إِلَى اللَّهِ وَمَنْ عَادَ فَأُولَئِكَ أَصْحَابُ

Mada

- Malipo ya wanaotoa hadharani na kwa siri.
- Watumiaji riba na matokeo yao.

Maoni

^① Aya hii iliteremshwa kuhusu Maswahaba Ahlu Sufa. Walikuwa takriban maswahaba 400 ambao walifanya Hijrah (uhamiaji) Madinah. Walikuwa hawana makazi, wala familia, Maswahaba ambao hawakuo, ambao walitumia muda wao kuabudu na kusoma. Mchana walijishughulisha na mambo ya Jihadi na wakati wa usiku walikuwa wakijifunza Quran.

^② Hii inajumuisha wanavyuoni, wanafunzi, na wahubiri ambao hawana muda wa kulipwa kutokana na kujitolea kwao kwa huduma ya kidini; hawaombi chochote kutoka kwa watu kwa sababu ya kujheshimu na utu. Takwimu hizo huficha umaskini wao, na kudhaniwa kuwa wanaishi kwa raha, ingawa uhalisia ni kinyume kabisa, ambao baada ya uchunguzi mdogo, hujulikana jinsi Maisha yao yalivyo magumu.

hao ndio watu wa motoni, humo watadumu ①

الَّذِي هُمْ فِيهَا حَلَدُونَ ④

2:276 Mwenyezi Mungu huondoa riba na kuongeza sadaka. Na Mwenyezi Mungu hampendi asiye na shukrani, afanyae dhambi sana.

يَسْأَلُ اللَّهَ الرِّبُّو أَوْ يُرِبِّ الصَّدَقَاتِ ۖ وَاللَّهُ لَا يُحِبُّ
كُلَّ كُفَّارٍ أَثِيمٍ ④

2:277 **Hakika**, wale walioamini na wakatenda mema, na wakasimamisha swala na kutoa Zaka, ujira wao uko kwa Mola Mlezi; hawata-pata hofu wala hawatohuzuniaka.

إِنَّ الَّذِينَ آمَنُوا وَعَمِلُوا الصَّلِحَاتِ وَآتَاهُمُ الصَّلَاةَ
وَأَتُوا الْزَكُوَةَ لَهُمْ أَجْرٌ هُمْ عِنْدَ رَبِّهِمْ ۚ وَلَا خُوفٌ
عَلَيْهِمْ وَلَا هُمْ يَحْرَنُونَ ④

2:278 Enyi mliaoamini! Mcheni Mwenyezi Mungu na acheni riba iliobaki ikiwa nyinyi ni waumini.

يَا أَيُّهَا الَّذِينَ آمَنُوا اتَّقُوا اللَّهَ وَذَرُّوا مَا بَقَى مِنَ
الرِّبَوِ إِنْ كُنْتُمْ مُّؤْمِنِينَ ④

2:279 Na msipotekeleza, basi kuweni na yakini na vita kutoka kwa Mwenyezi Mungu na Mtume wake. Na mukitubu, inaruhusiwa kwenu kuchukua raslimali zenu, ② msimdhulumu

فَإِنْ لَمْ تَفْعَلُوا فَإِنَّا ذُنُوبٌ حَرَبٌ مِّنَ اللَّهِ وَرَسُولِهِ ۝
وَإِنْ تُبْتُمْ فَلَكُمْ رُءُوسُ أَمْوَالِكُمْ ۝ لَا تَتَظَلَّمُونَ وَ

Mada

- Mwenyezi Mungu Mtukufu huharibu riba na kuongeza sadaka.
- Malipo ya matendo ya Waislamu.
- Amri kwa Waislamu kumcha Mwenyezi Mungu Mtukufu na kujiepusha kuchukua riba iliobaki.
- Onyo kali la vita dhidi ya Mwenyezi Mungu Mtukufu na Mtume wake َصَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ kwa wanao kula riba.

Maoni

① Anayekula riba huku akiichukulia kuwa ni halali, ni kafiri kwani hii ni haramu kabisa. Mtu mwenye kuhesabu kitendo chochote cha haramu kuwa halali ni kafiri na atakaa Motoni milele, na mtu anayekula riba huku akijua kuwa ni haramu, ni mtenda dhambi mkubwa na atakaa Motoni kwa muda mrefu sana.

② Hili ni onyo kali. Ni nani mwenye ujasiri hata wa kufikiria kupigana vita na Mwenyezi Mungu Mtukufu na Mtume wake? Ilipoteremka Aya hii, wale Maswahaba waliokuwa wakijihusisha na mambo ya riba waliacha mara moja na wakatubia. Kinyume chake, wanafikra wa Kiislam leo wako katika vita na Mwenyezi Mungu Mtukufu huku wakiandika vitabu na makala kuhusu umuhimu wa riba badala ya kutubia.

wala msidhulumiwe. ①

لَا تُظْلِمُونَ ②

2:280 Ikiwa (mdaiwa) ana shida, basi mpeni muda mpaka apate wepesi; na mkiifanya deni kuwa ni sadaka basi ni bora kwenu, ikiwa mnajua. ②

وَإِنْ كَانَ ذُو عُسْرَةً فَنَظِرَةً إِلَى مَيْسَرَةٍ

وَأَنْ تَصَدِّقُوا خَيْرَكُمْ إِنْ لَمْ تَعْلَمُوهُنَّ ③

2:281 Na iogopeni siku ambayo mtarejeshwa kwa Mwenyezi Mungu, kisha kila nafsi italipwa ilichochuma na wao hawatadhulumiwa.

وَاتَّقُوا يَوْمًا تُرْجَعُونَ فِيهِ إِلَى اللَّهِ شَمَّتْوُ فِي كُلِّ

نَفْسٍ مَا كَسَبْتُ وَهُمْ لَا يُظْلِمُونَ ④

٤٨

2:282 Enyi mliao mini! Mnapokopeshana deni kwa muda uliowekwa, basi andikeni. **Na mwandishi** aandike ‘makubaliano’ baina yenu kwa uadilifu. Wala mwandishi asikatae kuandika, kama alivyomfundisha Mwenyezi Mungu, basi aandike. **Na mwenye haki** (deni) juu yake aandikishe naye amche Mwenyezi Mungu, Mola wake Mlezi; na wala

يَا إِيَّاهَا الَّذِينَ آمَنُوا إِذَا يَئْتِمُ بَدَيْنَ إِلَى أَجَلٍ

مُسَيَّقًا كَتْبُهُ وَلَيَكْتُبَ بِيَمِّكُمْ كَاتِبٌ بِالْعَدْلِ وَلَا

يَابَ كَاتِبٌ أَنْ يَكْتُبَ كَمَا عَلَيْهِ اللَّهُ فَلَيَكْتُبْ وَلَيُبَلِّ

الَّذِي عَلَيْهِ الْحُقْقُ وَلَيَتَقَرَّبَ اللَّهَ رَبَّهُ وَلَا يَبْخَسْ

Mada

- Kuhimiza kuongeza muda kwa mkopaji mwenye shida (mdaiwa) na kusamehe deni.
- Amri ya kuogopa Siku ya kutisha, Siku ya Hukumu.
- Amri ya kuandika mkataba wa deni.
- Mwandishi aandike kwa uadilifu na asikatae kuandika.
- Mkataba uandikwe kwa uadilifu .
- Asiyeweza kuandika aandikishe.
- Baada ha kuandikwa washuhudishwe mashahidi.
- Katika kuandika mkataba kuna faida, liwe deni kubwa au dogo.
- Ikiwa biasahara ni ya mkono kwa mkono basi hakuna ubaya kutoiandika.

Maoni

① Ingawa aya hii inahu riba, lakini kwa ujumla Sheria na akili za kibinadamu pia zinalazimu kuwa dhulma isifanywe wala isivumiliwe; kuwe na juhudhi za kila aina za kukomesha dhulma, kwani wakati mwingine kuvumilia dhulma kunaweza kumpa nguvu dhalimu. Na ikiwa kuna hali ambapo msamaha utasadia, basi msamaha ni bora.

② Ikiwa mkopaji (mdaiwa) yuko kwenya hali ngumu kifedha, basi kumpa muda, au kupunguza deni au hata kulifuta kabisa, ni njia ya kupata ujira mkubwa.

asipunguze chochote ndani yake.^① Basi ikiwa mwenye haki (deni) hana akili au ni dhaifu au mnyonge au hawezi kuandikisha mwenyewe, basi mlinzi wake aandikishe kwa uadilifu. ^② Na mshuhudishe mashahidi wawili katika wanaume wenu, na ikiwa hamna wanaume wawili, basi mwanaume mmoja na wanawake wawili mionganii mwa mashahidi mnaowaridhia, ili (kama) mmoja wa wanawake kati ya hao wawili akisahau, basi mwingine amkumbushe.^③ Na mashahidi wasikatae pale wanapoitwa. Na wala msichoke kuliandika (deni) liwe dogo au kubwa, mpaka muda wake; hii ndiyo njia ya uadilifu zaidi mbele ya Mwenyezi Mungu, na iliyosahihii zaidi kwa ushahidi, na iliyokaribu zaidi kwamba msiwe na shaka (baadae); (andikisheni kila mkataba)^④ isipokuwa kama ni biashara ya mkono kwa mkono baina yenu, basi hakuna dhambi kwenu kwa kutoandika. Na mnapo uziana wekeni mashahidi, wala asidhuriwe mwandishi wala shahidi (au mwandishi wala shahidi asisababishe

مِنْهُ شَيْئًا فَإِنْ كَانَ الَّذِي عَلَيْهِ الْحُقْقَ سَفِيهًا أَوْ ضَعِيفًا
أَوْ لَا يُسْتَطِيعُ أَنْ يُبَلَّ هُوَ فَقِيرٌ لِّلَّهِ بِالْعَدْلِ
وَاسْتَشْهِدُوا شَهِيدًا يُنِ منْ رَاجِلَكُمْ فَإِنْ لَمْ يَكُونَا
رَجُلَيْنِ فَرَجُلٌ وَّ امْرَأَتْنِ مَنْ تَرْضُونَ مِنَ الشَّهِيدَاءِ
أَنْ تَضْلِلَ إِحْدَاهُمَا فَتَنَّكِرَ إِحْدَاهُمَا الْخَرَى وَلَا
يَأْبَ الشَّهِيدَ أَعْرِزَ إِذَا مَادْعُوا وَلَا تَسْعُوا أَنْ تَكْتُبُوهُ
صَغِيرًا أَوْ كَبِيرًا إِلَى آجِلِهِ ذُلْكُمْ أَقْسَطُ عِنْدَ اللَّهِ
وَأَقْوَمُ لِلشَّهَادَةِ وَأَدْعِنَ الْأَتْرَابَوَا إِلَّا أَنْ تَكُونَ
تِجَارَةً حَاضِرَةً تُدِيرُ وَهَا بَيْنَكُمْ فَلَيْسَ عَلَيْكُمْ
جُنَاحٌ أَلَا تَكْتُبُوهَا وَأَشْهِدُوا إِذَا تَبَيَّنَ وَلَا يُضَارَّ

Maoni

^① Ikiwa suala la deni ni la mkopo, au biashara au malipo ya awali ya bidhaa, au kukopesha bidhaa na kupokea malipo baadae au malipo ya awali ya kodi ya nyumba au duka, kwa mambo kama hayo, kuandikishana mkataba ni muhimu. Ingawa hukumu hii siyo ya lazima (wajib) lakini kuizingatia kutamuokoa mtu na matatizo mengi; haswa katika zama zetu, kushikamana na hukumu hii imekuwa muhimu sana.

^② Ikiwa mtu hawezi kuandika, kama vile mtoto, mzee sana au kipofu, basi mtu mwingine anaweza kuchaguliwa kuandika, na mtu atakayechaguliwa kuandika asikatae, kwani huu ni msaada bila hasara yoyote kwa mwandishi; fursa ya kupata thawabu ya bure haipaswi kupuuzwa.

^③ Baada ya kuandika mkataba inatakiwa kuthibitishwa kwa mashahidi ambao wanaweza kuitwa kama ikihitajika. Na mashahidi wawe wawili wa kiume au mwanaume mmoja na wanawake wawili.

^④ Hakuna kinachopaswa kupuuzwa katika kuandika mambo yanayohusiana na deni, liwe kubwa au dogo. Kiwango chake, aina yake na muda wake pia uandikwe. Faida ya mkataba huu ni kwamba, kwanzaa ni jambo la uadilifu mbele ya Mwenyezi Mungu, kwa vile inalinda haki za watu. Pili, hii njia itasaidia kuwarahisishia mashahidi kutoa ushahidi, na tatu, jambo hili litakuwa wazi kwa pande zote mbili na hautapatikana uhasi ndani ya miyo yao.

madhara); na ikiwa mtafanya hivyo basi hakika huu utakuwa uasi wenu. Na mcheni Mwenyezi Mungu; na Mwenyezi Mungu anakufundisheni.^① Na Mwenyezi Mungu ni mjuzi wa kila kitu.

2:283 Na mkiwa safarini na hamkumpata mwandishi, basi kukabidhiwa rahani (na mkopeshaji). Na kama mkiaminiana, basi aliyeaminiwa (mkopaji) arudishe amana ya mwenzake na amche Mwenyezi Mungu, Mola wake Mlezi. **Na wala** msifiche ushahidi, na yejote atakayeuficha basi moyo wake ni wenye kutenda dhambi, na Mwenyezi Mungu ni mjuzi wa mnayoyatenda. ^②

2:284 Vyote vilivyomo mbinguni na vlivyomo ardhini ni vya Mwenyezi Mungu. Na mkidhihirisha yaliyomo miyoni mwenu au mkiyaficha, Mwenyezi Mungu

كَاتِبٌ وَّلَا شَهِيدٌ هُوَ إِنْ تَفْعَلُوا فَإِنَّهُ فُسُوقٌ بِكُمْ

وَاتَّقُوا اللَّهَ طَوْبًا لِّمَنْ يُعِلِّمُ اللَّهُ وَاللَّهُ بِكُلِّ شَيْءٍ عَلَيْهِمْ

وَإِنْ كُنْتُمْ عَلَى سَفَرٍ وَلَمْ تَجِدُوا كَاتِبًا فَهُنَّ مَقْبُوضَةٌ طَوْبًا

فَإِنْ أَمْنَ بَعْضَكُمْ بَعْضًا فَلَيَوْدُ الَّذِي أَعْثَنَ أَمَانَةً

وَلَيُتَّقِ اللَّهُ رَبَّهُ طَوْبًا لَا تَنْتُقُوا الشَّهَادَةَ طَوْبًا وَمَنْ يَكْتُمْهَا

فَإِنَّهُ أَثِمٌ قَلْبُهُ طَوْبًا لِمَنْ يَعْلَمُونَ عَلَيْهِمْ

٢٩

مَا فِي السَّمَاوَاتِ وَمَا فِي الْأَرْضِ طَوْبًا لِمَنْ تُبَدِّلُ وَأَمَانَةً

أَنْفِسَكُمْ أَوْ تُحْفُوهُ بِحَاسِبَكُمْ بِهِ اللَّهُ طَوْبًا لِمَنْ يَشَاءُ

Mada

- Amri ya kuwa na mashahidi wakati wa biashara na kutomdhuru mwandishi wala shahidi.
- Ikiwa mwandisha hatopatikana wakati wa safari, basi kitu kiwekwe rahani.
- Katazo la kuficha ushuhuda.
- Mwenyezi Mungu Mtukufu atawahesabu watu kuhusu matendo na nia zao.

Maoni

^① Neno la Kiarabu ‘يَخَارُ’ linaweza kufasiriwa kwa maana ya ma‘rūf (kitendo ambacho kinajulisha mtendaji) au majhūl (kitendo ambacho hakijulishi mtendaji), ya kwanza ingemaanisha waandishi na mashahidi wasidhuru pande zinazokubaliana, na ya pili ingemaanisha wandishi na mashahidi wasidhuriwe.

^② Zingatia Aya ya 282 na 283; vipi Mwenyezi Mungu Mtukufu ametoa maelekezo ya wazi katika mambo yetu ya kidunia. Hili linadhihirisha ukamilifu wa dini yetu kwani inashughulikia mahitaji yote ya mwanadamu. Kuanzia itikadi, ibada mpaka miamala baina ya watu (mu‘āmalāt). Haki za wanadamu ni muhimu zaidi na hivyo Mwenyezi Mungu Mtukufu amezieleza kwa uwazi. Vile vile, kuna hekima nyingi katika hukumu za sheria ya Uislamu, na zina faida nyingi kwetu.

atakuhesabuni kwayo.^① Kisha amsamehe amtakaye na amuadhibu amtakaye. Na Mwenyezi Mungu ni Muweza juu ya kila kitu.

2:285 **Mtume** ameamini yaliyoteremshwa kwake, kutoka kwa Mola wake Mlezi na Waumini pia. Wote wamemuamini Mwenyezi Mungu, na Malaika wake, na Vitabu vyake, na Mitume wake, (wakisema) hatumtofautishi yeyote katika Mitume wake (katika kuwaamini). Na wakasema; “Ewe Mola Mlezi! Tumesikia na tumetii, tupe msamaha wako na kwako pekee ndiyo marejeo.”

2:286 **Hakika** Mwenyezi Mungu haikalifishi nafsi ila kwa kadiri ya iwezavyo. **Ni** yake faida ya iliyoyachuma na ni juu yake khasara ya iliyoyachuma. ^② **Ewe** Mola wetu Mlezi! Usitushike tukisahau au tukikosea. Ewe Mola wetu Mlezi! Usitubebeshe mzigo mzito kama ulivyowabebesha waliotutangulia, ewe Mola wetu Usitutwike tusiyoyaweza, na utusamehe, na utughufirie, na utuhurumie; Wewe ndiyo Mlinzi wetu, tunusuru dhidi ya kaumu ya makafiri.

وَيُعَذِّبُ مَنْ يَشَاءُ طَوَالِهِ عَلَى كُلِّ شَيْءٍ قَدِيرٌ^{٢٨٣}

أَمَنَ الرَّسُولُ بِمَا أُنْزِلَ إِلَيْهِ مِنْ رَبِّهِ وَالْمُؤْمِنُونَ
كُلُّ أَمَنَ بِاللَّهِ وَمَلِكِتِهِ وَكُتُبِهِ وَرُسُلِهِ قَاتِلُ فَرِيقٍ
بَيْنَ أَحَدٍ مِّنْ رُسُلِهِ قَاتِلُوَا سِعْنَاهُ أَطْعَنَاهُ غُفرانَكَ
رَبَّنَا وَإِلَيْكَ الْمَصِيرُ^{٢٨٤}

لَا يُكَلِّفُ اللَّهُ نَفْسًا إِلَّا وُسْعَهَا طَلَاهَا مَا كَسَبَتْ وَعَلَيْهَا
مَا كَنَسَبَتْ طَلَاهَا لَا تُؤْخَذُنَا إِنَّ نَسِينَا أَوْ أَخْطَانَا
رَبَّنَا وَلَا تَحْمِلْ عَلَيْنَا إِصْرًا كَمَا حَمَلْتَهُ عَلَى النِّسِينَ
مِنْ قَبْلِنَا حَرَبَنَا وَلَا تَحْمِلْنَا مَا لَا طَاقَةَ لَنَا لِهِ وَاعْفُ
عَنَّا وَاغْفِرْ لَنَا وَارْحَمْنَا وَقَنَةَ آنْتَ مَوْلَانَا فَانْصُرْنَا
عَلَى الْقَوْمِ الْكَفَرِينَ^{٢٨٥}

Mada

- Mambo manne yanayohusiana na msingi wa Imani.
- Watu wanaamrisha kulingana na uwezo wao.
- Mtu atapata thawabu kwa matendo mema na atapata adhabu kwa maovu yake mwenyewe.
- Waislamu kufundishwa dua muhimu.

Maoni

^① Binadamu huingwa na aina tofauti za mawazo moyoni mwake, yakiwemo mashaka (wasiwasi), azimio (azma), na nia. Kuepuka mashaka (wasiwasi) ni nje ya uwezo wa mtu binafsi, hivyo hakuna uwajibikaji kwa hilo. Mawazo yanayokubaliwa na moyo wa mtu na ambayo kuna nia ya kutekeleza yatamfanya mtu awajibike; Aya inahusu mawazo hayo iwapo mtu atafichua yaliyomo moyoni mwake au akayaficha, Mwenyezi Mungu Mtukufu atamhesabu mtu kuhusu hayo.

^② Aya hii inahusu malipo na adhabu ya Akhera. Hata hivyo hali kama hii hutokea katika ulimwengu huu pia, kwa ujumla mtu hupata matunda ya jitihada zake; mtu anayefanya kazi kwa bidii hufikia malengo yake, ambapo mtu mvivu hukabiliana na matokeo ya uvivu wake.